ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Pili - Tarehe 11 Mei, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 84

Utaratibu wa Faini za Maegesho za Papo kwa Papo

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny. Mhe. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:-

Kumekuwa na kero kubwa katika eneo la Bandari ya Malindi kwa Askari wa Polisi Jamii kufungia gari zinazodaiwa kuegeshwa nje ya utaratibu. Askari hao wamekuwa wanatoza fedha ya faini ya papo kwa papo ya shilingi 10,000/- ili gari ifunguliwe endapo itafungwa.

Je, kuna sheria au kanuni zinazowapa uwezo Askari wa Polisi Jamii kutoza faini za maegesho za papo kwa papo kwa gari zinazopatikana na makosa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti ahsante, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mwakilishi wa Jimbo la Paje, swali lake namba 84 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, eneo la Bandari ya Malindi ni moja kati ya maeneo yanayotembelewa au kufikiwa na idadi kubwa ya watu wakiwemo wageni na wenyeji. Kwa bahati mbaya sana udogo wa eneo hili ukilinganishwa na harakati zinazofanyika pale unatoa changamoto kubwa za kiusalama hasa kwa watumiaji wa barabara. Pamoja na hatua mbali mbali zinazochukuliwa kupunguza msongamano ikiwemo kuifanya barabara kuwa ya kwenda kwa upande mmoja wa njia moja, bado hali haijatengemaa. Kutofuatwa kwa taratibu za kuegeshwa gari sehemu zinazostahiki kwa kiasi kikubwa kunachangia msongamano uliopo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu fedha wanazotoza Polisi Jamii hasa kwa faini ya papo kwa papo ya shilingi 10,000/ kwa magari yanayofungiwa, Polisi Jamii hao wanafanya hivyo kwa niaba ya Baraza la Manispaa ambapo nao wamepewa uwezo wa kutoza faini chini ya kifungu cha 14(1) cha Sheria ndogo ndogo za Baraza la Manispaa (Sehemu ya Kuegesha magari na Vituo vya Mabasi) ya Mwaka 2002 ahsante.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa mji wetu umekua na kiasi cha kwamba kila eneo halina maeneo ya kuegesha gari rasmi, ukiacha bandarini lakini pia kadhia hii iko katika sehemu kubwa ya Darajani na eneo lile bahati nzuri lilikuwa na maduka yaliyovunjwa, wanapata shida sana kwa msongamano wa magari. Naomba kuiuliza wizara kupitia serikali kwa jumla. Je, kwa kuwa msongamano huu una kero na watu walioko bandarini hutaka kuweka gari zao huku upande mwengine wa Darajani ambako kuna eneo kwa sasa hivi liko wazi linalindwa, serikali haioni kuwe na mpango wa makusudi kulitoa kwa kuwa ujenzi wake bado unangojewa ikatoa utaratibu maalum wa kuweka gari pale ili kunusuru mtiririko wa kusumbua watu na magari yao huko bandarini.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali maarufu Shihata, Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele swali lake moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwanza tukiri na tukubali kama serikali changamoto ambazo zinawakumba madereva mbali mbali, hasa wale ambao wanaingia katika maeneo yetu ya mjini kwa maeneo mengi ya mjini kukosa kuwa na *parking* za uhakika. Lakini tumesikia ushauri wake na mawazo yake, kwa sababu eneo ambalo amelikusudia tayari limeshatengwa kuwa na *project* maalum, bahati nzuri au mbaya *project* ile bado haijaanza rasmi, tutazingatia ushauri wake wakati *project* ile iko mbioni kuanza. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Mji Mkongwe siku hizi hasa mitaa ya kwa Shamsu na Mkunazini kumekuwa na magari yanazuwia *parking* muda wote na zile ni *service area* ambazo mtu unakwenda, unaweka gari, halafu unafanya haja yako unaondoka. Je, wizara yake italisimamia vipi suala hili ili kuonesha huduma nzuri zinapatikana *parking* kwa wote na kwa muda maalum kama wanavyofanya kazi nchi nyengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Kweli kama ambavyo amezungumza Mhe. Mwakilishi kwamba katika baadhi ya mitaa yetu hasa ile ya Mkunazini imekuwa na changamoto kubwa sana ya maegesho ya magari. Hilo kama serikali lazima tukiri, lakini ililolifanya serikali kwa hatua ya kwanza iliona usumbufu ule unaanza kupatikana, zile gereji nyingi zilizokuweko katika maeneo yale hatua ya kwanza ni kuondosha gereji zile katika maeneo ya mjini kwenda katika maeneo ambayo yatakuwa yanastahiki kuwa *located*, ili kupunguza foleni katika maeneo yetu ya mjini.

Jambo la pili ambalo bado sisi madereva wengi tunao kwa sababu barabara ile ni ndogo matumizi na mahitaji ya mitaa ile sasa imezidi kuongezeka, lakini bado utakuta badala ya mtu kuweka gari kwa dharura ya dakika mbili ataweka atakwenda kufanya shughuli zake za siku nzima kitendo ambacho kinatoa usumbufu kwa madereva wengine.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue wazo la Mhe. Mjumbe na tutashauriana na wenzetu wa Manispaa, tutakaa chini ili kuliratibu kutizama namna bora zaidi ili kuwapunguzia madereva wetu na watu wanaomiliki magari usumbufu. Ahsante.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri swali langu liko hivi. Sisi sote ni mashahidi kwamba kuna eneo katika Manispaa ya mji wa Zanzibar pale Darajani, palikuwa pana makontena sasa hivi yameondoshwa makontena yale na sijui lini utaanza ujenzi wa pale. Kutokana na kadhia ya *parking* katika maeneo mbali mbali katika *Stone Town* ile. Je, serikali haioni haja kuwa na *temporary parking* ya pale Darajani kwa muda ambao mpaka watapokuwa tayari kuanza ujenzi wao ikahamishwa ili kuondoa msongamano wa utumiaji wa *parking* kwa wanaoelekea Malindi na Bandarini. Kwa sababu ikikaa pale tayari ile sehemu itakuwa haijakaa bure inafanya kazi, lakini sasa hivi eneo lile limekuwa kama kambi ya Vikosi vya SMZ. Je, serikali haioni sababu maalum kuona kwamba *just* watengeneze ile *temporary parking*.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani Mwakilishi mahiri wa wananchi Jimbo la Jang'ombe, mchapa kazi, mtiifu na tunathamini sana mchango wake.

Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu katika jibu la kwanza la nyongeza alilouliza Mhe. Ali Suleiman Ali, kweli anachokisema ni sahihi lakini bado kwa sababu eneo lina *project* yake maalum na kwa sababu bado *project* haijaanza ipo haja na upo uwezekano wa kuanza kuwa na *temporary parking.* Lakini bado tusubiri tukae na wenzetu walioko *government*, tutizame lini hasa *project* ile itaanza tutakapojua *time* ndio tutajua sasa kama tutakuwa tuna haja ya kuweka *temporary parking* kwa muda gani.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti namuomba Mhe. Abdalla Maulid atufahamu lakini tutatizama wazo lake, tutakaa na wenzetu tujaribu kufikiria ili kuweza kuondosha usumbufu hasa kwa madereva wetu wanaoingia katika maeneo ya mjini. Nashukuru Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru na kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana, lakini naomba niongezee majibu kwa Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo: *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunaelewa tatizo la msongamano wa magari na ufinyu wa *parking* katika maeneo ya Mji Mkongwe. Serikali imechukua hatua ya kumalizia *master plan* ya mji mzima wa Zanzibar na hayo yote yanaangaliwa kwa upana wake na ndio maana katika kuimarisha kuleta haiba ya mji na kuendeleza mji wetu ili uendane na hali halisi ya kisasa, serikali imefanya maamuzi ya kuendeleza ile *corridor* ya Darajani. Tayari michoro imekamilika, kazi za awali zote zimekamilika na kwa sababu ya utaratibu wetu tulionao na makubaliano na *UNESCO* kwa msingi wa kulinda hifadhi ya Mji Mkongwe, inabidi ramani zetu tuzipeleke *UNESCO* nao waziangalie watoe maoni yao, na ni kwa kufuata sheria pia tulizozianzisha hapa ndani. Kwa msingi huo kuna taratibu za kufuatwa ili kukamilisha huo mchakato, ndio maana mpaka sasa ukaona eneo lile limezuwiwa kwa makusudi ili ifanyike kazi iliyokusudiwa na tunaamini muda usio mrefu kuanzia sasa basi vibali hivyo vitapatikana na ujenzi ule utaendelea. Kwa sababu watu waliokuwa tayari kujenga maeneo yale wapo na serikali imeshajipanga kuendeleza sehemu ile na katika ujenzi huo basi, kutakuwa na maeneo maalum ya *parking*.

Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu na wananchi kwa jumla tuwe na subira tupokee matatizo tuliyonayo ya sasa ya ufinyu wa *parking* na tuchukue kila hatua zitakazowezekana katika kuona nafasi ndogo iliyopo inatumika vizuri, kwa kufuata maelekezo ya wenzetu watu wa Manispaa tutahakikisha kwamba tunashauriana nao vizuri ili tupunguze msongamano huo na ufinyu huo wa *parking,* ili wananchi wetu wasisumbuke.

Lakini tukubali kwamba, unapokusudia kufanya mambo mazuri ya kimaendeleo yapo matatizo yatajitokeza yakiwemo hayo ya ufinyu wa *parking* na msongamano wa magari. Kwa hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu na wananchi kwa jumla waungane na serikali wakati huu ambapo nia na dhamira ni kuendeleza eneo la Darajani liwe na haiba, liwe na mvuto, liwe la kisasa. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 160

Ujenzi wa Barabara za Ndani

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:-

Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na mimi awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama, pamoja na matatizo ya mvua ya hapa na pale lakini bado tuko salama kama hivi. Sasa naomba swali langu Nambari 160 lijibiwe.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipanga kimaendeleo ili kukuza maendeleo ya Zanzibar na watu wake hasa suala la barabara na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anastahiki pongezi, kwa nia yake ya dhati kuupandisha hadhi Mji wa Chake Chake Pemba kuwa Mji Nam. 2 Zanzibar. Hata hivyo, mji huo bado umekabiliwa na baadhi ya changamoto kubwa kwa upande wa njia zake za ndani kuwa ni mbaya sana na hazipitiki, kama vile njia ya msingini, njia ya Polisi Chake – Machomane, Madungu – Mgogoni, Chanjaani – Mpendae – Bandataka, Kiziwani Shungi – Mji Mpya, Misiioni na kadhalika.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa haraka wa kulimaliza tatizo hilo kwani zimo ndani ya Mji Mkuu Pemba.

(b) Je, njia ya Msingini ni njia iliyo ndani ya kitovu cha Mji wa Chake Chake na ni njia ya asili pia ni kero kwa wananchi, ni lini itamalizwa uzia huu.

(c) Njia ya kuanzia Tibirinzi kupitia Daraja Bovu la Tingatinga kuelekea Wesha. Je, serikali ina mpango gani kuhusu daraja hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijbu:
Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake namba 160 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, serikali imo katika mchakato wa kuhakikisha kuwa inatatua kero zote zinazowakabili wananchi wake na katika suala la njia na kwa sababu ndio chachu ya kuleta maendeleo katika sehemu yoyote ile. Serikali tayari imeshaanzisha mpango mkakati wa miaka mitano kupitia Mfuko wa Barabara na miongoni mwa njia zitazobahatika kupangwa kutengenezwa kwa Pemba ni njia ya Msingini pamoja na Madungu - Mgogoni (njia ya Mapinduzi). Njia hizo tayari zimeshapimwa na ni matarajio yetu kwamba, hata michoro imeshatayarishwa. Kwa upande wa njia nyeginezo zilizobaki zitatengenezwa kwa kadiri hali itakavyowezekana.

(b) Mhe. Mwenyekiti, njia ya Msingini ni njia muhimu kwa mji wa Chake Chake na kwa kulijua hilo ndio maana serikali yetu ikatoa kipaumbele kwa njia hii kutengenezwa ndani ya awamu hii ya Mpango Mkakati wa serikali wa miaka mitano, kwa kupitia Mfuko wa Baraza ili kuweza kupitika vizuri na kuondoa kero kwa wananchi wanaoitumia barabara hiyo.

(c) Njia ya Tibirinzi - Wesha kupitia Daraja la Tinga Tinga, serikali imo katika mchakato wa kutafuta ufadhili wa kuweza kutengeneza daraja la kisasa ili kuwarahisishia usafiri kwa wananchi wanaolitumia eneo hilo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi nimpe pongezi sana Naibu Waziri wetu ambaye kwa kweli maneno aliyosema yananitia moyo kwamba, kweli serikali imeona haja kwa njia ya Wesha ambayo daraja lake la Pondeani linatikatika na ndio kwenye miundombinu ya mafuta na umeme, kwa hivyo kulichukulia juhudi daraja letu la tinga tinga.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nina swali nataka nimuulize Mhe. Waziri. Pamoja na majibu yake mazuri lakini amesema kwamba tayari utafiti na upimaji wa barabara ya Msingini na barabara ya Mapinduzi kuelekea Mgogoni kwamba tayari zimeshapimwa na zimeshafanyiwa utafiti. Lakini nataka nimwambie Mheshimiwa kwamba haya ni mambo ambayo yanapimwa lakini yanabakia

ndani hayaoneshwi kwenye vipimo vya barabara halisi kwa wananchi ili wakaweza kujua kama mwisho wa barabara yao ni hapa. Kama njia ya Msingini ni njia ambayo imezungukwa na majumba pamoja na maeneo mengine.

(a) Ni lini watakwenda kuonesha nafasi au upana wa barabara ile ili kwa wale wananchi ambao wanasogea barabarani wasisogee na wale waliokwishasogea waweze kuziweka nyumba zao katika nafasi nzuri kabla ya kuvamiwa na ujenzi wa barabara.

(b) Mgogoni bado haijavamiwa kwenye ujenzi, lakini bado haijaonesha upimaji wake umefikia wapi. Je, hawaoni umuhimu wa kupeleka upimaji au uoneshaji wa mwisho wa barabara kabla haijavamiwa na wananchi kwa ujenzi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba nimjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said wa Jimbo la Chake Chake maswali yake mawili ya nyongeza ambayo nitayajibu kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, barabara ya Msingini na barabara hiyo ya Mapinduzi kuhusu suala la kuweka alama la kujua wananchi ni wapi ambapo mwisho wa njia utafikiwa. Mhe. Mwenyekiti, naomba nimwambie Mheshimiwa Mwakilishi kwamba kazi ya kutengeneza barabara ni hatua kwa hatua na kwa sasa ni kwamba tayari kama nilivyoweza kutanguliza kujibu kwa jibu langu la msingi kwamba tayari barabara hizo zimeshapimwa na imejulikana wapi ambapo kwa kweli barabara hizi zitafikia. Lakini kwa bahati mbaya kutokana na hatua kwamba sasa hivi ni kipindi ambacho cha mvua lakini na hiyo hatua nyengine ambayo ameishauri au ameisema naomba tutaichukuwa na panapo majaaliwa muda sio mrefu kazi hiyo itafanyika.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuweza kunipa nafasi asubuhi hii kuweza kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Waziri katika kijiji cha Ndikoni Shehia ya Chumbageni kuna barabara ambayo ile barabara tumeambiwa iko katika Manispaa.

(a) Je, ni lini barabara ile itafanyiwa matengenezo.

(b) Vile vile kuna barabara ambayo iko Ngwachani Shehia kuelekea Skuli ambayo skuli ile ni skuli ile ni kubwa na ni skuli ya Maendeleo lakini

imekuwa barabara ile ni kero kwa wanafunzi. Je ni lini barabara itafanyiwa matengenezo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Bahati Khamis Kombo Mwakilishi wa Wananchi Mahiri Jimbo la Chambani kama ifuatavyo:-

Kuhusu barabara ambazo Mheshimiwa amezitaja za Chumbageni na Ngwachani kuelezea kwamba ni lini ambazo nazo kwa vile zimeonekana ni kero ni lini zitafanyiwa ukarabati ili nazo ziweze kuruhusu hali ya kupitika na kurahisisha wananchi kupata huduma zao muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba katika Afisi ya Rais Tawala za Mikoa kupitia Mfuko wa Barabara kiufupi ni kwamba kumekuwa na bajeti ambazo sio zile kubwa sana ambazo za kuweza kutengeneza barabara nyingi kwa wakati mmoja. Kutokana na hali hiyo tumekuwa tukitengeneza barabara moja tunakusudia kutengeneza barabara zote ambazo ziko ndani ya *feeder road* katika hichi kisiwa cha Unguja na Pemba. Lakini sasa Mheshimiwa Mwakilishi nimwambie kwamba kwa sasa hivi bado hatujawa na mpango ambao wa moja kwa moja katika kuzifanyia ukarabati barabara hizo ambazo amezitaja. Ingawaje serikali ina mpango kwamba hizo pia nazo huangalia utaratibu ulio makini katika kuona kwamba nazo zinafanyiwa ukarabati.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwamba bajeti ni ndogo itakuwa haitoshi na kwamba hawana bajeti ya kutosha kutengeneza barabara zote hizo. Lakini naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza.

Katika jiji cha Chake Chake Shehia ya Michungwani nayo imo barabara ya Gombani Michungwani wananchi wale hii ni miaka takribani mia wanateseka kwa usumbufu wa barabara. Je, ni lini wizara yako itahakikisha kwamba wanawatengenezea barabara ile wananchi wangu wa Michungwani ili kufaidi matunda ya Serikali yao ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Jembe Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani kama ifuatavyo:

Mhe. Mwakilishi kama ambavyo niweza kutangulia kusema kwamba dhamira ya serikali ni kuhakikisha kwamba barabara zote zilizomo ndani ya visiwa vya Unguja na Pemba kwa kupitia taasisi hii ambayo tunaisimamia kuhakikisha kwamba barabara zote za *feeder road* na sisi tunazifanyia ukarabati. Lakini kutokana na bajeti ambazo amezielezea tutakuwa tukienda hatua kwa hatua. Barabara hiyo ya Michungwani ambayo umeielezea ni moja katika barabara ambazo ni *feeder road.* Lakini sasa Mhe. Mwakilishi barabara ambazo nimeweza kuzisemea kwa haraka haraka ambazo tutaweza kuzofanyika kazi katika mpango wa mkakati katika kipindi hichi ni hizo ambazo nimezitaja kwa Chake Chake.

Hivyo, naomba Mheshimiwa Mwakilishi pale ambapo tutapata nafasi ya kuona kwamba tunaweza kupata *fund* nyengine naomba nikuhakikishie kwamba na barabara hiyo ambayo umeitaja na nyengine tutazifanyia kazi kwa kadiri hali itakavyokuwa imeruhusu kifedha.

Nam. 21

Usimamizi wa Suala la Zaka

Mhe. Said Omar Said - Aliuliza**:**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi kwa kuweka Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kwa lengo la kusimamia haki za mayatima na maslahi ya wanyonge.

(a) Je, Serikali imelisimamiaje suala la zaka hapa nchini ili wanyonge wapate haki zao za Kisheria.

(b) Ni sababu gani zilizowafanya wafanyabiashara wakubwa na wadogo waliopo Zanzibar kutowajibika ipasavyo katika suala la zaka.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Said Omar Said Mwakilishi wa Jimbo la Wingwi swali lake nambari 21 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo yafuatayo:

Mhe. Mwenyekiti, Zaka ni moja kati ya nguzo tano za Kiislamu. Zaka ni jina linalotumika kwa mali maalumu, inayotolewa na watu maalumu kwa makundi maalumu baada ya kufikia kiwango maalumu kwa kuambatana na nia na shuruti maalumu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna taratibu mbali mbali zinazotumika ulimwenguni kwa vyombo vya serikali katika kusimamia, kukusanya na kugawa Zakka. Miongoni mwa taratibu hizo ni pamoja na :-

(1) Serikali kupanga hesabu na kukusanya kwa lazima kutoka kwa watu wote wanaowajibika kutoa Zaka kwa mujibu wa mali zao zilivyo.

(2) Serikali kushawishi na kuwaongoza watu wanaotoa Zaka ili watowe kwa hiari na usahihi.

(3) Serikali kupanga hesabu za Zaka pamoja na kodi hivyo kwa wanaotoa Zaka kusamehewa baadhi ya kodi.

Mhe. Mwenyekiti, , baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la msingi lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Serikali imekua ikichukua hatua mbalimbali katika kulisimamia suala la Zaka hapa Zanzibar. Muongoni mwa hatua hizo ni pamoja na kuweka Sheria Namba 2 ya mwaka 2007 iliyoanzisha Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na kuipa jukumu la kuratibu na kusimamia ukusanyaji na ugawaji wa Zaka. Katika kutekeleza jukumu hilo. Kamisheni ya Wakfu inahakikisha kwamba:-

i. Jamii inakua na elimu sahihi kuhusiana na mambo ya Zaka.

ii. Mtu mwenye uwezo na anaetaka kutekeleza wajibu wa Zaka anasaidiwa ili atekeleze wajibu wake kama inavyoelekeza Sheria,

iii. Mali za Zaka zinasimamiwa vyema na kutumika kwa kuzingatia Sheria na taratibu za kidini zilizopo.

iv. Taarifa za makusanyo na matumizi zinatolewa,

v. Halikadhalika jumuiya na mifuko inayodhamiria kukusanya na kugawa Zaka Zanzibar zinapewa vibali iwapo zitakidhi vigezo vya kisheria.

(b) Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa sababu zinazowafanya baadhi ya Wafanyabiashara na Waislamu wengine kutokutoa Zaka ni pamoja na Kupenda dunia na mali zaidi, hivyo kuwa na ubakhili wa kutoa kwa kudhani kwamba, kutoa Zaka ni kupoteza . Napenda kuchukua fursa hii kutoa wito kwa Waislamu wote, wafanya biashara pamoja na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao tunazo mali zilizofikia kiwango cha kutolewa Zaka kutoa zakka ili wanyonge wapate haki zao kwa mujibu wa Sheria ya Dini yetu ya Kiislamu. Ahsante.

Mhe. Mhe. Said Omar Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ili kumuuliza Mhe. Naibu Waziri suala moja tu la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa lengo kuu la kuweka serikali ni haki itendeke na ndio maana kukaweka Mahakama ya Kadhi hapa Zanzibar. Mahakama ni miongoni mwa mihimili ya dola. Je, Mhe. Naibu Waziri huoni kwamba bila ya serikali kuingiza mkono wake hakuna awezae kuipta haki yake ya kisheria.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Said Omar Said: Mhe. Mwenyekiti, narudia swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa lengo kuu la kuweka serikali huku ulimwenguni ni haki itendeke, kila mmoja apewe haki yake na ndio maana hapa Zanzibar pakaundwa Mahakama ya Kadhi kutokana na Uislamu uliopo hapa Zanzibar. Na kama tunavyojua kwamba Mahakama ni miongoni mwa mihimili mikuu ya dola.

Je, Mhe. Naibu Waziri huoni kwamba bila ya serikali kuingiza mkono wake kwa kutetea haki za watu hakuna awezae kuipata haki yake ya kisheria.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Said Omar Said swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, serikali imekuwa ikijitahidi kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata haki zao katika Mahakama zetu na katika taasisi zetu ambazo zile haki wananchi hao wanapaswa kuzipata.

Mhe. Mwenyekiti, nimwambie tu Mhe. Said Omar Said ni kwamba serikali inaendelea kuhakikisha kwamba wananchi wake wanazipata zile haki ambazo

wanazopaswa kuzipata katika taasisi katika Mahakama na vyombo vyengine vya dola.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia fursa na mimi kuweza kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo yako wazi na ya ufasaha zaidi.

Lakini katika majibu yake katwambia kwamba kuna makundi maalum ambayo yanapaswa kupewa zaka na huo ndio utaratibu kwenye dini yetu. Lakini pia kuna watu ambao maalum ambao wanapaswa kutoa hiyo na sadaka pia. Lakini pia kwenye vitabu vyetu tumeambiwa kwamba utaratibu wa utoaji wa zaka na sadaka kwamba utoe mkono wa kulia na wa kushoto uwe hauna habari.

(a) Je. Mhe. Naibu Waziri kwa hawa watoaji wa zaka ambao wako hapa ndani ya nchi yetu kuna utaratibu gani ambao wameandaliwa juu ya utoaji wao zaka na hizo sadaka ili kuwafikia wananchi bila ya kuona kwamba wananchi ambao wanapatiwa hizo zaka na sadaka na hadhaliliki au hawaoneleki.

(b) Je, kuna hawa watoaji zaka wangapi ambao hii Jumuiya ya Mufti Mkuu inawatambua kwamba hawa ndio watoaji wa zaka au waliojiorodhesha na taasisi hizi ziko ngapi ambazo zinatoa hizi zaka. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Wakfu na Mali ya Amana miongoni mwa kazi zake kama alivyosema awali ni kusimamia zoezi za zaka.

Mhe. Mwenyekiti, nimjulishe Mhe. Hidaya Ali Makame kwamba zoezi la ukusanyaji wa zaka linafanywa kisiri. Mhe. Hidaya Makame Ali kama wewe utakuwa na zile sifa ambazo za kutoa zaka basi Afisi yetu ipo unawasiana nao moja kwa moja halafu watakuelekeza namna gani ya kufanya. Kubwa zaidi usiri unakuwepo.

Kwa hivyo , wote ambao wanaoyoa zaka basi usiri unakuwepo na hazitotoka bahari kwa watu wengine ambao hawatapaswa kuzijua hizo bahari kwa ajili ya kujua nani alietoa zaka.

Suala la pili Mhe. Mwenyekiti, ni kweli zipo taasisi mbali mbali kama nilivyoeleza katika swali langu. Lakini taasisi nizozijata nataka zote kuzitaja kama vile kuna taasisi ya Jumuiya ya Zaka na Sadaka Zanzibar, hii nayo pia imepewa idhini na Afisi ya Wakfu na Mali ya Amana kukusanya zaka. Pia kuna Jumuiya ya Maimamu Zanzibar nayo pia inafanya hii kazi za kukusanya zaka na pia kuna Afisi ya Taarikat Kadiriya hii ipo katika utaratibu wa kupewa hicho kibali.

Kwa hivyo, tunazo jumuiya nyingi ambazo zinafanya kazi hii. Lakini vile vile kwa kusema ni watu wangapi ambao waliopata hizi zaka nikwambie tu Mhe. Hidaya Ali Makame kwamba kila mwisho wa mwaka wa kiislamu basi Afisi ya Wakfu na Mali ya Amana huwa inatoa ripoti yake kueleza watu wangapi ambao wamepewa zaka kwa mwaka huu kwa mwaka wa kiislamu na vile vile inaeleza watu wangapi ambao wamepewa hiyo zakka. Kama nilivyosema kwamba tutakapotoa zaka Mhe. Mwenyekiti, niwaambie Wajumbe kwamba tutakapokuwa na moyo wa mali zetu ambazo zina sifa za kutolewa zaka basi tuelewe kwamba tunaisaidia serikali kukuza uchumi na kuondoa umasikini. Kwa sababu tunapotoa zaka, zaka ile inatumika kwa watu pengine wanyonge wafanyabiashara wadogo wadogo ambao pengine wanahitaji kupewa msaada angalau kuendeleza biashara yao.

Kwa hivyo, niendelee kutoa wito kwamba Waheshimiwa Wawakilishi wananchi wote wa Zanzibar wanaosikiliza ni kwamba kama tutakuwa na mali ambazo zimeshapitiwa na mwaka mali ambazo zimekuwa zina sifa za kutolewa zakka basi tusisite kuzitolea zaka ili kuisaidia jamii yetu ya Kizanzibari ambayo inahitaji kusaidiwa. (*Makofi*)

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kunipatia fursa hii kuuliza swala moja la nyongeza. Lakini pia nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na hamasa kwa wale wanaostahiki kutoa zaka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nalitaka kuuliza kuna kipindi niliona utaratibu huu wa kutolewa hizi zakka na kusaidiwa wanyonge niliona vilihamasishwa baadhi ya vikundi vikawa vimepatiwa hilo jambo.

Sasa nilitaka kujua je, serikali mpango ule umeishiwa wapi au ni changamoto zipi zilotukwanza mpaka nimeona utaratibu ule kimnya haujaendelea au tumekumbana na kikwazo gani nilitaka kujua. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Ofisi ya Wakfu na Mali ya Amana huwa inafanya utaratibu mbali mbali wa kusaidia jamii pale ambapo watoaji wa zaka wanapofika katika ofisi ile. Kwa hivyo, ofisi inapokea ile zaka na kuvipatia vikundi mbali mbali au watu mbali mbali. Kwa hivyo, nimwambie tu kwamba ofisi inaendelea kutoa zaka katika vikundi mbali mbali vile ambavyo vinastahiki kupewa zile zaka, na vile vile watu mbali mbali ambao wanastahiki kupewa zaka.

Kwa hivyo, ofisi inaendelea na jitihada yake ile ile ya kutoa zaka kwa wale ambao wanastahiki, na bado sio kwamba serikali imesita kufanya hivyo, kwa sababu inafanya hivyo pale ambapo tu ile zaka inapelekwa katika ofisi husika, na mara tu inapopelekwa basi watu wanapatiwa hiyo zaka. Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba aelewe tu Mhe. Panya kwamba pale ambapo pengine ataona kwamba shughuli zile hazifanyiki, basi aelewe tu kwamba huo utoaji wa zaka wenyewe pengine unakuwa mdogo mdogo au unasuasua. Kwa hivyo, kubwa zaidi ni kuhakikisha kwamba zaka tunazitoa ili tuweze kuwasaidia jamii yetu na vikundi mbali mbali kama Mhe. Panya alivyojionea yeye mwenyewe.

Nam. 47

Uvamizi wa Vianzio vya Maji

Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis – Aliuliza:-
Kwa kuwa suala la upatikanaji wa maji safi na salama ni suala la msingi katika maisha ya binaadamu ya kila siku. Kwa kuwa suala la upatikanaji wa maji lina changamoto katika jamii ambapo licha ya jitihada za serikali lakini bado kuna wachache wanaovamia vianzio vya maji na kuharibu miundombinu iliopo.

(a) Je, kuna utaratibu gani uliopangwa ili kuzuia vitendo vya uharibifu vinavyofanywa katika vianzio hivyo vya maji.

(b) Je, serikali imechukua hatua gani kwa wale waliobainika kuvuruga au kuharibu miundombinu hiyo kwa makusudi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis Nafasi za Wanawake, swali lake nambari 47 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji inaendelea na jitihada za kuzuia vitendo vya uharibifu katika vyanzo vya maji, kwa kuendelea na uanishaji na upimaji wa maeneo hayo kwa nia ya kuyawekea mipaka maalum na hatimae kuyapatia hati za haki ya matumizi ya ardhi, kuendeleza upandaji wa miti, ujenzi wa uzio kwa kadiri ya hali ya uwezo inavyoruhusu, sambamba na utoaji wa taaluma kwa wananchi kupitia vyombo vya habari na mikutano ya wananchi kishehia juu ya ulinzi na utunzaji wa vyanzo vya maji, kwa lengo la kulinda rasilimali maji kwa faida yetu na vizazi vijavyo.

(b) Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Mamlaka ya Maji kwa kushirikiana na Wilaya na Mikoa, husika inafanya jitihada za kuwatafuta wanaofanya hujuma katika vyanzo vya maji na inapogundulika inawachukulia hatua zinazopaswa, ikiwa ni pamoja na kuwalipisha faini au kuchukuliwa hatua zaidi kwa mujibu wa sheria. Ahsante sana.

Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, napenda nimuulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa serikali imejitahidi kuweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa maji safi ili kuwaondolea kero wananchi wake, na kwa kuwa kuna baadhi ya watu kwa makusudi mazima hupanga njama za kuharibu miundombinu hiyo. Je, wizara imeweka mikakati gani ya kuhakikisha vitendo hivyo haviendelei.

Aidha, ni watu wangapi hadi sasa wameshatiwa hatiani kwa makosa ya aina hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Namna ya kuzuwia kwamba vitendo hivi haviendelei, kama kanisikiliza vizuri tumeainisha hapa, kwamba kwanza tunapanda miti, tunajenga uzio, lakini pia tunatoa elimu kwa wananchi kusudi wafahamu kwa

sababu ulinzi wa kwanza na muhimu wananchi wenyewe kufahamu umuhimu wa vianzio vya maji.

(b) Kuhusu ni wangapi wamepatikana na hatia hizo. Ni kwamba tunao kama saba ambao wamepatikana na wengi wao wametoleshwa faini ikiwa shilingi laki mbili au laki sita na wengine wamenunulishwa mabomba kutokana napale walipokuwa wameharibu. Ahsante.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, jembe letu kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba pale Jimboni kwangu Kinyasini kuna mashine ambayo wameifunga katika eneo la skuli, wakawa fedha ya kuunga umeme hawana mimi nikatoa shilingi laki tisa ikaenda kulipiwa, lakini matokeo yake mpaka hivi leo wananchi wa Kinyasini Sokoni mpaka Kisongoni maji hawajapatiwa, na mabomba ndio tatizo, mabomba yameoza mabomba mapya hamjawafungia na tumeshahangaika sana hamjaenda kufunga, mnataka afanye mwakilishi.

Swali langu moja ni kwamba ni lini mtakwenda kufunga mabomba katika eneo lile ili wananchi wangu wa Jimbo la Chaani Kinyasini wapate maji safi na mazuri, wakati mimi tayari nimeshachangia ume me kukulipeni shilingi laki tisa, kama mnataka chengine nijibuni sasa hivi hapa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, nimeipata hiyo taarifa na anaelewa kwa sababu mengi tumefanya, linapokuwa linatokezea la kufanya kuwasaidia wananchi wetu tunafanya. Sasa hili ningekuwa nimelipata labda tungekuwa tumeshakuwa na jawabu tukajua nini tumekwamisha na nini lini tutafanya.

Kwa hivyo, mimi nimuombe kwamba kama tulivyokua tumeshirikiana hayo mengine katika jimbo lake, basi na hili tushirikiane ili tuone lini tutaweza kukamilisha hiyo shughuli. Ahsante sana.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ili nikaweza kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, namuuliza kwamba katika kipindi hiki cha mvua kubwa huwa kunatokea maradhi ya mripuko kama kipindupindu, na mara nyingi husababishwa na maji.

Je, wizara kwa kupitia Mamlaka ya Maji, imejipanga vipi kutoa dawa hususan maeneo yanayoathirika na mripuko huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba ile sentensi ingekamilika vizuri. Kipindupindu kinasababishwa na maji yaliyochafuliwa sio maji tu. Sasa na maji yetu kiuwasili ni salama na pia tunajitahidi sisi kama ZAWA kuweka dawa stahiki kutokana na wasi wasi, ya kwamba kutoka kwenye chanzo cha maji mpaka kumfikia mtumiaji hapa kati yanaweza kuharibiwa. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Nam. 137

Changamoto ya Usafiri Kwa Maafisa Elimu wa Wilaya

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: (Kny: Mhe. Mwanaasha Khamis Juma) - Aliuliza:-

Maafisa wa Elimu wa Wilaya wanafanyakazi katika wakati mgumu katika kufatilia mambo mbali mbali katika kazi zao. Aidha, moja kati ya changamoto kubwa zinazowakabili ni tatizo sugu la kukosekana kwa usafiri wa uhakika.

Je, Wizara ina mpango gani katika kuwatatulia changamoto hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 137 kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Maafisa wa Elimu na Mafunzo ya Amali wa Wilaya na Mikoa, wana jukumu kubwa la kusimamia maendeleo ya elimu katika Wilaya na Mikoa yao. Utekelezaji wa majukumu yao unahitaji kupatiwa usafiri wa kuwawezesha kufuatilia kazi katika skuli. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imewapatia usafiri wa vespa maafisa wote wa elimu walioko Wilayani, wakiwemo wa Wilaya mpya ya Magharibi.

(b) Afisa Elimu wa Wilaya ya Magharibi B ndiye aliyekuwa Afisa Elimu wa Wilaya ya Magharibi kabla ya kuvunjwa wilaya hiyo na kuwa mbili. Afisa Elimu wa Wilaya Magharibi A alikuwa Afisa Elimu msingi wizarani, ambaye aliruhusiwa kuhama na usafiri wake aliokuwa nao akitumia alipokuwa

wizarani. Katika vyombo hivyo, Afisa wa Elimu wa Wilaya ya Kaskazini B chombo chake kilipata ajali na kipo wizarani kwa ajili ya matengenezo, na vespa moja ya Mratibu wa Elimu Mbadala na Watu Wazima, Wilaya ya Magharibi B kiliibiwa na kesi yake iko polisi.

Mhe. Mwenyekiti, wizara inafanya juhudi ya kuwapatia usafiri maafisa hao wawili kwa haraka kadiri inavyowezekana. Hata hivyo, wizara yangu inatambua kuwa Maafisa wa Elimu wa Wilaya wakati mwengine wanapata usumbufu mkubwa wa ukosefu wa mafuta, na kwa vile majukumu yao yako chini ya Ofisi za Wakuu wa Wilaya, ninawaomba Waheshimiwa wa ofisi zao zichangie pia katika kuwapatia mafuta. Ahsante.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kutokana na majukumu mengi ya Wakuu wa Wilaya, tukizingatia kila programu ina bajeti yake. Je, kwa kutegemea Wakuu hawa wa Wilaya hatuoni kama tunawaongezea mzigo mkubwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba kiutendaji sasa hivi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inashirikiana kwa karibu na Ofisi ya Tawala za Mikoa au na Ofisi za Wilaya na Mikoa.

Mathalan Ofisi ya Tawala za Mikoa zinawalipa mishahara walimu hawa na kwa upande wa maposho tunalipa sisi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Ndio maana tukasema kwamba tusaidiane katika suala la kuwapatia huduma za usafiri. Sisi wizara tumetoa vespa, basi Wilaya na Mikoa watatoa mafuta ya kusaidia uendeshaji wa shughuli hizo. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, na mimi napenda kumuuliza swali moja dogo la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Wilaya yetu ya Kati tuna majimbo matatu ambayo ni Tunguu, Chwaka na Uzini. Lakini pia katika wilaya yetu hatuna fursa za kibiashara ukizingatia na maeneo ya wilaya nyengine ambazo ukusanyaji wa kodi katika wilaya zao ziko juu zaidi, kitu ambacho hupelekea pia Ofisi za Halmashauri pamoja na Wilaya kuweza kusaidia katika mambo tofauti ya maskulini kwetu.

(a) Swali ni kwamba je, serikali haioni kufanya kazi kwa kuongeza bidii zaidi na kasi katika kuongeza fedha kwenye mwaka huu wa bajeti, ili kuweza

kufidia fedha kwa ajili ya kusaidia skuli zetu pamoja na walimu ili kupunguza gharama ambazo zinawakabili.

b) Mhe. Mwenyekiti, uko utaratibu ambao umetumika katika nchi tofauti wa kuweza kuwakopesha walimu kwa muda mrefu, ili baada ya muda fulani zile gari au vespa zinabakia kuwa mali zao, ambapo serikali inafidia kiasi fulani cha fedha na yule mwalimu mwenyewe anakuwa anaingiza kiasi fulani cha fedha, ili waweze kupata nafasi hizo za usafiri. Je, serikali inaweza kuliangalia suala hili ili kuweza kulitekeleza. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la kuongeza fedha. Nafikiri suala hili liko dhahiri kwamba taasisi zote na wafanyakazi wote wa serikali, tunaombwa kuongeza juhudi, maarifa na ufanisi ili kuweza kuongeza tija na pato katika kazi zetu na pato hilo baadae litasaidia bila shaka katika kutatua huduma mbali mbali, zikiwemo hizi za usafiri na nyenginezo zinazohusu walimu.

(b) Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba sasa hivi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa kupitia mifuko yake mbali mbali SACOS zake zile, zinawakopesha walimu vyombo vya usafiri wakati wowote wakiwa tayari wanakopeshwa. Hivi juzi tu tuliwakopesha walimu vespa zenye thamani ya shilingi milioni mia moja katika kisiwa cha Pemba. Watakapotokea na walimu Unguja, basi kwa kupitia mfuko huo watakopeshwa vyombo hivyo vya usafiri. *(Mkofi)*

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri pale kasema kwamba Wilaya ya Kaskazini B Ofisa wake vespa yake ilipata ajali. Naomba aniambie tu kwamba ajali hii aliyopata sasa hivi ni muda gani, na hiyo vespa ina gharama gani matengenezo yake. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, ajali hii ilitokea kwa kipindi kirefu kidogo na wizara kwa sasa kwa kweli inafikiria zaidi kununua vespa mpya kuliko kutengeneza. Kwa hivyo, tunahakika kwamba taratibu za

manunuzi zimeshaanza na wakati wowote taratibu hizo zitakapokamilika Ofisa wa Elimu wa Wilaya ya Kaskazini B atapata chombo hicho cha usafiri.

Nam. 41

Ajira ya Zaidi ya Wafanyakazi 150 Kwa Wizara ya Afya

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza:-

Mnamo mwezi wa Machi, Wizara ya Afya imeomba kibali cha ruhusa ya kuajiri wafanyakazi wapya katika kada mbalimbali katika Hospitali zetu Zanzibar wapatao 150.

(a) Je, Kitengo cha Damu Salama watapatiwa wafanyakazi wangapi katika kuondoa tatizo la upungufu wa wafanyakazi katika kitengo hicho.

(b) Je, katika Hospitali ya Chake Chake kuna upungufu wa wafanyakazi wangapi.

(c) Ni idadi gani ya wafanyakazi wanaohitajika kwa Wizara ya Afya kwa ajili ya Hospitali zetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 41 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani, kwamba ni mdau na mfuatiliaji mkubwa wa shughuli zinazofanyika katika kitengo hiki cha damu salama. Ni kwa lengo la kutaka kuona serikali pamoja na taasisi nyengine wanakipa umuhimu mkubwa kitengo hiki kwa umuhimu wake. Lakini pia kuwapa moyo wananchi kuhamasika na kujitokeza kuchangia damu kwa manufaa yao na kwa taifa kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Abdalla Diwani katika maelezo ya swali lake la msingi, alieleza kwamba Wizara ya Afya imeomba kibali cha ruhusa ya kuajiri wafanyakazi wapya, katika kada mbali mbali wapatao 150. Mhe. Mwenyekiti kama ulimi ulivyokuwa hauna mfupa na wakati mwengine mkono pia hukosea kidogo kuandika, hivyo naomba niweke sawa kidogo takwimu hii ili iendane na dhamira halisi ya muulizaji wa suala hili alivyokusudia kwa kusema. Serikali

imetupa kibali kwa kuajiri wafanyakazi 295 wa kada mbali mbali na sio wafanyakazi 150.

a) Mhe. Mwenyekiti uchache wa wafanyakazi katika sekta ya afya umejitokeza katika ngazi tofauti za utoaji wa huduma hizi kuanzia vitengo, idara, vituo vya afya na hata hospitali zetu zote. Wafanyakazi ambao wanaajiriwa watagawanywa katika sehemu tofauti nilizozitaja kulingana na umuhimu wa mahitaji kwa sehemu husika, sehemu ambayo inaonekana ina upungufu mkubwa ndio inapelekewa kipaumbele zaidi kutokana na umuhimu wake.

Lakini kutokana na mpango tunaoutayarisha wa kuwagawa wafanyakazi tunatajia kuwapeleka wafanyakazi 3 katika kitengo cha damu salama.

b na c) Mhe. Mwenyekiti kutokana na mpango wa makisio ya mahitaji ya wafanyakazi yaliyofanywa mwaka 2013 na Wizara yaani *minimum staff requirement* inaonesha kunajitajika wafanyakai 170 wa kada mbali mbali kwa hospitali ya Chake Chake, hivi sasa hospitali hiyo ina jumla ya wafanyakazi 172 ambao wengi kati ya hao ni kada saidizi.

Kwa kuwa mpango huo wa makisio umeshapita muda na kwamba idadi ya wananchi inaongezeka siku hadi siku pamoja na ongezeko la vifaa vya kisasa vyenye kuhitaji wataalam maalum hivi sasa Wizara inanedelea tena kufanya tena mapitio ya mpango huo, mara itakapokamilisha tutapata makisio halisi ya wafanyakazi sio tu kwa hospitali ya Chake Chake na vituo vyengine vya Afya bali pia hospitali zote na Wizara nzima. Hivyo mahitaji ya Hospitali zetu za Zanzibar yatajulikana hasa mara baada ya kukamilika mapitio ya mpango huu wa mahitaji ya wafanyakazi kama nilivyoeleza kabla.

Namuomba Mhe. Muwakilishi Abdala Maulidi Diwani kumuahidi kwamba tutakuletea mahitaji hayo kwa maandishi mara yatakapokamilika ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Maulidi Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nishukuru sana kuona jitihada zangu kwa umoja zinaonekana ninazofanya kwa nia safi kuwasaidia Wazanzibari nje ya sekta ya afya kwa kutumia nguvu zangu nashukuru sana, na pongezi zako nimeipokea.

Lakini katika suala langu hili ni kweli kuna tatizo na upungufu wa wafanyakazi katika kada ile ya damu salama na hata juzi walivyokwenda Mkwajuni kufanya

kazi hii imebidi tuwaazime wanafunzi kutoka Chuo cha Afya kuweza kufanya na unapeleka wafanyakazi watatu kutokana na gawio ulilokuwa nalo.

Je kuna mkakati gani maalum kwa umuhimu wake ile taasisi kuona kwamba inapata wafanyakazi wa kutosha hilo moja.

Pili pamoja na mwenendo mzuri kabisa umepewa ruhusa kuajiri wafanyakazi 295 katika kada hii ya afya na nia thabiti ya Rais wetu wa Zanzibar jinsi kuona namna gani Hospitali ya Mnazi Mmoja au huduma ya afya katika Zanzibar inakuwa sio changamoto tena bali inakuwa kwa bahati mbaya ndio mtu apate hiyo. Kuna masikitiko ya kutosha katika Hospitali yetu ambayo mnaita Hospitali ya rufaa kwa Zanzibar, unakwenda katika hospitali hiyo kuna uhaba wa wafanyakazi hata katika ngazi ya *nurse* na madokta wasaidizi katika hospitali ya Mnazi Mmoja.

Je. lini litamalizika tatizo hili ili kuona Wazanzibari wanaokwenda plae kuweza kutatua matatizo yao kwa sababu hata msomaji wa X- Ray katika hospitali ya Mnazi Mmoja wapo wawili, lini tatizo hili litaondoka?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa ruhusa yako nimjibu Mheshimiwa Muwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe suala lake lenye (a) na (b) kama ifutavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mpango tulionao Wizara kuhusu kituo cha damu salama ni kwamba baada ya wafanyakazi hawa watatu ambao tunawapeleka, basi kila tutakapoendelea kuwaajiri wafanyakazi tunaangalia na idadi ambayo tunaiajiri na kule tutaendelea kupeleka mpaka mahitaji kamili yakamilike, kwa sababu sasa hivi kuna upungufu wa wafanyakazi wasiopungua 11. Sasa tumejipanga kila awamu ambayo tunafanya uajiri basi tuhakikishe kwa umuhimu wa kitengo kile tunapeleka wafanyakazi wapya.

Lakini kuhusu hospitali ya Mnazi Mmoja na mapungufu yaliyopo ya wafanyakazi yakiwemo mpaka ya *orderly*. Mhe. Mwenyekiti naomba kumjibu Mheshimiwa kwamba uajiri unafanyika lakini sio kwa mara moja tunaajiri vijana hawa wafanyanyakazi hawa 295 kwa mara moja. Sasa hivi wamepelekwa wafanyakazi na wanaendelea kupelekwa taratibu tunaomba licha ya wewe Mhe. Mwakilishi lakini hata na wananchi watuvumilie kwa kadhia hii kwa sababu ile *shortage* pale ilikuwa ni kubwa sana na Serikali tuna Wizara tunajitahidi kui-*cover* taratibu ili kuhakikisha tunakamilisha lile lengo.

Lakini pia sio Mnazi Mmoja tu Mhe. Mwenyekiti na Mhe. Mwakilishi ni katika hospitali zetu zote na nyie pia mnaona kwa sababu mnapata nafasi mnatembelea kusudi kwenda kuona hali ilivyo ili kutushauri nini tufanye, tunawashukuru sana kwa hili. Sasa tunaomba muvumilie hii *process* tunayokwenda nayo kwa sababu tukiwapata 20 wanapaswa kugaiwa kila sehemu sio kuwapeleka pahali pamoja tu kama tunavyofikiria. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi ya kuuliza suala la nyongeza katika wizara hii mama, mimi swali langu litakuwa na vitoto (a) na (b).

Mhe. Naibu Waziri tunaona kwamba suala la damu na suala la X-ray ni vitu muhimu sana katika hospitali zetu.

a) Ni lini Wizara yako itafikiria kuweka benki ya damu katika hospitali ya Chake Chake ili kuondoa matatizo ambayo yanawafika wananchi pale ambapo watahitaji damu.

b) Ni lini Wizara yako itafikiria kutafuta mashine ya kusafishia *X-Ray* katika Hospitali ya Chake Chake na kutafuta mashine ya *washing machine* pale katika Hospitali ya Chake Chake ili kuondoa tatizo la mashine ambazo ipo hazifayi kazi kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Zulfa muwakilishi wa viti maalum Mkoa wa Kusini Pemba swali lake lenye (a) na (b) kama ifutavyo:

Mhe. Mwenyekiti suala la kuweka wafanyakazi wa damu salama katika Hospitali ya Chake Chake kama nimemuelewa sasa hivi wapo, kwa sababu Pemba kipo kitengo ambacho kinashughulika na damu salama kipo Wete lakini wafanyakazi wamesambazwa katika vituo vya Chake Chake, Micheweni na sina hakika vizuri Vitongoji siwezi kukuthibitishia, ili inapotokea tu dharura wao wana-*donate* pale wanawahamasisha wananchi pamoja na kupokea damu, pamoja na kuagizia damu ya kuwasaidia wananchi. Kwa hivyo nakuthibitishia kwamba pale yupo mtu ambae anashughulika na jambo hili, lakini Makao Makuu ya kitengo hicho yapo Wete.

Kuhusu mashine ya kusafisha Picha za *X-Ray* kama nimemsikia vizuri kutokana ma matatizo ya mic, hii mashine Mheshimiwa sina hakika vizuri nisikujibu kitu ambacho sina uhakika nacho, lakini kama hapana mashine hiyo

basi tunakuahidi kwamba tutafuatilia tuhakikishe kwamba mashine ipo, lakini pia kuna mashine ambazo sasa hivi tumeziigiza katika kufanyiwa ukarabati kwa hivyo naamini kama ipo mashine ambayo imeharibika na hiyo itakuwa miongoni mwa mashine ambao zinashughulikiwa kwa kufanyiwa ukarabati. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza suala dogo la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Lakini kabla nimpongeze kwa majibu yake mama na yale ya nyongeza ambayo ametangulia kujibu.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze vile vile Wizara ya Afya kwa kuweza kufikiria suala zima la kuwaajiri wafanyakazi katika kuziba mapengo katika hospitali mbali mbali katika visiwa vyetu. Lakini kadri utakavyoendelea kuajiri maana yake inazuka tatizo la ukosefu wa makazi katika baadhi ya hospitali husasan zile ambazo zipo vijijini suala langu lipo hapa.

Kuna nyumba ambazo zimejengwa katika hospitali mbali mbali vijijini ili ziwasaidie wale madaktari ambao wanaajiriwa na kupangiwa katika sehemu hizo, lakini imeonekana kwamba nyumba nyingi hazitumiki ipasavyo madaktari wanapangiwa lakini hawakai katika nyumba zile na matokezeo yake kwamba wanaishi mijini wanafika katika vituo wamechelewa na wanaondoka mapema, mfano mzuri ni kituo cha Afya cha Uzi daktari anafika saa 4 lakini saa 7 gari ikipita anaingia kuelekea mjini.

a) Je, Mhe. Waziri suala hili unalifahamu.

b) Ni hatua gani Wizara inachukua ili kuona kwamba nyumba zile zinazojengwa zinaleta maslahi kwa wananchi katika maeneo yale.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mheshimiwa swali lake lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, suala hili tunalifahamu na ni tatizo sugu katika Wizara yetu, karibu wafanyakazi asilimia 60 wanaofanya kazi vijijini na ambao nyumba zipo kwa ajili ya kuishi wafanyakazi wale hawataki kuishi katika nyumba zile. Suala hili tumelibaini wakati tunapofanya ziara zetu ndani ya vituo vyetu vya afya vilivyomo vijijini Unguja na Pemba, nyumba ni nzuri zina viwango zipo pahali pazuri na zina *facility* karibu zote, lakini tatizo la wafanyakazi wetu kutokutaka kukaa katika vituo hivi.

Hatua tuliyoichukua Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Wizara imeshaanza kuwapa adabu ndogo ndogo za maandishi wale wafanyakazi ambao hawataki kukaa katika vituo vyao na hawana sababu maalum, imeshaanza kuchukua hatua na ilianza kuwaambia kwa maneno katika vikao vyao lakini sasa inaendelea na hatua ya kuwaandikia na baadae itafuata hatua nyengine kwa mujibu wa kanuni za utumishi.

Nam. 111

Ukodishaji wa Majengo Kwa Ajili ya Matumizi ya Afisi za Serikali

Mhe. Suleiman Sarahan Said **-** Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa nia njema wakati mwengine hutoa fursa za kukodi majengo kwa Wizara husika lakini Wizara hizo huwa hazijiwekei malengo ya kupata majengo yake ya kudumu na wakati Serikali inamiliki ardhi na maeneo ya wazi au majengo mabovu.

(a) Je, bado zipo Wizara na Idara za Serikali zinazokodi majengo mpaka hii leo.

(b) Je, ni lini Serikali imeweka kikomo cha kukodi majengo kwa Ofisi za Wizara na Idara .

(c) Je, Serikali haioni kufanya hivyo ni kupoteza fedha za Serikali.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji **–** Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti nimefurahi sana kusimama mbele ya Baraza lako tukufu na kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 111 lenye kifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:

(a) Ni kweli kwamba bado zipo Wizara na Idara za Serikali ambazo zinaendelea kukodi majengo kwa ajili ya shughuli za kiofisi hasa kisiwani Pemba. Hata hivyo, Serikali ina mpango wa kuhakikisha kwamba inajenga majengo kwa ajili ya matumizi ya Ofisi za Serikali na hivi sasa ujenzi wa jengo la Wizara ya Fedha na Mipango unaendelea kisiwani Pemba. Jengo hilo litakapokamilika litaweza kutumika kwa ajili ya ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Wizara ya Kazi, Wazee, Uwezeshaji, Vijana na Watoto

(b) Mhe. Mwenyekiti, kama hali ya fedha itakuwa nzuri, Serikali imedhamiria kwamba ifikapo mwaka 2020 Wizara na Idara zake zote ziwe katika majengo yanayomilikwa na Serikali.

(c) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna fedha ambazo zinatumika kwa kulipia kodi za majengo hayo, lakini kama nilivyokwisha eleza katika majibu yangu hapo awali, ni kwamba Serikali imeliona suala hilo na tayari imeanza kulifanyia kazi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, na pia nimshukuru Mhe. Waziri kwa kunijibu masuala yangu *short and clear*, lakini nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba pale Chake Chake ndio kitovu cha Mji wa Pemba na ndio Mji Mkuu na ndio sura ya Pemba, pale kuna Ofisi ya Mkuu wa Wilaya au nasema Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Wilaya pale alikuwa na jengo zaidi ya miaka 30 mpaka 40 lilikuwa linatumika kama Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, baada ya muda Mkuu wa Wilaya yule ikawa jengo lina matatizo au linatakiwa matengenezo akaondoshwa kuwekwa katika eneo la banda nasema sio nyumba ni banda la kuwekwa *temporarily* ili nyumbe ile itengenezwe na arudishwe pale.

Matokeo yake nasikia imetokea Afisi kwamba jengo lile sasa limeshatengenezwa liko vizuri limepata Ofisi nyengine au atakabidhiwa mtu mwengine na Mkuu wa Wilaya katika eneo lake la banda limeshaachana wakati wowote litaanguka na mtu yule ni kiongozi mkubwa sana.

a) Je, ni lini atamtafutia ofisi ya uhakika kwa hadhi yake Mkuu wa Wilaya wa Chake Chake.

b) Kwa nini kama bado ofisi nyengine zina kodi na kama nyumba ile ambayo ilikuwa ina nembo ya Mkuu wa Wilaya hasa kwamba ndio ofisi ya mkuu wa Wilaya, kwa nini asikodiwe kurudishwa katika hadhi yake mpaka itakapopatikana nyumba nyengine.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mheshimiwa Muwakilishi wa Chake chake, napenda nimhakikishie tu kwamba hata mimi naamini kwamba Chake Chake ndio Mji ambao uko kati kati ya Kisiwa cha Pemba na bila ya shaka wengi tukienda kule tunashuka kwa ndege pale Chake Chake Pemba, kwa hivyo Wizara yetu hii itajitahidi kuhakikisha kwamba sura ya mji wa Chake Chake iwe ni sura nzuri kwa sababu mgeni akiingia kwa mara ya kwanza Pemba anaingia kwa njia ya ndege, kwa hivyo hilo tunalitilia maanani.

Lakini jibu hasa la suala lako kuhusu makaazi au ofisi ilizotumika na Mkuu wa Wilaya ningependa nikukumbushe tu Mheshimiwa kwamba Mkuu wa Wilaya iko Wizara maalum inayoshughulikia suala hilo, na mimi nakuhakikishia kwamba nitakwenda kuungumza na Waziri anayehusika na suala hilo na tutafanya mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba majengo ambayo anatumia Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya lazima yawe na hadhi ya utawala, maana yake utawala ni kitu muhimu sana unapokwenda katika nchi kukaribishwa ukaenda kwa Mkuu wa Mkoa, au Mkuu wa Wilaya au kwa Mkuu wa Nchi basi yale majengo lazima yawe na hadhi yake. Nakuhakikishia kwamba hilo tutalifanyia kazi. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Kwanza nampongeza sana Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na nataka nitie nyongeza kidogo tu jamii ifahamu kilotendeka Pemba kwa sababu isijengeke dhana, labda Mkuu wa Wilaya tumemnyanganya jengo lile. Jengo lile sasa hivi linatumiwa na Wizara ya Katiba, Sheria ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, jengo lile likuwa bovu miaka mingi sana aliyekuwa Waziri wa Utumishi wakati ule, Mhe. Haji Omar Kheri akaliomba jengo lile ili litengenezwe kwa hivyo tukatiliwa pesa kwa ajili ya jengo lile na kwa usalama wa uongozi wa pale wakatafutiwa eneo jengine wakaenda wakakaa.

Na sisi wakati ule, Mhe. Omar Haji Kheri ni Waziri wa Utumishi akaliomba jengo lile na katiliwa pesa ili alitengeneze baadae akae yeye kwa utaratibu wa makubaliano maalum ya kiserikali na ndivyo ilivyofanyika. Kafanya matengenezo jengo likawa zuri, likafika kiwango cha kuridhisha kwa hivyo sasa jengo letu tumekabidhiwa na mkandarasi, tumekabidhiwa tayari na tunataka tuingie. Ghafla tukapata taarifa kwamba kuna Mkuu wa Wilaya kenda kubandika bao lake lile la Mkuu wa Wilaya pale, Serikali ni moja ya Taasisi zote za Serikali. Yakafanyika mazungumzo na bahati nzuri, Mkuu wa Wilaya yuko chini ya Utawala wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ na yeye ndiye aliyeliomba jengo lile, anajua sana historia yake.

Kwa hivyo, tukawasiliana na waziri anayehusika na akazungumza na viongozi kwa vile jambo linaeleweka hatimae jengo lile likarejeshwa katika ile ile taasisi ambayo imetengenezwa kwa gharama zake fedha za utumishi. Kwa hivyo jengo lile hakunyanganywa ni taratibu za kiserikali tu kapangiwa mahali pengine na Wizara ya Utumishi imetengeneza wao si kwa gharama ya pesa nyingine yoyote si kama serikali imetoa kwa lengo jengine lolote isipokuwa Wizara ya Utumishi ipate mahali pa kukaa.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa maelezo hayo, nataka ijengeke hoja tu hakunyanganywa. Ahsante. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri. wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora naomba ukae. Katibu kwa wizara inayofuata.

Mhe. Mwenyekiti: Swali linalofuata katika Wizara hiyo hiyo, Mhe Shehe Hamad Mattar wa Jimbo la Mgogoni, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Swali litaulizwa na Mhe. Shehe Hamad Mattar, Jimbo la Mgogoni.

Nam. 153

Ukataji wa Bima kwa Vyombo vya Baharini na Nchi Kavu

Mhe. Shehe Hamad Mattar – (Aliuliza)**:**

Kwa kuwa wananchi wote wenye kumiliki vyombo vya aina mbali mbali vya baharini au nchi kavu wanalazimika kukata Bima katika Shirika la Bima la Zanzibar kwa ajili ya kulinda mali zao au abiria wanaovitumia vyombo hivyo dhidi ya janga lolote likitokea.

(a) Je katika mwaka wa fedha 2015/2016 na 2016/2017 ni ajali ngapi zilizotokea.

(b) Ni ajali ngapi zilizotokea baharini na ngapi nchi kavu.

(c) Ni ajali ngapi zimeweza kulipwa bima na zenye thamani ya kiasi gani.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Shehe Hamad Matar Mwakilishi wa Jimbo la Mgogoni swali lake namba 153 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Ahsante sana, Mhe. Mwenyekiti, katika kujibu suala ambalo limeulizwa na Mhe. Shehe Hamad Mattar, kwanza kabisa nataka nimuhakikishe kwamba afya ni nzuri kama ulivyoniulizia anasema hakuniona Barazani kwa sababu tulikwenda safari na Mhe. Rais Djibout. *(Makofi)*

(a) Mhe. Mwenyekiti, napenda kulijuilisha Baraza lako tukufu kuwa jumla ya ajali 1,167 zilitokea katika vyombo mbali mbali vya usafiri wa majini na nchi kavu kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 na 2016/2017.

(b) Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa ajali hizo jumla ya ajali 11 zilitokea kwa vyombo mbali mbali vya usafiri baharini na vyombo 1,156 ni kwa vyombo vya usafiri wa nchi kavu. Katika ajali hizo za vyombo vya nchi kavu jumla ya ajali 610 zilitokea kwa upande wa Unguja na ajali 546 zilitokea kwa upande wa Pemba.

(c) Mhe. Mwenyekiti, Wizara yetu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usafiri Baharini pamoja na Idara ya Usafiri na Leseni, zimepitisha sheria zinazowataka wamiliki wote wa vyombo vya baharini na nchi kavu kuvikatia bima vyombo vyao. Aidha, suala la idadi ya walioathirika ambao wamepatiwa malipo yao ya bima baada ya ajali, kwa sasa wizara ilifuatilia ili kuhakikisha wamiliki hao wa vyombo pamoja na mashirika ya bima wanatekeleza wajibu wao. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa majibu ya Waziri wa Ujenzi wa Mawasiliano na Usafirishaji, lakini nishukuru kwa majibu yangu ya swali langu (a) na (b) lakini sijaridhika katika swali (c) kwa sababu swali (c) linasema ni ajali ngapi zimeweza kulipwa na bima na zenye thamani kiasi gani na sio swali la kuwashirikisha wamiliki wa vyombo kukata bima. Tayari wamiliki wa vyombo wameshakata bima lakini nilitaka kujua wangapi wamelipwa bima.

(b) Na ni sababu zipi zinazowafanya wananchi kulalamika kwamba hawalipwi Bima wakati wanapopata ajali zao. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako ningependa kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba swali la bima linakuwa ni swali gumu sana hasa kwa hawa watu wana vyombo vyao wanaofanyia biashara, kwa sababu kukata bima kunaongeza gharama zao za kufanya biashara, na huwa mara nyingi wanakwepa kukata ile bima ili wapunguze matumizi.

Sisi katika Wizara yetu tutahakikisha ni kwamba kwanza tunawataka wenye vyombo vyote vya baharini na nchi kavu wakate bima, na huwa tunahakikisha kwamba chombo kimetumika nchi kavu hakiwezi kutumika mpaka kiwe kimekatiwa bima na askari polisi wana haki ya kuisimamisha gari ikiwa inahisi ile gari haikuonesha kuwa ina bima na kama haina bima inatakiwa pale pale

ipelekwe kituo cha polisi ili isititembee bila ya bima kwa sababu akija akipata ajali inakuwa matatizo.

Jibu la nyongeza, ni kwa kwamba kuna Makampuni mengi, mashirika mengi ambao watu wanakata Bima na haya Mashirika ukiwauliza wenyewe wahusika, watakwambia kwamba Shirika la Bima la Zanzibar ndio mshirika bora ukikata bima yako kule ukipata ajali, hawachelewi kukulipa. Lakini yako malalamiko kwamba kuna mashirika mengine ya bima hapa unakwenda unakata bima lakini ukipata ajali basi itakua hadithi nyingi, mzunguko wakupeleke kule, ili kupata uhakika wanataka uhakika kwamba kweli inatokea ile ajali halafu mtaanza kujadiliana kuhusu habari ya fidia.

Kusema kweli Mhe. Wizara yetu haina uwezo wa kuyalazimisha haya mashirika kwamba wawe wanalipa fidia ikitokea ajali hii, tunamwachia mwenye chombo ili akate bima ambayo inayokubalika kiserikali ni Bima ya kutosha. Lakini ikitokea ajali akenda kudai fidia inakuwa sisi hatuchughuliki na huku. Kama nilivyokufahamu Mhe. Mwakilishi jibu lake litakuwa ni hilo kwamba, na watahadharisha wawe na hadhari hawa wenye vyombo vya baharini na nchi kavu kwamba wanakata bima ya kutosha na wanakata Bima kutoka katika Shirika ambalo kweli lina historia ya kuhakikisha kwamba linawapa fidia pale ambapo wanapata ajali. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

MUONGOZO

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Mwenyekiti kwa mujibu wa Kifungu cha 37(1) kinasema kwamba Waziri ajibu swali, Kifungu 37

Mhe. Mwenyekiti: umeniomba kuhusu muongozo sijasema chochote unaendelea.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Bado sijakuelewa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Shehe Hamad Mattar, kuhusu muongozo Kanuni ya ngapi.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti Kanuni ya 37(1) kinachomtaka Mhe. Waziri ajibu swali kwa usahihi na kwa ufupi, lakini mimi katika majibu yake sijaridhika naye. Kwa sababu nnavyoelewa bima kuna aina mbili au tatu lakini nnayozungumza hapa ile bima inayomfanya mtu aweze

kulipwa fidia kama chombo chake amelipia kiasi cha kupata *comprehensive* na hayo ni mabima ambayo huwa yanatakiwa kuwa mtu kulipwa.

Kuna Bima hii ya kuchangia tu mbali, hii inayostahiki kulipwa ni wangapi wamelipwa? Kwa sababu kuna malalamiko kama mtu amepata ajali na chombo chake kinastahiki kulipwa lakini halipwi, ndio nilitaka kujua idadi gani wamelipwa. Sio swali la kukata bima. Bima unakata lakini wale wanaostahiki kupata *comprehensive* ni wangapi wamelipwa. Hilo ndio swali langu. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Kuhusu utaratibu nimekuelewa, lakini kama nimemfahamu Mhe. Waziri amekujibu na jawabu yake amekwambia swali la bima linatokana na mtu mwenyewe na isitoshe na lile shirika husika, halafu alizungumza kuwa wao hawana mamlaka ya kuingilia lile Shirika la Bima. *(Makofi).*

Kwa hivyo Mhe. amekwisha kujibu. Washehimiwa Wajumbe muda wa maswali umekwisha, muda wa maswali na majibu umekwisha, nikuruhusru Mhe. Waziri, ukakae. Tuendelee Katibu na masuala mengine. *(Makofi)*

HOJA YA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea na sasa nimwite Mhe. Yussuf Hassan Iddi wa Jimbo la Fuoni akifuatiwa na Mhe. Masoud Abrahman Masoud.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kuweza kunipa fursa hii adhimu kabisa ya kuweza kutoa michango yangu, kuhusiana na Bajeti Ofisi ya Rais Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nimpongeze Makamu wa Pili wa Rais kwa utendaji wake makini, katika kulitumikia Taifa letu. Halkadhalika niwapongeze Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji wote wa Ofisi hii kwa kutekeleza vyema Bajeti mwaka huu 2017/2018 pia Mhe. Mwenyekiti nitumie fursa hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu kwa Ripoti yao safi ambayo imetusaidia kutuonyesha njia katika kuchangia Hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, ki ujumla niipongeze Wizara hii ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mafanikio makubwa ambayo yamepatikana katika utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2016/2017. Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu utakwenda kwenye utekelezaji wa kipindi cha miezi 9 ya Julai/Machi 2017. Nianze kwenye ukurasa wa 16 katika Shughuli za Uratibu, katika shughuli hii kuna mambo mengi katika *programme* hii yametekelezwa kwa mujibu ya utekelezaji ule wa Julai/Machi lakini katika shughuli ya C ambayo katika kitabu cha mwaka jana inapatikana katika ukurasa wa 24 katika *programme* hii kuna shughuli. Samahani Mwenyekiti, katika shughuli C ukurusa wa 24 sio programme ya Uratibu na Shughuli za Serikali naomba radhi, ni suala la kukabiliana na maafa, kuna C kanuni ya kukabiliana na maafa ambapo mwaka jana walitueleza katika kitabu chao hiki wataandaa hizo kanuni za sheria za kukabiliana na maafa. Lakini katika utekelezaji wa kitabu hichi cha 2017/18 taarifa hii haimo, kwa hivyo ilikuwa tumuombe Mhe. Waziri atakapokuja atueleze ni sababu zipi au hii kanuni tayari imeshaandaliwa au vipi.

Vile vile, ukija kwenye ukurasa huo huo wa 24 kwenye kitabu hichi cha 2016/17 kwenye *programme* ya Uratibu wa Sherehe za maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi Wakuu.

Mambo mengi katika *programme* hii yametekelezwa lakini ukija ukurasa 25 (e) kuna kukamilisha mapitio ya Sheria Nam. 10 ya Mwaka 2002 ya Kuwaenzi Viongozi Wakuu, ambapo mwaka jana Wizara iliahidi kwamba itafanya hayo mapitio ya Sheria hiyo lakini ukija kwenye kitabu hichi cha 2016/17 jambo hilo halionekani. Sasa vile vile, tunaomba Mhe. Waziri atakapokuja atupe maelezo jee hayo mapitio ya sheria yamefanyika na lini sheria hio itawasilishwa hapa Barazani kwa ajili ya kufanyiwa mabadiliko.

Lakini vile vile, Mhe. Mwenyekiti nikija ukurasa 37 wa kitabu hiki cha Bajeti ya mwaka 2017/2018 katika *programme* hii hii ya Sherehe ya Maadhimisho ya Kitaifa ukurasa wa 37 katika kipengele cha (e) kuna kufanyia matengenezo eneo la kaburi la Mhe. Abeid Amani Karume liliopo Kisiwandui pamoja na Dkt. Omar Ali Juma. Sasa mimi nashauri tu kwamba kuna Viongozi wengine, wamesahauliwa na makaburi yao ni vyema nayo yakafanyiwa matengenezo, akiwemo Mzee wetu Sheikh Idrisa Abdul Wakil Nombe kule Makunduchi lakini halkadhalika Mzee wetu Sheikh Aboud Jumbe Mwinyi. Kwa hivyo nilikuwa naishauri wizara kwamba makaburi haya nayo yaingie katika mpango huu ya kufanyiwa matengenezo katika Bajeti ya 2017/2018. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikija ukurasa wa 18 ambapo katika ukurasa huo umeelezewa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, tunaishukuru sana Serikali ya

Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwezesha kutoa fedha hizi kwa kutupa sisi Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi, ili kuleta maendeleo katika majimbo yetu. Hadi Machi, jumla ya majimbo kwa mujibu wa kitabu hichi 46 yameshapatiwa fedha hizo, likiwemo jimbo langu la Fuoni lakini na pengine mpaka kwa muda huu nafikiri kwa muda huu kama limebakia Mhe. Hamza, lakini majimbo yote 53 tayari yameshapatiwa fedha hizo. Kwa hivyo tunashukuru sana serikali tuiombe basi mwaka unaokuja fedha hizi zipatikane kwa wakati kwa sababu safari hii kidogo zimechelewa na ilikuwa imetupa mzigo mkubwa.*(Makofi)*

Lakini katika maelezo haya, katika maelezo ya ukurasa wa 18 wizara imesema imetoa mafunzo kwa Wajumbe wote wa Kamati hapa kidogo napata mashaka, kwanza sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao ndio wenye viti wa Kamati hizi. Tulizungumza kipindi kile kwamba tupatiwe mafunzo ya kuendesha hizi kamati zetu, lakini mpaka tunaingiziwa fedha hizi za maendeleo sisi Wenyeviti hatujapatiwa mafunzo yoyote. Tuiombe Wizara baada ya kumaliza hichi kipindi cha Bajeti, watupatie mafunzo hayo ili yale mapungufu ambayo yamejitokeza katika miaka iliyopita ya kuzisimamia vizuri pesa hizi basi yasiweze kujitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kwenye Kamati zetu ametoka mtu mmoja tu aliyepata mafunzo ambaye ni Katibu. Hapa tumeambiwa wajumbe wote wa Kamati. Kama ni wajumbe wote mbona sisi wengine hatuna taarifa hiyo. Mhe. Waziri atueleze kwamba ni kweli kwamba mmmetoa mafunzo kwa wajumbe wote wa Kamati au mmetoa mafunzo kwa katibu mmoja mmoja kwenye kila kamati.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 28 kuhusu na Tume ya dawa za kulevya. Niipongeze serikali kwa jitihada zake inazochukua katika kupambana na suala zima la dawa ya kulevya. Ukija kwenye (iii) ukurasa wa 28 tumeambiwa nyumba 9 zimepatiwa ruzuku kwa ajili ya kuwawezesha kufanya shughuli zao hizi za *sober houses*. Lakini taarifa hii haikuwa wazi kwamba jee hizi *sober houses* ni zote 9 za Unguja au ni Unguja na Pemba. Kwa hivyo Mhe. Waziri tunaomba akija hili atufafanulie hapa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kwa mwaka wa 2016/17 ni vijana wangapi ambao wamepata hii huduma ya upatikanaji nafuu katika *sober* hizi. Kwa sababu tunataka tuone pesa iliyoingia katika ruzuku matokeo yake yakoje, vijana wangapi ambao wamepata hii huduma kwa upande wa Unguja na Pemba. Vile vile katika kitabu hiki cha 2017/2018 hatuoni taarifa yoyote inayohusiana na kile Kituo cha Kurekebisha Tabia kilichokuwepo Kidimni. Serikali pale

imewekeza pesa nyingi katika kituo kile, tunaomba tupate muendelezo wa kile kituo kama kimekamilika au bado ujenzi unaendelea, nihatua gani ambayo imefikia.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho ukitizama ukurasa wa 59 wa kitabu hichi cha bajeti ya 2017/18 hii Tume ya Kuratibu Udhibiti na Kuratibu dawa za kulevya ndio taasisi pekee ambayo inapata fungu dogo. Mwenzangu jana Mhe. Mussa hapa alizungumza kwamba ile bajeti ya Tume ya Ukimwi basi wapewe hawa na ile ya dawa za kulevya iende kule. Kwa hivyo ipo haja kama tupo *serious* na suala la dawa za kulevya basi kwa bajeti hii ya 518 nahisi ni ndogo sana kuweza kukabiliana na *issue* kubwa kama hii. Ipo haja ya hawa wenzetu kuweza kuongezewa fungu ili waweze kufanya shughuli zao kwa umakini zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile napenda kukumbushia tu ahadi ya Mhe. Rais mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete alipotembelea ile skuli ya Kitongani. Tulipata majibu kwamba baadhi ya maandalizi ya utekelezaji wa ahadi ile imeanza. Mimi nataka kujua hatua iliyofikiwa mpaka sasa utengenezaji wa barabara kutoka Fuoni Mtundani hadi katika ile Skuli ya Kitongani ambayo ni ahadi ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tokea mwaka 2009. Ningeomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho basi na hilo anipatie majibu.

Mhe. Mwenyekiti, nikija kwenye ukurasa wa 57, ukiangalia hapa nahisi kama kuna chanzo kimoja cha mapato nahisi kama hapa hakipo. Naomba Mhe. Waziri akija atwambie hichi chanzo kingine cha mapato kimekwenda wapi, chanzo chenyewe ni cha Idara ya upigaji chapa. Ambapo ukitizama ukurasa wa 63 kwenye viambatanisho hichi chanzo kipo na hadi kufikia Machi mwaka 2016/17 chanzo hiki pekee kimeingiza 534 milioni sawa na asilimia 37. Lakini hichi chanzo safari hii hakipo, sasa sijui kimekwenda wapi? Akija Mhe. Waziri kufanya majumuisho basi atueleze kwamba hichi chanzo kimetoka hapa Afisi hii na kimekwenda Afisi nyengine na kule kilipopelekwa tuangalie kweli kimekwenda.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimalizie kwa kutaka ufafanuzi katika sehemu za makusanyo ya wizara lakini kiujumla mimi naunga mkono hoja hii ambayo imewasilishwa jana na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwa asilimia mia moja. Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti. Ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Yussuf Hassan Iddi wa jimbo la Fuoni kwa mchango wako. Sasa nimwite Mhe. Masoud Abrahman Masoud wa Jimbo

la Bububu akifuatiwa na Mhe. Shehe Hamad Matar na Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis ajitayarishe.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii, kwanza na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa tukiwa wazima.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane mkono na wenzangu kuichangia hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwanza nianze na masuala ya maafa. Sasa hivi viongozi sote tuliyokuwemo ndani humu Waheshimiwa Wawakilishi pamoja na serikali kwa ujumla kila tunapofika mwezi wa April tunakuwa na hofu ya kunyesha mvua kubwa zenye kuleta mafuruko. Suala hili kwa sababu limekuwa la kila mwaka serikali ni lazima ijipange kuhakikisha tuna kinga na kinga ndiyo itakayotusaidia kuliko kusubiri wakati wa tatizo limeshajitokeza ndio tunaanza kujitayarisha.

Mhe. Mwenyekiti, maeneo ya Mwanakwerekwe, Kijitoupele na maeneo mengine sasa hivi hali siyo nzuri. Sasa tumuombe Mhe. Waziri aje atwambie ni matayarisho gani au vikao vingapi wamefanya vya kujikinga kabla ya kuanza hizi mvua za masika. Ili tuone kuwa serikali inachukua juhudi gani za kuweza kujikinga kuliko kusubiri kuja kutibu wakati tatizo limeshajitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, pili niombe sana wenzetu wa Mamlaka ya Maji ZAWA, sasa hivi mvua hizi zinazonyesha, kuna baadhi ya wananchi kwenye maeneo mbali mbali wamechimba visima na visima hivyo sasa hivi baadhi yao vimejaa maji na vyengine vinapitiwa na maji ambayo baadhi ya maeneo vyoo vimefura na vimeingia uchafu. Niwaomba wenzetu wa Mamlaka ya Maji ZAWA wahakikishe wanatusaidia kutupatia dawa kwa sababu wananchi wa kawaida wakitumia yale maji lolote linaweza kutokea na wananchi wetu wakasababisha kupata maradhi ya kipindupindu.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwenye jimbo langu tatizo limejitokeza hasa katika eneo la Mbuzini. Mafuriko yametokea baadhi ya nyumba mpaka sasa hivi zina maji ndani. Sababu ya msingi ni ujenzi wa makuta kwenye maeneo ambayo yanapita maji, makuta yale yanazuia maji yasiende na tayari yanaingia kwenye nyumba za watu. Nimshukuru Mkurugenzi wa Manispaa ya Magharibi (A) baada ya tatizo lile nilimpigia simu na waliweza kufika katika eneo na wameliona hilo tatizo. Niombe sana serikali kuna baadhi ya maeneo wameamua kuvunja kwa sababu wameona kwamba kuna tatizo. Lakini kuna na baadhi ya nyumba zimejengwa kenye njia za maji, lazima serikali iziangalie.

Nyumba hizi kila baada ya mwaka itabidi zinatusababishia kujaza maji kwenye maeneo mengine na kutusababishia hasara kubwa kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mama mmoja anaitwa Bi Kulthumu nyumba yake imejaa maji, vifaranga vya kuku karibu 1000, vimekufa na mpaka sasa hivi maji yamo ndani. Kilichosababishwa ni kuta, kuna nyumba ambazo zimejengwa kwenye njia ya maji. Niiombe serikali kupitia kwa Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Manispaa, suala hili walisimamie ili liweze kutekelezeka vizuri.

Lakini hapo hapo Idara ya Mawasiliano kuna barabara ya Mbuzini ambayo wamejenga, wamechimba msingi mkubwa na msingi ule nao umeshajifukia na maji hayapati kupita. Maji yanajaa hayawezi kutoka katika eneo lile na nyumba zinaendelea kujaa maji. Niiombe serikali itusaidie kutupatia kata pira la kwenda kuufukua tena ule msingi ili maji yaweze kutoka na wananchi wetu wapate unafuu wa maji ambayo sasa hivi yamejaa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapa niende kwenye Idara ya Uchapaji. Jana Mhe. Abdalla Diwani aliizungumzia sana, lakini inasikitisha kuwa sasa hivi hata lile gazeti ambalo linatoka la kila siku linakwenda kuchapishwa Dar-es-Salaam. Serikali kwa nia nzuri tu iliomba msaada kutoka Serikali ya Oman na walipatiwa fedha hizi na serikali ikashauriana na wataalamu wa Idara ya Uchapaji wakenda wakanunua mashine ambazo wanazitaka wao. Leo iweje kuwa mashine zile haziwezi kufanya kazi ipasavyo na gazeti la serikali tunakwenda kuchapisha Dar-es-Salaam. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atupe maelezo angalau kidogo yatakayotusaidia na sisi tuweze kujiridhisha.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niipongeze Afisi ya Makamu wa Rais ambayo inaratibu shughuli zote za serikali. Nataka niseme Afisi za serikali sasa hivi kumekuwa na utaratibu mbovu na hasa kwa wale viongozi wa kwenye taasisi za serikali. Unaondoka unakwenda kwenye Afisi Mkurugenzi, wala maafisa wengine huwakuti, unawakuta wafanyakazi wadogo wadogo. Baadhi ya Idara au Mashirika ukienda ZAWA asubuhi saa moja, au moja na nusu, utawakuta wafanyakazi wapo na wanapanga kazi vizuri. Ukenda Shirika la Umeme saa moja, moja na nusu ukenda unawakuta wapo na wanapanga kazi zao. Lakini maeneo mengine ukenda bosi hajafika, bosi hajafika.

Nimuombe Mhe. Waziri kwa sababu yeye ndiye msimamizi wa shughuli za serikali atwambie muda sahihi wa kufika kazini na muda sahihi wa kuondoka kazini na muda gani ambao unakwenda mfanyakazi katika taasisi ya kukusanya

mapato unafika masaa mawili unakuta kwenye kitundu hayupo wananchi wamekaa foleni wanamsubiri aje anawapotezea muda watu wana shughuli zao mbali mbali. Nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja hapa atwambie utaratibu mzuri au wasimamizi wa maafisa uendeshaji kwenye maafisi haya wanasimamia vipi hata unafika kwenye Afisi saa 3 bado bosi hajaja. Itakuwa tunaidhulumu serikali.

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kaamua kwa makusudi kwa kukaa na viongozi wetu hawa kupandisha mshahara kutoka asilimia mia moja. Lazina unapopata nyongeza ya mshahara na kazi ufanye zaidi, sio tunapata mshahara mkubwa lakini kazi tunafanya kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, nikondoka hapa niende kwenye miradi ya TASAF. Niipoongeze Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa usimamizi mzuri wa shughuli za maendeleo. Napenda sana niwakumbushie kuna baadhi ya miradi imefanyika kwa muda mrefu na miradi hiyo imefika asilimia 50. Pesa zile ni za wafadhili na watakapokuja kuuliza miradi ile inakuwa bado haijakamilika. Niombe kwamba inapotoka misaada mengine kwanza tuangalie ile miradi ambayo ilifanyika kabla na haijamalizika.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye suala zima la sherehe za kitaifa. Niwapongeze watu wa Sherehe na Mapambo, mara hii kwa mara ya kwanza Waheshimiwa Viongozi na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kadi za mialiko walipata mapema. Naamini sote tulipata kadi hizo. Niombe waendelee na juhudi yao ile ile, zinapotokea shughuli zozote za kiserikali ndani ya majimbo yetu Waheshimiwa Wawakilishi tusinuse kama mabalozi, tuhakikishe na sisi tunapata mialiko mizuri ili tuweze kuwapokea viongozi wetu ambao watakuja kwenye majimbo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, niliwahi kuwasikia baadhi ya viongozi pahali anapokuja Mhe. Balozi Seif Ali Iddi hata Mwakilishi wa jimbo hajui. Hilo sio jambo zuri kwamba Mhe. Balozi anakuja kwenye jimbo langu nikawa mimi mwenyewe mwenye jimbo sina taarifa. Ni vizuri serikali inapopata taarifa mapema tujuulishwe ili tuweze kushirikiana na kiongozi huyo mkubwa ambaye anakuja kwenye majimbo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu naiunga mkongo hotuba hii asilimia mia kwa mia.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Masoud Abrahmani Masoud wa jimbo la Bububu. Sasa nimwite Mhe. Shehe Hamad Matar, akifuatiwa na Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis na Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa ajitayarishe.

Mhe. Shehe Hamad Matar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa hai mpaka sasa hivi. Pia nichukue fursa hii kwa kuwapa pole wale wananchi wote waliofikwa na hasara kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha, tumuombe Mwenyezi Mungu atupe mvua zenye neema na zisiwe zenye nakama.

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba hii napenda nichangie katika sehemu mbali mbali, kwanza nikianzie kwenye sehemu ya hali ya uchumi wa Zanzibar. Katika hotuba hii tumeweza kuona kwamba uchumi wetu umeongezeka kutoka asilimia 6.5 hadi asilimia 6.8, kwa kweli hii hali ni ndogo sana lakini ndiyo imeshakuwa. Hata kwenye hotuba inaeleza sio sisi Zanzibar tu hata nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara na kanda ya Afrika Mashariki ndiyo hivyo hivyo kwa hivyo imekuwa kama ni sare kwa hivyo tujitahidi. Lakini hapo tulipofika sio pabaya kwa vile hatukushuka chini zaidi. Hata hivyo naiomba sana serikali kusimamia vyema vianzio vyetu vya mapato ambavyo kuwa tumevigundua na vile ambavyo tumeviibua vipya ili viweze kufanyiwa kazi ili kuhakikisha kwamba tunapita hatua zaidi kuliko hapa tulipo.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kuchangia katika ukurasa wa 5 na wa 6 panapozungumzia malengo ya serikali kwa mwaka 2017/18. Sina budi kutoa shukurani zangu kwa serikali kuendelea na utekelezaji wake wa kupunguza umasikini katika dira ya maendeleo ya 2020 katika MKUZA III, hasa pale ilipoonesha kwamba kuimarisha huduma za kijamii mbali mbali ikiwemo makaazi ya watu na maji safi na salama, hizo ni miongoni tu mwa huduma za jamii. Katika hili naishauri sana serikali inapofika wakati wa utekelezaji wa kuweka makaazi haya ya wananchi basi itumie vizuri hii ardhi ambayo tulikuwa nayo ni ndogo na watu wanaongozeka siku hadi siku, sisi tuweze kuitumia bila ya kuona athari inapatikana kwa kujenga majengo ambayo yataweza kuchukua watu wengi. Kwani hivi sasa tunaona sehemu kubwa inachukuliwa kwa vibanda vidogo vidogo eneo hili ambalo kuwa kama tutajenga majengo ya kudumu makubwa yataweza kuhifadhi watu wengi na eneo lililobakia tutaweza kulitumia kwa shughuli za maendeleo kama vile viwanda na kilimo na hii itaweza kutusaidia pia vile katika kukuza uchumi wetu.

Lakini pia vile vile tuchukuwe tahadhari iweze kusimamia suala hili hili la makaazi ya watu wale ambao kuwa hawatapata fursa ya kujijengea wenyewe basi isikubali kabisa kabisa kulitumia eneo la kilimo kwa kufanya maakazi au sehemu ambazo kuwa zinakuwa zinaleta athari baadaye kuweza kuipa mzigo Serikali. Kwa hivyo hapa Serikali naiomba itakapofika wakati kama huu tuanze kutibu kukinga badala ya kutibu.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika kuchangia ukurusa namba 7 na inayozungumzia masuala ya mtambuka kwenye mazingira. Mazingira katika wizara hii imezungumza mazingira na mazingira ina maana pana sana lakini katika humu imejaribu kueleza masuala ya upandaji wa miti katika sehemu za juu na sehemu za pwani.

Kwa kweli tumeona hali ya sasa hivi nchi yetu inapovamiwa na bahari ukipita sehemu nyingi unakuta tayari bahari inakuja juu kutoka na uchafuzi wa mazingira kwa hivyo, sasa tunakosa sehemu za makaazi kwa upande mwengine lakini pia vile sehemu za kulima ni mabonde mengi sasa hivi yamenza kuvamiwa na maji ya bahari na kuyazuiya baadaye yatachukua harama kubwa sana. Ili kuepusha hili Serikali iweze kuweka mkakati makusudi wa kuhakikisha kwamba hizi fukwe zinapandwa miti lakini hata kwa upande wa juu kulingana na mabadiliko ya tabia ya nchi basi tuweze kusimamia kwa mikakati mikubwa kwamba wananchi tunapanda miti, na niwaombe wananchi tusiwe wabishi kwa hili kwa sababu ushahidi uliopo sehemu ambayo kuwa miti iko kwa wingi hali ya hewa inabadilika.

Lakini hata baharini sehemu ambayo kuwa imepandwa miti maji hayana nguvu kuweza kuiporomoa ile ardhi na kuipeleka sehemu ya bahari kubwa, kwa hivyo wananchi wanakuwa hapa tusiwe wabishi na sisi tukubaliane na Serikali kuliunga mkono suala la upandaji wa miti kuweza kulinda mazingira yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nende katika ukurasa wa 10 unapozungumzia masuala ya watu wenye ulemavu kwa kuwa wizara hii ndio inahusika ya watu wenye ulemavu na inasema kwamba imejitahidi sana kwa kufatilia kesi za udhalilishaji kwa watu wenye ulemavu lakini kwamba ni lazima sisi sote tuelewe kwamba sisi waheshimiwa na wananchi wote popote alipo ni mlemavu mtarajiwa, kwa hivyo watu wenye ulemavu nao wanastahiki kupewa haki zao kulingana na hali ilivyo.

Lakini jee ni kesi ngapi katika kufatilia kesi za udhalilishaji ni kesi ngapi zilizosajiliwa na ngapi zimepata ufumbuzi wake na adhabu gani iliyotolewa ili wale ambao kuwa wana nia ya kufanya vitendo kama hiki waone kwamba huku

hakuwendeki. Ni vyema kwamba hizi kesi zikafatiliwa kwa ukweli na kuonekana zimefikia wapi zisibakie kwenye vitabu, kwa sababu wananchi sasa hivi kila mmoja anapiga kelele suala la udhalilishaji hata jana tunasikia sasa hivi jana sasa hivi kijana na miaka 23 kenda kumdhalilisha kikongwe wa miaka mingi tu ni udhalilishaji huo hata si mlemavu lakini ni udhalilishaji kwa hivyo, kesi kama hizi naomba sana tusizifumbie macho kama tunavyozungumza masuala ya madawa ya kulevya basi na hili tulione kwamba lina umuhimu wake kama tulivyozungumza mswada uliopita hapa.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kuchangia katika ukurasa wa 33 katika Ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais katika kifungu kinachozungumzia kukabiliana na maafa kifungu hiki katika makadirio kimeonesha kwamba kimepangiwa 1,506,233,000/= kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa kweli kimtazamo naiona ni kubwa lakini ni ndogo. Pamoja na kuongezeka kwamba mwaka jana awamu iliyopita ilikuwa 850,867,000/= lakini tuangalie ukubwa wa tatizo sasa hivi mwaka huu lilivyotokezea, limeongezeka hatukutarajiwa lakini ndo lishatokezea na siku zote hotuba ya ijumaa inatakiwa uiangalie vile wakati uliopo kama inaelekea ramadhani tutowe hotuba ya kutayarisha mwezi wa ramadhani.

Kwa hivyo na sasa hivi naona mimi nichangie katika suala hili ambao kuwa liko mbele yetu la mvua ilivyo tuathiri kwa Pemba na Unguja, kwa hivyo kutokana na ukubwa wa tatizo hili naiomba Serikali na kuishauri kwa nia safi kabisa bila kuathiri nia ya kuenzi Mapinduzi yetu matukufu ya mwaka 1964 na kuenzi viongozi wetu wakuu wa kitaifa kwa mwaka huu fedha hii iliyowekwa katika kifungu cha sherehe na maadhimisho na kuenzi viongozi wakuu ipunguzwe, tusisherehekе kwa mwaka unaokuja ila tu tutumie asilimia ishirini na tano (25%) ya fungu hili tuweke kwa kuwaenzi viongozi wakuu na asilimia iliyobakia sabini na tano (75%) tuielekeze katika masuala haya hasara iliyotokezea nchini mwetu kama kwa fidia au kwa kutengeneza miundo mbinu ambayo kuwa itaweza kutusaidia katika taifa letu hali ni mbaya sana. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, huo ni mchango wangu katika suala la maafa lakini pia niendelee katika Ofisi hii.

Mhe. Mwenyekiti, suala la utafiti, suala la utafiti mipango yake na sera ni muhimu sana katika ofisi hii inafanya kazi kubwa sana hatuwezi kuendelea katika kufanya mambo ovyo ovyo bila ya kufanya utafiti na ofisi hii ina masuala mengi yanayofanya utafiti na baadaye kupata ufumbuzi ili tuweze kupiga hatua tunapokusudia. Lakini nikiangalia mwaka uliopita asilimia thalathini na tatu tuu (33%) ya fedha yake ndio iliyopata hadi Machi 2017 naiomba sana Serikali na Waziri wa Fedha basi hayupo lakini mawaziri wapo

kwa mwaka huu kifungu hiki kipewe asilimia mia moja ya fedha yake yote iliyopewa, kama hapa imekuwa na asilimia thalathini na tatu tu ni ndogo sana hatujui katika miezi mitatu iliyobakia kama itawaongezea au watabakia hapo hapo, naomba sana kifungu hiki kipewe pesa zake kikamilifu waweze kufanya shughuli za mipango ya Sera na Utafiti.

Vile vile imeelezwa katika bajeti iliyopita kwamba ofisi hii ilifanya matengenezo katika ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais iliyoko Dar es Salaam na Dodoma na sasa imeeleza tena katika bajeti hii hotuba hii inarudia tena. Mimi naomba waziri atakapokuja atueleze kwamba mwaka jana waalifikia asilimia ngapi ya matengenezo yalokusudiwa na mwaka huu yamebakia kiasi gani ili isiwe ni jambo hili hila siku linaendelea kurudia kwa matengenezo kwa sababu kuna shughuli nyengine ambazo tungeweza kuzifanya au kama ni matangenezo au ni kujenga kabisa tukafanua kama haiwezekani kutengeneza basi tujenge upya, kuliko kuendelea kutengeneza jambo hilo hilo ambapo linaweza kutia hasara.

Baada ya hayo mimi nikushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara hii kwa juhudi yake kubwa na mambo yake mengi yanayohusu nchi nzima kuratibu ni kazi kubwa sana lakini na kufatilia utekezaji. Naunga mkono mia juu ya mia hotuba ya Mhe. Makamu wa Rais. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Shehe Hamad Mattar kwa mchango wako sasa nimwite Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis Mwakilishi wa Viti Maalum akifuatiwa na Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa na Mhe. Miraji Khamis Mussa ajitayarishe.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante Mhe. Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia machache katika hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niungane na wenzangu waliotangulia kwa kutoa pole kwa watanzania wote waliopatwa na maafa *inshaallah* Mwenyezi Mungu atatupa wepesi kwa hili. Lakini pia nianze kuipongeza Serikali kwa jihudi kubwa zinazochukuliwa kwa kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanapata huduma muhimu za kijamii pamoja na kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha huduma hizi zinaimarika zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii niende ukurasa wa 16 Programu ya Pili Uratibu wa Shughuli za Serikali fungu (C012) (i) lakini kabla ya kusema chochote pia niipongeze Serikali kwa hatua inayochukua kuelimisha wananchi

juu ya suala zima la kukabiliana na maafa kupitia vyombo mbali mbali vya habari na hasa pale ilipotolewa tahadhari ya kuwa wananchi wanaoishi katika sehemu zinazotuwama maji au ambazo zinakuwa mara nyingi zinapatwa na maafa kutafuta sehemu zenye usalama kwa kipindi hiki cha mvua naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Elimu ile Mhe. Mwenyekiti, imesaidia sana wananchi wameelewa dhamira ya Serikali hasa katika suala hili la kukabiliana na maafa lakini vile vile niendelee kuishauri Serikali kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kwa kila jambo panapostahiki ili kutoa uwelewa zaidi kwa wananchi kwa masuala yote ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 18 (viii) imeeleza kuhusu ufatiliaji wa marejesho ya matumizi ya fedha ya mwaka 2015/2016 hapa nilikuwa nataka ufafanuzi Mhe. Waziri atakapokuja anieleweshe je, katika ufatiliaji huo tumefanikiwa vizuri au kulikuwa na changamoto zozote na kama zilikuwepo basi changamoto hizo ni vyema tukaelezwa na vipi walikabiliana nazo.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 19 (xiv) imeelezwa kuwa Ofisi imesimamia programu ya TASAF ambapo malipo ya kaya masikini yamefanyika naelewa kulikuwa na vigezo vya kufanya mtu alipwe kiasi gani kutokana na hali jee utaratibu ukoje wa malipo hayo nilikuwa nataka kujua. Mtu alichopangiwa kulipwa tuseme mwezi huu mtu kalipwa elfu 30,000/= mwezi unokuja analipwa ile ile au kunakuwa kuna mabadiliko yoyote ningeomba kupatiwa ufafanuzi ili nikapata kuelewa zaidi lakini pia wananchi wakaweza kuelewa. Kwa sababu kuna maneno yanasemwa kwamba; mtu ambayo hayana uhakika hapa ndio nitapata jibu la uhakika. Mwezi huu nimepatiwa shilingi 30,000/= kaya masikini lakini mwezi unaokuja napata shilingi shilingi 28,000/= au 25,000/= na mwezi mwengine zinakuwa zinabadilika badilika jee utaratibu wa kutolewa fedha hizi ukoje ili tupate uwelewa sisi kama viongozi lakini vile vile na wale wananchi ambao wanapatiwa huduma hiyo wapate uwelewa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 21 (xviii) imezungumziwa Uratibu wa Vikao vya Baraza la Watu wenye ulemavu hilo na Vikao vya Maafisa Waratibu wa Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, naelewa kwamba au tunaelewa kwamba waratibu hawa wamewekwa kwa mujibu wa sheria namba 9 ya mwaka 2006 kifungu 21 naomba ninukuu kinasema hivi:

"Wizara zote za Serikali chini ya masharti ya sheria hii zitaanzisha na kuweka mtu maalum kwa madhumuni ya kuhakikisha utekelezaji na ufatiliaji wa masharti ya sheria hii".

Mhe. Mwenyekiti, kinachonisikitisha mimi kwamba hichi ni kitu ambacho kipo kwa mujibu wa sheria waratibu hawa wapo kwa mujibu wa sheria ndani ya wizara zetu, lakini utekelezaji wao naweza kusema bado haujawa mzuri. Kwa sababu ungelikuwa utekelezaji wao uko vizuri naamini changamoto nyingi zinazowakabili watu wenye ulemavu kupitia Wizara zile zingepungua. Changamoto haiwezi kuondoka kabisa lakini zingepungua kwa asilimia fulani lakini kila uchao, kila tukija hapa tunakuta kuna changamoto nyingi ambazo zinawakabili watu wenye ulemavu katika jamii na wizara zetu hizi ndizo zinazoandaa mipango ya Utekelezaji na Mipango Mikakati ya Wizara.

Lakini cha kusikitisha bado ni wizara chache tu ambazo zinajumuisha mipango yao wanajumuisha masuala ya watu wenye ulemavu na kama ni hivyo ningeomba Mhe. Waziri kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ikatoa elimu maalum au mafunzo maalum kuanzia kwa Mawaziri kwa sababu sio mawaziri wote ambao wanaelewa hili au wanalifanya hili au wanalitekeleza hili.

Lakini si Mawaziri tu Makatibu Wakuu wa Mawaizara lakini na Wakurugenzi pia wakaelewa kwamba huyu Mratibu anayeratibu masuala ya watu wenye ulemavu katika Wizara ana kazi maalum ya kuhakikisha kwamba, mipango yote ya wizara inayotengenezwa pale, inaangalia ujumuisho ya watu wenye ulemavu katika wizara zetu ili kuondoa changamoto zinazowakabili watu wenye ulemavu katika jamii.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ya mwaka 2015/2016 ukurasa wa 27 ilieleza katika programu (c) 0125 ilipanga utekelezaji mwaka 2015/2016 kama vitabu tunavyo tutaiona hii, kwanza kupitia upya Sheria namba 9 ya mwaka 2006. Lakini pili kusimamia Utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni za watu wenye ulemavu, vile vile kuimarisha mazingira ya kazi lakini pia kujenga uwezo wa wafanyakazi wa Idara ya Watu wenye Ulemavu.

Lakini nilipoangalia kitabu hiki ambacho bajeti yake ambayo tunaipitia hivi sasa hivi utekelezaji uliofanyika ni mwengine na hivi vyote ambavyo ninavyovisema hapa sikuona utekelezaji wake. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze jee haya yote yametekelezwa kwa kiasi gani kwa sababu huku sikuyaona itabidi anipe ufafanuzi juu ya kupitia upya ile sheria. Kwa sababu tunaelewa kwamba Sheria ya Watu wenye Ulemavu ina

mapungufu makubwa na mapungufu haya ndiyo yanayopelekea kutokea changamoto zote hizi. Kwa sababu sheria ile miongoni mwa changamoto zake kwamba imeweka makosa lakini adhabu zake hazikuwekwa, kwa maana hiyo si rahisi ile sheria kutekelezeka vizuri kwa hiyo tulitegemea kwamba sheria ile itafanyiwa marekebisho ili iweze kufanyiwa kazi vizuri lakini matokea yake sikuiyona.

Lakini vile vile kuimarisha mazingira ya kazi kuimarisha mazingira ya kazi tunaelewa kwamba kuna watendaji wa Idara ya Watu wenye Ulemavu wengine wamepelekwa Vijijini ili kuratibu masuala yale katika Mikoa. Lakini sasa kule wako katika Mikoa wanafanya kazi katika Vijiji tafauti tafauti na hawana usafiri wa uhakika wa maafisa hawa kwa hiyo, inakuwa ni shida kufanya ufatiliaji lakini vile vile kuzipata zile takwimu pamoja na kujua mahitaji ya watu wenye ulemavu na changamoto zinazowakabili katika jamii.

Hivyo ni matumaini yangu kwamba katika bajeti hii itayazingatia haya ili kuboresha zile huduma kwa watu wenye ulemavu wazipate kama inavyostahiki lakini vile vile wafanyakazi hao wanahitaji kujengewa uwezo, na tukiangalia bajeti yetu ya mwaka 2016/2017 tukiangalia kiambatanisho namba 1 imeonesha dhahiri kwamba Idara ya Watu wenye Ulemavu haitaweza kutekeleza majukumu yake kama ilivyojipangia ni asilimia ishirini na mbili (22%) ya fedha ambazo zimetengwa walizopatiwa ukiangalia Idara ile ina mambo mengi, inataka kununua visaidizi ili kuwawezesha watu wenye ulemavu wamudu mazingira.

Lakini hata hivyo inataka kuona watoto wenye ulemavu wanaweza kujifunza vizuri, lakini utakuta watoto wengine wamo majumbani wanashindwa kwenda skuli kutokana na ukosefu wa visaidizi, wanategemea idara hii iwasaidie kuhakikisha wao wanaweza kumudu mazingira na kupata zile haki zao za msingi ikiwemo elimu. Lakini kuna wanafunzi wenye ulemavu ambao wanahitaji kujiendeleza katika masomo ya elimu ya juu na uwezo mdogo watategemea idara hii pia iwa-*support* ili na wao waweze kukidhi haja na kupambana na soko la ajira katika suala zima la elimu.

Mhe. Mwenyekiti, tunapoweka bajeti ndogo kwa wizara hii naamini kwamba itakuwa hatuwatendei haki, kwa sababu yale malengo yote ambayo yamepangwa ili kuwaondoshea kero watu wenye ulemavu yatakuwa hayatekelezeki na kila siku tutaendelea kulalamika. Lakini ni busara kabisa nimuombe Mhe. Waziri kupitia bajeti hii iangalie upya mahitaji ya watu wenye ulemavu, iangalie mahitaji yote ya msingi ambayo inatakiwa idara hii kuyatekeleza pamoja na mambo mengine. Pia waweze kuwaingizia fedha kwa

mujibu wa bajeti ambayo tunaipitisha hapa ili waweze kutekeleza vyema majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja, nategemea yote yatafanyiwa kazi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwantatu kwa mchango wako, sasa nimwite Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa nafasi za wanawake akifuatiwa na Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia wenye afya njema katika Baraza hili la Tisa.

Mhe. Mwenyekiti, pia nikupongeze wewe kwa kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia Hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia mchango wangu nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa maendeleo anayotupatia katika nchi yetu. Lakini pia nimpongeze Makamu wa Pili kwa kutuwasilishia ripoti yake hii naamini Waheshimiwa Wajumbe wameifahamu ndio maana wakapata kuichangia. Vile vile nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri na watendaji wao wote kwa kazi nzuri wanazozifanya katika Ofisi hii ya Makamu wa Pili. Mhe. Mwenyekiti, lakini…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa samahani kidogo naomba niwajuilishe wajumbe nitampisha Mhe. Mwenyekiti Shehe Hamad Mattar aendelee na kikao, lakini kabla ya kumpisha kulikuwa kuna tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti anaomba Wajumbe wote wa Kamati hii wakutane katika ukumbi Nam. 2 baada ya kumalizika au kuakhirishwa kwa kikao hiki. Ahsante sana.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti, Shehe Hamad Mattar alikalia kiti)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante tunaendelea.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naendelea na mchango wangu. Mimi nitaingia katika hali ya kisiasa katika mchango wangu

wa mwanzo. Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutekeleza kwa uhakika ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2015/2020.

Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli kitabu chetu hiki cha makadirio tulichowasilishiwa jana katika hali ya siasa kila kitu kimejieleza. Mimi tu nataka kutoa nasaha zangu kwa wananchi kwamba waachane na propaganda zilizokuwepo mitaani kuhusu masuala ya kufanyika uchaguzi. Kitabu chetu hiki kimetutolea taarifa kwamba uchaguzi hakuna mpaka 2020, kazi iliyobakia ni kazi ya kuendesha nchi yetu. Kwa hivyo, wananchi waache kusikiliza maneno ya nje, uchaguzi umekwisha walioingia katika Baraza ndio wanaendelea, wengine waliobakia wasubiri 2020.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nimpongeze tena Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kututilia saini sheria ya kusimamia masuala ya mafuta na gesi asilia. Kusema kweli Mhe. Mwenyekiti kitendo hiki alichofanya Rais wetu wa Zanzibar ni kitendo cha historia katika nchi yetu na kitendo kizuri.

Mhe. Mwenyekiti, hatua tunaziona zinachukuliwa Mkurugenzi Mwendeshaji wa taasisi hiyo tayari ameshateuliwa inaonesha serikali ipo vizuri katika masuala haya ya gesi asilia na mafuta. Pia tayari imejipanga kuona wataalamu wetu wanakwenda kusoma ili suala hili likamilike kwa ukamilifu. Kwa hivyo, natoa shukurani zangu za dhati kwa serikali kwa hatua inazozichukua kuhusu masuala ya mafuta na gesi asilia.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea niende katika ukurasa wa 34, katika ukurasa huu kitabu cha hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili kuhusu programu ya pili ya uratibu wa shughuli za serikali ambapo moja ya jukumu kuu katika utekelezaji ni kukabiliana na maafa. Mhe. Mwenyekiti, naomba kusisitiza Mhe. Waziri kupitia ripoti hii awe karibu na wananchi wote waliokabiliwa na maafa katika kipindi hiki kinachoendelea cha mvua.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na mchango wangu katika Ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais kuhusu Ofisi ya Baraza la Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti, Ofisi yetu hii ya Baraza la Wawakilishi ambapo jengo hili ndio tunafanyia kazi zetu za kupitisha sheria za nchi. Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia katika kumbi zetu ambazo ziko juu mfano mzuri sehemu ya kompyuta ya Waheshimiwa Wajumbe, Mheshimiwa chumba hicho kinavuja. Lakini pia nije katika chumba Nam. 2 Mheshimiwa juzi wakati tunapitisha bajeti ilinyesha mvua na sisi tulikuwemo mule Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano kusema kweli tulikosa raha kutokana na kuvujiwa na maji. Kwa hivyo, basi naiomba

Ofisi ya Makamu wa Pili kupitia bajeti hii, basi iangalie jengo letu hili la Baraza la Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti, jengo hili ikinyesha mvua kila pahala linavuja hususan huko juu, jengo hili ndilo ambalo tunafanyia kazi zetu sisi waheshimiwa sio vizuri tukisema kama linavuja. Kwa hivyo, naiomba Wizara hii ya Makamu wa Pili basi ilione jengo letu hili ilifanyia marekebisho tuondokane na kadhia hii ya kuvujiwa na maji ya mvua.

Mhe. Mwenyekiti, pia tukizingatia katika mihimili mikuu ni Baraza, Mahakama na Serikali. Kama nilivyosema awali kwamba katika jengo letu kila panapo matatizo basi Ofisi ya Makamu wa Pili iliangalie na jengo hili la Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kuhusu mmong'onyoko eneo la Ikulu ya Mkoani Pemba. Mhe. Mwenyekiti, hali ambayo inapelekea kuhatarisha maisha ya wananchi pamoja na watendaji katika eneo hilo. Mimi naomba kumuuliza Mhe. Waziri je jambo hili analijua? Na kama analijua tunataka utupatie maelezo utachukua hatua gani kuona hili suala linamalizika kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu kusema kweli niipongeze serikali kwa hatua walizozichukua wawakilishi wa majimbo. Kama walivyotangulia wenzangu kusema hapa wawakilishi wa majimbo wameanza kupata pesa za majimbo kwa hivyo hapa serikali naipongeza, lakini kwa upande wa wawakilishi wanawake bado hatujazingatiwa kupatiwa ruzuku yoyote ile, licha yakuwa wawakilishi hao wanajukumu la kuhudumia makundi wanayoyawakilisha.

Mhe. Mwenyekiti, naishauri serikali kuwapatia ruzuku wawakilishi wa viti maalum ili na wao waweze kutatua vyema changamoto zinazotukabili. Suala hili kama ninakumbuka sio mwanzo kulisemea, nakumbuka Mabaraza yaliyopita kama sisi wanawake tuna changamoto, tuna wanawake ambao wametuchagua tena sisi tunachaguliwa katika Mikoa. Kwa hivyo, na sisi tunaomba wizara suala hili itufanyie na sisi tuwe tunapata asilimia ili tuone na sisi changamoto tunaweza kuzikabili, kwa sababu na sisi wanawake tunazo changamoto. Kama tunavyofahamu changamoto zinawakibili wanawake, kama sasa hivi habari ya maafa wanaopata shida ni wanawake na watoto na viongozi wao ndio sisi wanawake. Najua wapo wanaume katika majimbo lakini sisi wanawake ndio wanaotulalamikia zaidi. Kwa hivyo, kama tungepewa na sisi tuna mfuko huu tunaingiziwa wanawake ingekuwa rahisi sana kuitekeleza kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa mchango wangu huo kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Magharibi naunga mkono ripoti hii asilimia mia juu ya mia. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante kwa mchango wako sasa anafuata Mhe. Mohammed Mgaza Jecha akifuatiwa na Mhe. Suleiman Makame wajitayarishe.

Mhe. Mohammed Mgaza Jecha: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Makamu wa Pili wa Rais. Kama inavyoonekana na mimi leo kuweza kueleza au kuchangia katika Wizara ya Makamu wa Pili shughuli zetu za bajeti. Kwanza tumpongeze Mhe. Makamu wa Pili pamoja na Waziri wake, Naibu wake na watendaji wake wote kwa hatua wanazozichukua kufanikisha wizara hii ikiwa ni mtu anayeshughulikia hali ya serikali sasa hivi. Kiongozi Mkuu wa Serikali ni Makamu wa Pili kutokana na hali hii Wizara ya Makamu wa Pili wa Rais inachukua juhudi kubwa kushughulikia masuala haya ili kuendesha nchi yetu kwa mambo yanayotokea katika kuwasilisha masuala yetu yote.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikiendelea kutoa mchango wangu ningeomba zaidi sana kuhusu hali ya athari ya mvua kutokana na wajumbe wengi wamekwishaeleza na mimi tu nilikuwa nachangia moja au mawili kuhusu masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Kampuni moja ya Kichina ipo hapa Zanzibar na kampuni ile sasa hivi inajenga mitaro kwa ajili ya mambo ya maafa kama haya yanavyotokezea. Mhe. Panya Ali Abdalla alizungumza kama jimbo lake sasa hivi limekuwa katika hali nzuri kwa ajili yakuondosha ule mtaro ulioko kule, Mwenyezi Mungu akajaalia akasema kama safari hii wamepata nafuu wao kutokana na hali ya kuondoshewa mtaro huo. Kwa hivyo, nilikuwa naomba na huko ambapo kunaitwa Mwanakwerekwe ipelekwe ile Kampuni ya Kichina ikatathmini pale kwenye lile Ziwa ijuulikane kama yale maji yataweza kuondoka au hayaondoki, kwa sababu mna sehemu nyengine wamefanikiwa wale Wachina kuyaondosha yale maji. Sasa itakuwa kila siku tu mvua zikinyesha Mwanakwerekwe kwa nini hawapeleki wale Wachina wangeenda wakaangalia pale.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba wapelekwe Wachina pale kuangalia yale maji yanayokuwa ni tatizo kubwa ambalo ni la kila mwaka linatokezea Mwanakwerekwe, Mwanakwerekwe gani hiyo isiyomalizika. Kwa sababu kama ingelikuwa kuna maelekezo mazuri yakuweza kujua kama athari zinazotokea kila mvua basi na Mwanakwerekwe ingelipewa kipaumbele tena

cha kwanza kabisa. Mheshimiwa kwa sababu mvua inapotokezea kwa Zanzibar yetu ndio jumla ya mambo yote haya yanayotokezea, kwa sababu ni mwahala mule mule hakuna mambo mapya. Mwahala mwenyewe ni mule mule Mwanakwerekwe, Kijitoupele, mara unasikia Kwahani, mara unasikia Kiembesamaki lakini mwahala mule mule ambapo kila siku inaponyesha mvua. Sasa mimi nilikuwa naomba zaidi tu hili suala la maafa lifanyiwe bajeti kama bajeti nyengine, kwa sababu inakuwa kila mwaka na tunayajua kama haya yatatokezea. Sasa kwa nini isipangiwe bajeti na hiyo ikajuulikana kama mwaka huu Mwanakwerekwe tutaiondosha, ikajuulikana kama Kiembesamaki nayo tunaiondosha. Kwa hivyo, ilikuwa naomba tu wizara ipange hili suala la bajeti kwa sababu inaonekana kwa kila kipindi inaponyesha mvua maafa yanaweza kutokezea.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi katika Jimbo langu la Mtambile nataka atueleze ni yale maafa yanayoharibu barabara tu au yale maafa yanayotokezea kuharibu gati au kuharibu pahala pengine, lakini kutokana na hivyo na sisi tumeathiriwa katika majimbo yetu. Jimbo la kwangu mimi zaidi kwa sababu kuna nyumba Kengeja 14 zimeathirika kwa ajili ya mvua hii, kuna Mtambile nyumba 6, Kangani nyumba 6 kuna shehia nyengine inaitwa Mgagadu/Mzingani zimeathirika nyumba zinafika 8. Lakini sasa hivi kutokana na hali ilivyo imeonekana tu kuna maeneo matatu ambayo yameathirika zaidi, lakini na haya ya kwetu na wananchi sasa hivi wameshajua kama athari zilizotokezea. Kwa hivyo na haya maeneo ambayo yamepata athari hizo tuweze kufikiriwa vile vile, kwa sababu wananchi wote sasa hivi wameangalia athari za mvua na masheha wameshaandika hivyo wameshajenga matumaini ya kuwa na wao watabahatika pengine kwa maafa haya yatakayotokezea.

Kwa hivyo, tulikuwa tunaomba Mheshimiwa na mule sehemu mlimopata athari kama zile za mvua tuangaliwe kwa jicho la huruma. Kwa sababu wale wote sasa hivi utapokwenda wewe Mwakilishi ndani ya jimbo lile watakutizama wewe kama unaekwenda kuondoa sasa hivi, au kwenda kuwaambia kitu. Ukienda ukifika tu, ukiwafariji kama hukuacha chochote basi watakwambia ilikuwa haina haja ya kuja, kwa sababu kila mmoja keshakuwa na matumaini ya kwamba kuna maafa yametokezea na nyumba zetu zimeanguka tunaweza tukabahatika masuala kama hayo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina maneno makubwa isipokuwa ni hayo tu kwa leo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, Mwenyezi Mungu atujaalie salama. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante kwa mchango wako, anayefuata ni Mhe. Suleiman Makame Ali na baadae atafuatia Mhe. Hassan Khamis Hafidh (Diaspora).

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nami nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi niende kwenye suala mtambuka kuhusu mazingira. Mazingira ni muhimu sana katika maisha ya kila siku kwa sababu bila ya mazingira kusema la ukweli hali ingekuwa tete.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze hii wizara ambayo iko chini ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kuhakikisha kwamba suala la mazingira linapewa kipaumbele kwa upandaji miti, lakini pia niipongeze wizara hii au ofisi hii kwa kuhakikisha kwamba mazingira wanayasimamia ipasavyo. Kwa mfano, kama kule Ndagoni wakulima si chini ya 300 walikuwa tayari wanakosa kulima mpunga, lakini kutokana na kwamba wizara hii ilivyo makini na kuhakikisha kwamba wanawafanyia kila lililo zuri wananchi wake wamelisimamia suala lile na limepigwa tuta lenye urefu wa mita kama 450 kama sikosei, ili kuhakikisha mashamba yale wakulima wanalima na wanapata zao la mpunga vizuri. Kwanza naipongeza sana wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 19 kwenye kaya masikini. Mheshimiwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Rais wetu makini Dkt. Ali Mohammed Shein kusema la kweli inakwenda vizuri na inahakikisha kwamba wananchi wanaondokana na dhiki ya kila aina. Mhe. Mwenyekiti, kwenye kaya masikini hili ni suala ambalo nataka lifikiriwe na sifikirii labda kamati kama ilikwenda kuhakikisha kwamba kuna baadhi ya kaya masikini wamekwenda kuzitembelea.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye kaya masikini nilithubutu kusema kwamba baadhi ya maeneo kuna uoza, hizi pesa wale waliokusudiwa kupewa hawazipati kama ipasavyo. Kwa sababu kuna maelezo kwamba mtu ikiwa kama hakwenda kumpeleka mtoto kliniki anakatwa pesa ile au kama atakuwa mwanawe atatoroka skuli anakatwa pesa ile. Lakini cha kushangaza baadhi ya maeneo mengine ikiwa kama kuna mkutano wa jamii, mfano kama wa shehia yote mwana kaya masikini hakwenda kwenye mkutano ule si wa masuala ya kaya masikini anakatwa pesa, ile inahusiana na nini.

Kwa mfano, niseme hapa kwamba kuna shehia moja ambayo ni Shehia yangu ya Ndagoni juzi kulikuwa na ufunguzi wa Kituo cha Afya, Mhe. Waziri wa

Afya alikwenda kule lakini taarifa kama wananchi wa Shehia ya Ndagoni wengi wao hawakuwanayo, nikapata tetesi kwamba wale waliopata pesa katika kaya masikini watakatwa pesa zile kwamba hawakuhudhuria kwenye mkutano ule. Kwa hiyo, mimi nataka kujua kwamba wanahusianaje kwamba kituo cha afya ni cha Shehia ya Ndagoni lakini leo akatwe mtu anayepewa pesa zile za kaya masikini kwa kuwa hakwenda kwenye kushiriki katika ufunguzi wa kituo cha afya, siku nyengine hata taarifa hana. Mhe. Mwenyekiti, naomba hili liangaliwe na lisimamiwe vizuri ili kuhakikisha kwamba wananchi wanaondokana na usumbufu huo.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 15 kuhusu masuala ya pesa ambazo zinatoka kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na kusaidia jamii katika Zanzibar nzima tuseme. Mhe. Mwenyekiti, nimeona hapa kwamba Jimbo la Mhe. Balozi, Makamu wa Pili wa Rais kama alivyosema jana Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kuna mambo kidogo, namsifu kwa sababu ni kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, hilo naliunga mkono asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, hapa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais iliahidi kompyuta mbili tu na *printer* moja kule Ndagoni, ambapo kama ni kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, lakini imeshindwa kufanya hivyo mpaka jana nikaambiwa kwamba hali itakaporuhusu. Sasa mimi najua kwamba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sharifu hili anaweza kulifanya, lakini mimi nilitaka nijue hizi kompyuta mbili na *printer* moja zina gharama kiasi gani hata ifike miaka minne wananchi wale washindwe kupewa kompyuta zile ambazo ni ahadi kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Inasikitisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama ingelikuwa sikuogopa kuingilia ahadi ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sharifu, maana nimwite Sharifu kwa sababu yeye dua yake akiomba labda huwa hairudi, aliniombea dua kwamba nitakuwa Mwakilishi na ni kweli imekubaliwa Mwenyezi Mungu ameipokea dua yake; kama ingelikuwa sikuona tabu kuingilia ahadi yake basi mimi ningelikuwa tayari nishazitoa zile kompyuta na *printer* moja aliyoahidi.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki niseme mengi sana hayo yanatosha naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, anayefuata Mhe. Hassan Diaspora na baadae atafuatia Mhe. Rashid Makame Shamsi na kama muda upo atafuatia Mhe. Miraji Khamis Kwaza.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana na mimi kunipa fursa hii ya kuwa mchangiaji katika hotuba hii ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambayo waziri wake kaka yangu Mhe. Mohammed Aboud Mohammed na naibu wake ndugu yangu Mhe. Mihayo Juma N'hunga, Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Mwera anayeishi katika Jimbo la Welezo.

Mhe. Mwenyekiti, pili napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Welezo kwa kunichagua na kuwapa pole na maafa yaliyotukuta sisi wana Welezo ya mvua iliyosababishwa na Mwenyezi Mumgu, ahadi yangu kwao tutashirikiana bega kwa bega katika kutatua matatizo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, tatu nachukua fursa hii kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuwaongezea mishahara wananchi, wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asilimia mia moja. Nataka kumpa pongezi wafanyakazi wote wa serikali wamependezewa na wamefurahi na kila siku wanamuombea dua aendelee kuiongoza Zanzibar kama anavyoiongoza kwa busara.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kuchangia bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kama ifuatavyo: Mheshimiwa nitaanza na Tume ya Uchaguzi. Tume ya Uchaguzi kama sikosei ina jukumu la kusimamia uchaguzi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapofika muda wake, tumeona tarehe 25 Oktoba tulikuwa na uchaguzi mkuu. Mheshimiwa uchaguzi mkuu wa tarehe 25 Oktoba, 2016 haukwenda vizuri, kuna sababu nyingi za msingi zilizosababisha uchaguzi ule usiende vizuri na hatimae kufikia uchaguzi ule kufutwa ikabidi urejewe. Katika kufutwa uchaguzi ule tuna kila sababu ya kumpongeza Al-haj Jecha Salum Jecha kwa kutufutia uchaguzi na kutufanyia uchaguzi mwengine na Baraza hili leo tuna Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Tisa ambao wote *almost* ni wanachama kutoka Chama cha Mapinduzi na chama rafiki, lakini wote wana lengo la kuyalinda na kuyatetea Mapinduzi Matukufu ya Januari, 1964 kwa maendeleo ya wakwezi na wakulima.

Mhe. Mwenyekiti, sababu moja iliyofanya uchaguzi ule uharibike ilikuwa ni katiba, maneno yaliyokuwemo ndani ya Katiba ya Zanzibar kipengele namba 19 Tume ya Uchaguzi. Kipengele (c) kinamtaka Rais wa Zanzibar anapoteuwa wajumbe wa Tume ya Uchaguzi lazima ashauriane na kiongozi wa upinzani. Mimi nataka kusema mambo mawili Mhe. Mwenyekiti, leo tunataka kuipitishia mabilioni ya pesa Tume ya Uchaguzi, lakini Katiba ya Serikali ya Mapinduzi inamtaka Rais wa Serikali ya Mapinduzi anapotaka kuteuwa wajumbe wa tume lazima ashauriane na watu kutoka chama cha upinzani.

Mhe. Mwenyekiti, katika nchi ya Kimapinduzi suala hili sio sahihi, hawezi Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kushauriana na mpinzani katika kuteuwa wajumbe wa tume, wajumbe ambao kwa jina la babu yangu alinihusia alinambia Hassan mjukuu wangu mtu yeyote Mzanzibari ambaye hayatambui na hayathamini Mapinduzi Matukufu huyo ni Hizbu. Sasa mtu ambaye hayatambui Mapinduzi Matukufu aingie katika Tume ya Uchaguzi kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kitu ambacho sisi na wao tunatofautiana ki-*ideology, outcome* yake ndio yale yaliyotokea kutuvurugia uchaguzi uliotokea tarehe 25 Oktoba, umevurugika kutokana na kuwa katiba inamruhusu na inamtaka Rais aweze kuwa na Hizbu ndani ya Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kupitia hii mimi Hassan Khamis Hafidh nimeona aa, hii katiba haiko sahihi. Mimi nitapokuwa Rais kwa sababu nina nia ya kuchukua fomu nataka nimwambie Mwanasheria Mkuu mambo haya, mimi sitokuja kuyataka haya, naweza nikampa nafsi katika serikali yangu lakini kwanza anihakikishie kwamba atafuta mambo haya yanayowapa Hizbu *room* kuwemo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar watu ambao hawayatambui Mapinduzi moja Tume ya Uchaguzi lazima afute na mambo mengi yamo. Katiba inaeleza wazi wazi ni Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lakini ndani yake inatoa *room* kwa Hizbu kuwemo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kitu ambacho si sahihi. *This is Revolution Government of Zanzibar, if you are Hizbu you have no chance to be one of the member of the Government Zanzibar.*

Mhe. Mwenyekiti, kwa hapo naomba Mwanasheria Mkuu ajue, ninayo nia ya kugombania urais na nikiwa mimi rais ahakikishe kwamba anatafuta vipengele vyake vya sheria vinavyoweza kufuta Hizbu kuwemo katika serikali yangu, nitampa masaa kumi. Mzee Abeid Amani Karume alisema mtapokuja kuwatafuta wasomi wanaweza wakaja wakatuharibia. Sasa Mwanasheria Mkuu najua ni msomi tusiende watutengezee hii sio katiba sahihi, vipengele vyengine haviko sahihi. Kwa sababu hawayathamini Mapinduzi yanayachafua Mapinduzi. Hiyo ilikuwa kuhusu Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda kwenye maafa. Idara ya Maafa ni miongoni mwa idara katika Ofisi ya Makamu wa Pili tunaiba pesa nyingi sana, lakini kinachonishangaza idara hii ipo kusubiri maafa, jana nilisema imekaa kama mchimba makaburi. Sasa mimi hapa nataka kuiomba tu iwe *proactive* Idara ya Maafa, hebu iwe kama Idara ya Maafa ya Washington, Marekani ambayo kazi yake kubwa ni ku-*manage* na kufanya *research* katika kukabiliana na maafa, lakini pia kuyalinda maafa yasitokezee. Hakuna asiyejua mvua za masika

zikiongoka kuwa zitasababisha maafa, sasa Idara ya Maafa inapewa mapesa chungunzima kuyaombea maafa yatokee hii sio sahihi. Naomba wabadilike kama Rais wetu anavyosema wajue jinsi gani ya kuyalinda maafa yasitokee Zanzibar, lakini inapobidi kutokezea wafanye jukumu la kuya-*manage*.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda kwenye Sherehe na Mapambo. Idara hii ni miongoni mwa idara katika Ofisi ya Makamu wa Pili. Mhe. Mwenyekiti, hapa sina mengi bali nataka kusema wazi wazi, tumekuwa tunauona utaratibu mbovu usiofurahisha kumkuta mtu asiyehusika ana kadi ya *VIP* kubwa A au B unamkuta kakaa na Balozi wa Nchi za Nje waseme nini hawajui. Mheshimiwa haya sio sahihi naiomba idara hii kwenye sherehe zote za serikali za kitaifa kadi hizi zitizamwe nani tunampa. Kwa sababu unamkuta Mhe. Mwakilishi aliyepata uwakilishi kwa shida hana kadi lakini mpambe huko nje anayo kadi tena ya *VIP* kubwa, njia hii sio sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda katika uratibu wa shughuli za SMZ, pia hii ni idara moja katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais nitaanza moja kwa moja katika suala la Muungano. Mhe. Mwenyekiti, katika suala la Muungano juzi tumeshuhudia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limepitisha sheria tunayoiita *Refundable Tax* kuiondosha. Zamani ilikuwa kinachokuja Zanzibar *tax* inakuwa *collected* kule kule Dar es Salaam halafu *ZRB* wanakwenda kuchukua pesa zetu. Juzi wamepitisha sheria kwamba zile *tax* tu-*collect* wenyewe sasa nini *outcome* yake.

Mhe. Mwenyekiti, *outcome* yake kwamba wafanyabiashara wadogo wadogo wameshindwa kufanya biashara bana ya Tanzania Bara na Zanzibar kwa sababu wanatozwa mara mbili, wanatozwa *tax* Bara na wanatozwa *tax* Zanzibar wanapoingia na mzigo wao. Najua na ukweli kwamba unapoliuliza unaambiwa ah, wabunge wenu ilipopita hii sheria si wapo? Kweli wabunge wapo hapa mimi nawaomba tu Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanatakiwa jamani kuitetea Zanzibar sio kwenda kuchukua pesa kule Bungeni, kuitetea Zanzibar kwa mambo kama haya yanapopita wayalinde kwa manufaa ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kinachonishangaza! Najua mambo kama haya kabla ya kukaa kuna vikao Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Wizara ya Fedha na Uchumi, sasa ukiangalia kunako bajeti bilioni za pesa zimetumika vikao vimekaa lakini sasa vikao hivi kinachonishangaza vimekaa kupitisha mambo kama haya ambayo yana lengo la kuwasumbua kidogo wananchi wetu wafanyabiashara kwa sababu imekuwa vigumu. Sasa naomba mambo kama haya tusiwe tunayakubali kwa sababu hayaleti tija nzuri kwa maendeleo ya

Zanzibar. Leo hii mfanyabiashara mdogo anashindwa kufanya biashara, wafanyabiashara wengi Zanzibar wameshakaa kitako hawawezi tena kufanya biashara kwa sababu wanapata *double taxation* baina ya Bara na Zanzibar na hii ni Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda upande wa Polisi. Kwanza napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mkuu wa *Traffic* Zanzibar, Mkuu wa *Traffic* Zanzibar anafanya kazi nzuri. Juzi nilikuwa namsikia anavyotoa *analysis* ya ajali alivyolenga kupunguza ajali; asiyemjua Mkuu wa *Traffic* Ndugu Mkadam ni aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini. Mimi nampongeza sana aendelee uzi huo huo, lakini Mhe. Mwenyekiti Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni ofisi moja inayoshughulikia mambo ya Muungano, hawa Polisi wanapata shida halafu tunawalaumu hata bajeti ya mafuta wanakuwa hawana tuwe tunawapa.

Kwa mfano, mafuta Pemba kuwachukua mahabusu kutoka Wete kuwapeleka Mkoani inashindikana kwa sababu hawana pesa ya mafuta. Sasa jambo hili sio sahihi tuwape mafuta, tuwawezesheni na kama hawapewi tuwasimamie wapate ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi, kwa sasa hivi Mheshimiwa wanafanya kazi nzuri nampongeza sana kaka yangu Mkadam aendelee uzi huo huo na Mwenyezi Mungu atamjaalia.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije katika kesi ya mchanga. Naamini ndio miongoni mwa inayofanya uratibu mambo ya SMZ, Mheshimiwa bila ya kutafuna maneno *issue* ya mchanga kwa Zanzibar imekuwa ni *issue* mbaya kwa wananchi, imepelekea serikali yetu kusemwa vibaya na wananchi na kwa sababu ya bei ya mchanga wafanyabiashara wameupandisha vibaya wanafanya wanavyotaka. Nilisema katika bajeti yangu hakuna mfanyabiashara mwenye dini, dini ya mfanyabiashara ni faida na kitabu chake ghilba. Serikali imetoa bei elekezi na bei elekezi hizo hazifuatwi na wafanyabiashara ya mchanga, naiomba serikali isimamie wananchi wake wananyanyaswa katika kuuziwa mchanga na hawana pengine pa kuupata mchanga lazima waupate.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hilo naomba kusema kwenye Ofisi ya Faragha. Mheshimiwa kuna Ofisi ya Faragha pia tunaipa pesa naomba ifanye kazi vizuri ofisi hii kwa sababu imeleta aibu kubwa hapa, kuona Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwamba, utaona mbona pesa za serikali zinatumika jimboni. Mimi namkubali sadaka huanza nyumbani, lakini mimi nakataa Mhe. Makamu wa Rais pesa anazo za kutosha hawezi kutumia fedha ya serikali jimboni, lakini hii imetokana na maandishi na kutokuwa na umakini wa ofisi ya faragha. Kabla havijaletwa vitabu jamani tuvitizameni hiki ni chombo kikubwa, leo tunakuja

hapa tunaleta aibu kwa Makamu wetu wa Pili wa Rais kitu ambacho si sahihi. Mimi naamini Makamu wa Pili wa Rais pesa ya serikali hajaitumia kutumia mambo yake ya jimboni lakini haya ni *error* ya maandishi ya kibinadamu.

Pia nachukua fursa hii kumualika Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aje Jimbo la Welezo na siku hiyo akitaka atapiga *lunch*, atapiga *dinner*, aje kutembelea jimbo hilo aone changamoto zinazozikabili jimbo la Welezo, naamini kwa cheo chake na ujembe wake atatoa amri zitekelezwe zile changamoto zinazotukabili sisi watu wa Welezo ikiwemo barabara ya Hawai ambayo Mhe. Rais ameiahidi kuitengeneza, huu ni mwaka wa tatu na nusu haijatengenezwa. Kwa hivyo, naiomba Ofisi ya Faragha iliratibu hili namualika mimi Mwakilishi wa wananchi jimbo la Welezo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aje kutembelea Welezo ili atusaidie changamoto.

Utaratibu

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Mhe. Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mchangiaji anapotosha umma kwa kusema kitabu hiki kimekosewa, kitabu hiki kimeletwa sahihi na wenyewe hawakusema kama kimekosewa. Kwa hivyo, asiseme kama kuna *error* ya uandishi kitabu hiki kiko sahihi naomba nimpe taarifa.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, ahsante lakini naomba nimuweke sawa Mheshimiwa aliyesema mimi kiswahili najua na nimesoma. Nilisema naamini kitabu hichi kimekosewa. Sasa kama unajua kiswahili utajua nini maani yake sijathibitisha kama kimekosema, nilisema naamini kiswahili changu cha mjini cha kusoma na cha kwetu Mchangani sikosei.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hassan Khamis Hafidh una dakika mbili.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo Afisi ya SMZ Dar es Salaam Mhe. Mwenyekiti, naamini Afisi ya SMZ Dar es Salaam inafanya mambo mazuri na naomba iongezewe bajeti inafanya uratibu mzuri katika kusimamia shughuli za SMZ kule Tanzania Bara. Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba kusema kwamba waongezewe bajeti na mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho ni *issue* ya madawa ya kulevya. Katika *issue* ya madawa ya kulevya kwa heshima muda wangu umebakia dakika nne naziona nakuomba sana kuna nyumba iko hapa Kidimni imeshapewa mapesa mengi

Mhe. Mwenyekiti hebu tupewe hasa kiasi gani imetumia kiasi gani kimebakia na mpaka leo wameshatumia kiasi gani nyumba yenyewe haiendani na pesa yenyewe iliyopewa hebu tupewe hesabu kamili.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kuna mambo ya Muungano. Mhe. Mwenyekiti, katika Katiba ya Tanzania mambo ya Muungamo ni 22 ikiwemo mafuta na gesi asilia. Naomba nije kujibiwa Mhe. Mwenyekiti, Elimu ya Juu tumeambiwa ni Muungano sasa mbona wafanyakazi wa Elimu ya Juu Zanzibar hawalipwi mshahara na Taasisi ya Muungano kama wanavyolipwa Wizara ya Mambo ya Ndani, Usalama, Jeshi. Kwa nini hawalipwi na lini wataanza kulipwa ni hii Idara ya Muungano hii Elimu ya Juu inaaza wapi haswa hilo la kwanza.

Pili Mhe. Mwenyekiti, mafuta na gesi, tunaambiwa mafuta ni mali ya Muungano kwa mujibu wa katiba na wanainuka viongozi Bara wanafanya kejeli na sie tushapitisha sheria. Naiomba serikali kupitia Afisi ya Makamu wa Pili naiomba iitake Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupeleka mswada wa kufuta katika orodha wa mambo ya Muungano mafuta na gesi ili Wazanzibari tupate kuanza kuyachimba mafuta yetu kwa sababu kwa sasa hivi katiba ni mali ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hiyo Takwimu nayo imo katika orodha ya mambo ya Muungano. Nataka kujua Afisi ya Takwimu Zanzibar iko wapi na hizo takwimu mbona hawalipwi mshahara na watu wa Muungano tunaowalipa katika Bajeti ya SMZ nataka Mhe. Waziri anieleze hilo.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, taasisi inayohusu

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umemaliza.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Nataka kujua utafiti gani umefanyika na Afsi ya Utafiti ya Muungano Zanzibar iko wapi na wanalipwa mshahara na ina ajira ngapi na utafiti gani umefanyika na faida yake ni nini na wao wako wapi.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache na kwa heshima kubwa naomba kuiunga mkono bajeti hii asilimia 50 mpaka nitakapojibiwa masuala yangu nitaunga mkono yote. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kulingana na orodha ulivyokuwa mkubwa na wachangiaji wapo wengi pamoja na kuwa tunaona muda upo, lakini ni vyema nitoe tahadhari wale ambao kuwa watakuwa tayari waweze

kuchangia kwa maandishi. Kwa sababu orodha hapa bado ni wengi hata tukigawa muda huo itakuwa hautoshi.

Kwa hivyo, Waheshimiwa wafuatao itabidi wajiandae kwa kuchangia kwa maandishi kama hali itaruhusu tutapunguza afuatae ni Mhe. Ali Khamis Bakar, Mhe. Hidaya Ali Makame, Mhe. Bihindi Hamad Khamis, Mhe. Khadija Omar Kibano, Mhe. Zulfa Mmaka Omar na Mhe. Panya Ali Abdalla hawa wajiandae kwa kuchangia kwa maandishi.

Kama muda utakuwa unabakia tunaweza tukapungza. Ahsanteni. tunaendelea.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuichangia hotuba hii ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Lakini kabda sijafanya hivyo, nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na watendaji wake wote katika kuiandaa na kuiandika vyema hotuba hii muhimu ya bajeti ya wizara inayohusika.

Nichukuwe fursa vile vile kuipongeza Kamati ya Kusimamia Viongozi wa Serikali chini ya Mwenyekiti wake mahiri Mhe. Omar Seif Mwakilishi makini wa Jimbo la Konde. Lakini niwapongeze Wajumbe wote walionitanguliwa kwa kuweza kuwasilisha michango yao kwa ufasaha ambayo itaisaidia na kuiweka vizuri hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika afisi yake.

Mhe. Mwenyekiti, sina budi kabla ya kutoa michango yangu kutoa pole kwa wale wote Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla ambao wamepatwa na maafa katika kipindi hichi cha mvua zinazoendelea na hususan wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika michango yangu kwa kuanza na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Mhe. Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo ni mfuko muhimu sana kwa ajili ya kuibua miradi mbali mbali ndani ya majimbo yetu ambayo wakati mwengine inarahisisha katika kupunguza changamoto zinazowakabili wananchi wetu. Niishukuru Afisi ya Makamu wa Pili kwa kuweza kutuwezesha Waheshimiwa Wawakilishi mpaka hivi sasa kuweza kupata fedha za Mfuko wa Jimbo wa mwaka 2016/2017.

Pamoja na shukurani hizo niseme kwamba Mfuko wa Jimbo kwa kweli ni mfuko ambao unatusaidia sana sisi Wawakilishi katika kupunguza changamoto na tunapopunguza changamoto maana yake vile vile tunarahisisha kuipunguzia

changamoto Serikali Kuu. Inaonekana kwamba kwa *trend* inavyoonesha mfuko wa jimbo ulianza mwaka 2011/12 na ulianza na shlilingi milioni kumi. Lakini 2012/2013 zikaongezeka zikawa kumi na tano milioni 2013/2014 milioni kumi na tano lakini 2014/2015 mfuko wa jimbo ukaongezeka ukawa milioni ishirini. Mfuko ambao tumetiliwa hivi sasa ulikuwa ni milioni ishirini inaonekana kuna *trend* ya miaka miwili miwili. Ningeiomba sana wizara inayohusika basi kufikiria kwamba mfuko utakaokuja 2017/18 basi tuwe na ongezeko la shilingi milioni tano iwe milioni ishirini na tano.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto ndani ya majimbo zinaongezeka siku hadi siku na hali ya maisha inaongezeka ni vyema kuweza kufikiria kuongeza milioni tano katika mfuko ambao tunautarajia mwaka huu kuupata. Lakini pamoja na hayo kuna wenzetu wa viti maalum, tunawenzetu wanaowakilisha walemavu makundi yao haya yamo ndani ya majimbo na wao vile vile wanakabiliwa na changamoto. Tuiombe wizara inayohusika kuweza kufikiria kuwapa mfuko na wao wa kuweza kusaidia makundi yao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano Wawakilishi wa walemavu ndani ya Baraza hili wako wawili ambao wanawakilisha walemavu wote wa Zanzibar Unguja na Pemba kama hatukuwapa mfuko hawa kwa kweli hawezi kusaidia makundi yao. Kuna makundi ya vijana ambayo yana Mkoa mzima, kuna makundi ya akina mama yana Mkoa mzima. Kwa hivyo, nina imani kwamba makundi haya yatakapopewa na wao mfuko watasaidiana na sisi Wawakilishi tuliochanguliwa na wananchi katika kuona kwamba changamoto zilizomo katika majimbo tunazipunguza kadiri iwezekanavyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba hii ilisemwa kuna mafunzo ambayo yametolewa, lakini niungane na wenzangu kuna haja ya kuendelea kutoa mafunzo kwa kamati za mifuko ya majimbo nyengine hazijapata mafunzo Mhe. Mwenyekiti. Lakini na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili tuweze kusimamia uzuri mifuko hii basi naomba sana mafunzo yatolewe mara moja baada ya bajeti hii ili kuona kwamba tuna uelewa mkubwa wa kuweza kusimamia matumizi sahihi na taratibu za mfuko huu.

Mhe. Mwenyekiti, nielekee sasa katika masuala yanayohusiana na watu wenye ulemavu. Mhe. Mwenyekiti, sisi sote tuliomo ndani humu ni walemavu watarajiwa kama mtu hana ulemavu basi atarajie katika maisha haya kwamba anaweza akapata ulemavu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, la kushangaza sana katika bajeti ambayo imepita Mwakilishi anaewakilisha walemavu amesema lakini na mimi naomba nikomelee msumari ukweli bajeti ambayo walitengewa na fedha walizotiliwa asilimia 22 hatuwatendea haki hata kidogo walemavu wenzetu

wanakabiliwa na changamoto nyingi sana, wana mahitaji maalum mengi sana, wanakabiliwa na umasikini ukilinganisha na sisi, wanataka elimu bora, wanataka afya bora. Kwa kweli hatuwatendea haki niiombe sana wizara inayohusika kuweza kulitazama hili katika bajeti hii kama inawezekana basi tufanye *adjustment* kutoa kutoa kifungu katika bajeti moja tuwaongeze na kwa robo hii iliyobakia ya miezi mitatu basi kama kuna fedha basi watiliwe.

Mhe. Mwenyekiti, walemavu ni watu kama watu wengine kwa hivyo, hali hii kwamba vifungu vyote ambavyo tulipitisha wao ndio wapate asilimia ndogo kwa kweli hatukutenda haki Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nielekee katika Tume ya Ukimwi. Mheshimiwa tukubali kwamba bado tuna janga la ukimwi japo inaonekana kwamba hivi sasa kama tumelinyamazia tumelifumbia macho kwa sababu hata ndani ya vyombo vya habari zile hewe hewe zinazohusina na ukimwi hizisikii ukilinganisha na nyuma. Najua kwamba wahisani au wafadhili wetu wamepunguza michango yao katika kusaidia harakati za kupiga vita ukimwi na mambukizo yake. Lakini Mhe. Mwenyekiti, tukitizama bajeti ile ya mwaka jana na bajeti ya mwaka huu inaonekana bajeti imeshuka baada ya kupanda.

Mwaka jana tulikuwa na bilioni 1.2 mara hii tuna milioni mia nane na arubaini na sita wakati tunalazimika kuendeleza mapambano zidi ya ukimwi. Tukubali tusikubali vitendo, matukio ambayo yanaashiria kuongezeka kwa virusi hivi sasa ni mengi ukilinganisha na nyuma. Ningeiomba sana wizara inayohusika kuweza kuitazama bajeti hii pamoja na wahisani kupunguza misaada yao lakini tuangalie suala hili kwa umakini vyenginevyo kama hatukupiga hewe hewe Mhe. Mwenyekiti, tutakuja kujishitukia pabaya tutapoteza nguvu kazi nyingi tutapoteza vijana wengi sana.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa kuna gesti bubu nyingi, kuna disko kwa wingi, kuna ubakaji mwingi kuna vitendo vya uasharati vingi, hivi vyote ni viashiria vya kuongezeka kwa virusi vya ukimwi. Sasa leo tunapopunguza bajeti sijui tutakua tunaelekea wapi. Ningeiomba sana wizara kuweza kufikiria fungu hili bajeti inayohusiana na ukimwi kuweza kuongezwa ili kuinusu jamii yetu ile harakati za kupiga vita maambukizi ya ukimwi ziweze kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika suala zima la udhibiti wa dawa za kulevya. Mhe. Mwenyekiti, hili ni janga la madawa ya kulevya na niipongeze sana serikali kwa juhudi zake inayochukuwa imeunda tume ya kitaifa ya kuweza kukabiliana na suala hili la madawa ya kulevya lakini bado juhudi zinahitajika.

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha kidogo katika bajeti iliyopita katika suala la udhibiti wa dawa za kulevya wenzetu wamepata pesa asilimia ishirini na nane katika asilimia mia. Nayo niseme kwamba suala hili au bajeti hii wenzetu wa udhibiti wa madawa ya kulevya hatujawatendea haki. Hili janga ni kubwa lakini kwa nini sasa asilimia ya fedha iwe ndogo. Mimi nafikiri tuwe makini kama tunataka kuweza kuhakikisha kwamba nchi hii iwe salama na suala la dawa za kulevya kwanza tuhakikishe bajeti yetu inakuwa nzuri na hii ndio itakayofanya zile program pamoja na shughuli ambazo tumejipangia ziweze kutekelezeka. Vinginevyo hatuwezi kufikia lile lengo tunalolitaka hasa la kuweza kuondosha janga hili la madawa ya kulevya ambalo linaathiri sana vijana wetu.
Juzi katika vyombo vya habari kuna Tume ya Kuratibu na kudhibiti dawa za kulevya wanasikitika hata mazingira wanayofanyia kazi sio mazuri. Mheshimiwa Naibu nimpongeze ameenda kuzungunza nao. Sasa hii ni ishara kwamba bado hatujawa makini katika kuona kwamba suala hili au tatizo hili linaondoka. Lakini hata katika hotuba yetu hatuoni takwimu zinazohusiana na suala hili kuweza kuona ukubwa au udogo wa tatizo hili na hapa nipende niseme Mhe. Mwenyekiti, bajeti hii ambayo tunaipitisha ukweli imekosa jaduweli za kitakwimu nyingi ambazo zilikuwa zinaulazima ziweze kupatikana.

Bajeti nzuri na ambayo inaweza ikamfanya mtu kuweza kujenga imani juu ya fedha tunazozipitisha ni ile ambayo inasheheni takwimu ichanganue takwimu vizuri. Hapa tulitakiwa tuweze kuona mchanganuo wa masuala la ulemavu, mchanganuo wa masuala la ukimwi pamoja na mchanganuo wa masuala ya madawa la kulevya. Hii ingeweza kutusaidia sana katika kuchangia vizuri bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie sasa na suala la mapato. Mhe. Mwenyekiti, tumeelezwa kuhusiana na suala la mapato wizara yetu hii katika bajeti ya mwaka jana ni kwamba ilikuwa na vianzo viwili Mhe. Yussuf Hassan Iddi alilichangia vizuri, ilikuwa na vyanzo viwili. Chanzo kimoja ni Wakala wa Upigaji Chapa. Wakala wa Upigaji Chapa ndio chanzo ambacho kina fedha nyingi za mapato, la kushangaza sana katika kitabu hichi na hata ukienda kwenye kitabu kikubwa chanzo hichi hakionekani, chanzo kilichopo ni cha ukodishaji wa milango na vifaa vya Sherehe na Mapambo. Kwa kweli inawezekana wenzetu wamesahau na kama wamesahau basi watwambie watakapokuja kwa sababu hichi ndio chanzo kikubwa cha mapato katika wizara hii.

Lakini katika kitabu kikubwa unapoangalia kuna chanzo ambacho kimetajwa cha Tume ya Uchaguzi ambazo ni karibu shilingi laki nne na kidogo. Sasa hichi chanzo sijui kina vitu gani kinavyochangia hizi laki nne na kidogo.

Naomba Mheshimiwa atakapokuja tuweze kukiona chanzo hichi kiko vipi kwa sababu itakuwa ni chanzo kipya kwa mwaka huu. Lakini la kushangaza vile vile kwamba chanzo hichi hakimo sasa katika hii hotuba ndani ya kitabu kidogo, hiki chanzo cha Tume ya Uchaguzi. Kwa hivyo, ningependa marekebisho hayo yafanyike ili wajumbe tuweze kujiridhisha kuweza kuona kwamba vyanzo hivi viko makini, viko sawa na vina changia hii wizara na vile vile kujiridhisha kwamba ile asilimia ambayo inapatikana basi iwe inaendana na uhalisi.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii kumuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha, tunapitia katika wizara nyingi ambazo zinawekwa hizi *ceiling* za mapato, lakini sijui ni vigezo gani ambavyo vinapitiwa ili kuweza kuiwekea *ceiling* ya mapato wizara au taasisi inayohusika.

Kwa mfano hata wizara hii, kwenye masuala yanayohusiana na vifaa kuna shilingi milioni 12 na zaidi. Tuwashukuru wenzetu wamewaza kukusanya kwa asilimia 98, tuwashukuru sana. Lakini ni kweli shilingi milioni 12 zilikuwa halisi, hatukuwa na uwezo wa kukusanya ziaidi ya shilingi milioni 12. Nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha kuweza kutazama vyanzo, watendaji wake waweze ku-*study* vyanzo mbali mbali vya mapato ili kuweza kuona kwamba vyanzo hivyo vina uhalisi. Kwa sababu mtu anaweza akakuambia kavuka makadirio ya mapato, lakini kumbe kile kiwango cha *ceiling* alichowekewa kilikuwa ni kidogo. Kwa hivyo, tutakuwa tunajidanganya na mapato ya serikali yatakuwa yanavuja.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naona unajiandaa hapo lakini mimi niunge mkono hotuba hii kwa asilimia mia na nikushukuru sana kwa nafasi hii ulionipa. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuwa miongoni mwa wachangiaji wa hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Lakini na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwa hotuba hii na uwasilishaji mzuri. Lakini pia niwapongeze wasaidizi wake Mhe. Naibu Waziri na Makatibu Wakuu kwa kazi nzuri na uchambuzi mzuri wa bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye kitabu moja kwa moja kuchangia eneo la hali ya uchumi wa Zanzibar. Katika ripoti hii tumeoneshwa hapa taarifa ya hali ya uchumi, mwaka wa fedha 2015/2016 kulikuwa kuna asilimia 6.5 ukuaji, lakini mwaka 2017/2018 iko kwenye asilimia 6.8, ni asilimia chache sana ambayo inaonekana uchumi wetu kuongezeka. Maana kutoka asilimia 6.5 kwenda katika asilimia 6.8 nasema ukuaji wa uchumi hatukuenda vizuri, hatukushuka lakini pia hatukupanda vizuri.

Kwa hivyo, nichukuwe fursa hii niishauri tu serikali kwa ujumla wake pamoja na kuwa bajeti ya Wizara ya Fedha inakuja, lakini tunaweza tukachangia hapa tukapunguza maneno kule, kwa sababu hali ya uchumi imezungumzwa ukuaji wake.

Kwanza niongeze jitihada, najua jitihada zipo, lakini iongeze jitihada kwa makusudi katika kuvisimamia vianzio vya mapato viliopo. Mjumbe mwenzangu katika uchangiaji wake alisema serikali haijawa na mfumo mzuri hata kutoa yale makadirio kwa wizara. Mfumo huu hauwezi kupatikana kama Wizara ya Fedha yenyewe kupitia idara yake ya mapato, ambayo kama sikosei ni idara mpya tu kabisa, haijafanya *study* ya vianzio vyote tulivyonavyo na ikawa inapita na inashauri kwa zile taasisi ambazo ni wakala wetu wa kutukusanyia mapato. Naweza kusema zipo taasisi kubwa zinakusanya mapato vizuri, lakini makisio wanajipangia wenyewe, kwa maana malengo. Lakini na kile ambacho wanakusanya pia majawabu wanayatoa wenyewe.

Kwa hivyo, idara hii ifanye kazi vizuri ili angalau kwa vile vianzio tulivyonavyo, basi mapato yaongezeke, huduma ziongezeka na uchumi uweze kupanda. Naomba sana kwenye eneo hili serikali kwa ujumla wake basi iendelee kusimamia, lakini endelee kufanya *study* ya kila kianzio ambacho tunacho kwanza, tuvisimamie vile tulivyonavyo ili tuone tutafikia wapi. Nasema idara hii ambayo inasimamia tathmini kwa ujumla wake wa vianzio vyetu basi ifanye kazi vizuri.

Lakini eneo jengine naishauri tena serikali katika kukuza uchumi, basi na sisi tuanzishe ile *conversion centre*, itatusaidia kuongeza mapato kwa sababu mikutano mingi mikubwa na mikutano mashuhuri inaweza kufanyika ndani ya nchi yetu. Lakini tukianzisha ile basi pia tutakuwa tunaongeza namna bora pia ya wale wenzetu watakaokuja kufanya mikutano katika *conversion centre* hii, basi watalala kwa maana ile *accommodation* watapata hapa, lakini watatalii hapa angalau *shopping* ndogo ndani ya nchi yetu watafanya.

Kwa hivyo, tuanzishe hii inaweza kutusaidia kuongeza mapato na uchumi wetu ukaongezeka. Lakini pia niishauri serikali, kwa sababu nchi yetu imezungukwa na bahari, leo ukiiangalia nchi yetu pamoja na kuwa imezungukwa na bahari, lakini hatuna chuo cha mabaharia. Kwa hivyo, ni lazima serikali sasa i- *focus* kwenye kuanzisha *marine institute* hizi ambazo zitatoa mabaharia wataongeza ajira, watakwenda kufanya kazi nje na wataleta pesa za kigeni ndani na uchumi utaongezeka.

Kwa hivyo, naomba nimalizie katika eneo hili la uchumi kwa kuishauri serikali kuanzisha pia *shipping cargo*, ambayo itatusaidia kupokea meli nyingi za kigeni kuja kushusha mizigo yake hapa, kutakuwa kuna faida kubwa, kuna *warehousing* nyingi zitajengwa zitafanyakazi vizuri. Lakini pia tutakuwa tuna uwezo wa kupokea hata wageni wengine kwa kupitia utaratibu wa kuanzisha *shipping cargo* hizi kuja kuweza kusaidia uchumi wa nchi yetu. Kwa hivyo, niombe katika maeneo haya kwa uchache tu, yale mengine nitakuja kuyataja siku ya bajeti kuu ya Wizara ya Fedha.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nisogee eneo jengine la Tume ya Uchaguzi. Nilipoangalia katika bajeti hii wamepangiwa programu mbili. Moja uendeshaji wa shughuli za uchaguzi. Lakini mbili usimamizi wa kazi na uratibu wa masuala ya utawala. Niseme tu katika programu zote mbili hazikuzingatia zile changamoto za Tume ya Uchaguzi. Juzi tu mwezi Disemba ilitolewa ripoti hii ya Tume ya Uchaguzi, na ukiisoma kwa undani wake yako maeneo muhimu yameainishwa, na kuainisha zile changamoto zenyewe za uchaguzi. Kwa hivyo, bajeti na programu hizi zilizopangiwa hatukuzingatia zile changamoto zao walioziainisha wenyewe, watafanyakazi vipi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna eneo humu naomba nilinukuu. Wanasema tume inaendelea kukabiliwa na ufinyu wa majengo ya Ofisi za Wilaya Unguja na Pemba. Aidha, kutokana na majengo katika Wilaya ya Magharibi A, Magharibi B ambazo zina idadi kubwa ya wapiga kura, na wananchi wanahitaji kuhudumiwa wanapata usumbufu mkubwa. Leo tumeleta bajeti haikuzingatia na tunaelekea kwenye uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Magharibi A na B, maana zamani tulikuwa tunaita Magharibi, wako katika Wilaya ya Mjini pale, Wilaya ya Mjini hapa Magharibi hapa Maisara. Wanatoka Wilaya ya Magharibi huku wanaingia Wilaya nyengine ndio wanakutana na Ofisi ya Tume, na hiyo ofisi ukiingia mule unakuta wakiingia wafanyakazi wanne au watano hata huyo anayekuja kutafuta huduma hapati kiti cha kukaa, maana nafasi haipo.

Kwa hivyo, tumeleta bajeti imezingatia maeneo mengine, lakini yale maeneo ambayo wenyewe wameyasema katika taarifa yao hayakuzingatiwa. Sasa nimuombe tu Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atuambie serikali itachukua hatua gani za ziada na za dharura ili kuona maeneo haya tunayafanyia kazi, kwa sababu hapa ukipitia zile programu hamna kifungu ambacho kitakwenda ku- *support* eneo hili na leo tuko bajeti hii ya mwaka 2017/2018 na 2019 huko harakati zitaongezeka huwezi kuja kujadili vitu kama hivi. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri aje aniambie kwa programu hizo hizo labda tuta- *reallocate* kwamba tunaweza tukafanya hivi na hivi, basi tu mimi nataka maelezo lakini tuone hii taarifa ya wenzetu tumeizingatia.

Leo unakwenda Wilaya ya Kaskazini B kuna ofisi wakiingia watu wanne au watano haingii, hao maafisa peke yake wako 12, wanakaa kwa *shift*, sijui utaratibu gani wa kuzungumzia mzuri. Lakini niiombe tu serikali ijuwe Tume ya Uchaguzi hii inakabiliwa na changamoto kubwa katika maeneo haya yenyewe ripoti imesema.

Lakini katika eneo hilo hilo Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii pia ya Disemba 2016, imetoa changamoto nyingi katika uchaguzi mkuu ulioharibika, tukaja katika uchaguzi wa marejeo. Kuna mjumbe mwenzangu kasema kwamba hatuko rafiki sana na matumizi mazuri ya demokrasia nchini kwa Tume ya Uchaguzi tuliyonayo. Lazima kwa umoja wetu tulifikirie hili vya kutosha, ili tuone tunapoingia katika uchaguzi tusisababishe malumbano ya kuharibu uchaguzi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, leo ukisoma ripoti unakuta makamishna wa tume wamegombana humu, na sababu ya kugombana kila mtu ana-*declare interest*. Leo katiba kifungu hicho cha 119(1)(c) kinaruhusu kupatikana kwa wajumbe ambao watatokana na kiongozi mkuu wa upinzani, hatuwezi kuwa na katiba hii. Leo viongozi wa upinzani utampata hapa atatoa watu wake, Mhe. Said Soud ana chama chake na yeye atakuja siku moja asimame atake atowe watu wake, kuna vyama vyengine karibu 30. Kwa hivyo, tuone imefika wakati sasa tusitetee vyama fulani katika kuunda Tume ya Uchaguzi, uchaguzi huu una vyama zaidi ya 30 vitakuja huko vinagombania kwa pamoja. Tume iwe huru na uhuru wake maana yake iwe hakuna watu wa kwenda kutetea au kwenda ku-*declare* zile *interest* zao. Leo watu wanataka kufanya maamuzi ya nchi, hawafanyi kundi moja limegoma na unalijua linatoka wapi, hatuwezi kuwa na katiba itakayokuwa inaruhusu matumizi mabaya ya demokrasia nchini, matumizi mazuri ya demokrasia nchini ni lazima tuwe na tume huru ambayo itazingatia ule ubora na matumizi bora ya demokrasia.

Kwa hivyo, kuwaruhusu watu wakatoka na aina ya kundi fulani, hatuwezi kuwa na tume huru ambayo itakuwa na matumizi bora ya demokrasia. Kwa hivyo, mimi nasema tu nashauri hili ili kabla rafiki yangu Mhe. Said Soud na yeye hajaja kudai wake na wengine wakaja kudai wao, basi tuone. Maana hawa wote wanagombea kwa kupitia vyama vyao, kwa hivyo tusiruhusu aina tu. Kwa hivyo, kwenye eneo hili naamini serikali imenisikia na hili halileteki hoja binafsi tunasubiri mswada ambao utaleta tume bora ambayo, maana kama unaletwa mimi ningeleta na ninajua ningepata *support* ya watu wawili. Lakini nasema busara itendeke katika kutengeneza demokrasia nchini, tusilete katiba ambayo inabeba tu aina fulani ya watu tumpe uhuru Rais afanye maamuzi ya kuteuwa tume bila ya kumshurutiza apitie wapi, hatuwezi kuwa na tume bora.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye Tume ya Kuratibu Dawa za Kulevya. Kwenye eneo hili kuna programu mbili nimezipitia kwa umakini na niwapongeze sana kwa juhudi zao ambazo wamezichukua. Lakini pia hapa naomba niishauri serikali pamoja na jitihada hizo ambazo wanazichukua, lakini bado kubaki na tume tu itakayoendelea kuratibu hizi changamoto tutaendelea kuwa nazo tena kwa kiasi kikubwa na hatuwezi kutatua suala hili kubwa la madawa ya kulevya. Naomba sasa niishauri serikali katika maeneo muhimu kama ifuatavyo.

Tume ile ibaki lakini tuanzishe kamisheni ambayo itakuwa inaweza kusimamia na kuratibu masuala ya dawa za kulevya, ambapo kamisheni hii itakuwa na *staff* wanaojitegemea ndani ya kamisheni ile, tukifanya hivi maana yake unaweza ukampata Mkurugenzi wa Upelelezi mule ndani, lakini unaweza ukampata Mkurugenzi wa Operesheni, unaweza ukampata Mkurugenzi wa *Intelligentsia*, ikisha unawapelekea wafanyakazi kupitia taasisi tofauti. Maana sasa hivi Tume hii ya Kuratibu Madawa ya Kulevya wafanyakazi wake wanatoka Jeshi la Polisi, hatuwezi kuwa na tume ya aina hii ikisha baadae Polisi wabakie kama Polisi wakakamate washtaki kwa upande wao, lakini kuanzishwe kamisheni ambayo itachukua wafanyakazi wengi ambao watatoka katika vitengo tofauti. Kamisheni ile iwe na uwezo wa kuratibu na kusimamia shughuli zake yenyewe. Mhe. Mwenyekiti, leo ukiwacha yule mkurugenzi ambaye yuko sasa katika tume mwenyekiti wa ile tume Makamu wa Pili, mwanzo alikuwa Makamu wa Kwanza, sasa hivi kwa sababu hayupo kwa dharura ambazo kazipata tarehe 20 Machi, kwa hivyo eneo hili limesogezwa kunako Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, leo wajumbe wale wa tume wanatoka katika maeneo tofauti, kukutana kwao kunachukua muda na eneo hili muhimu. Sasa tuanzishe kamisheni itakayokuwa inafanyakazi, maana yake mnasema saa 24 wao wako

na kazi ile tu, sio watu wakutane kwa muda baadae atabakia mkurugenzi mmoja na maafisa sita ndio wanaipeleka ile taasisi, hatuwezi kufika kadhia hii ni kubwa. Kwa hivyo, tuanzishe kamisheni ambayo itakuwa inafanyakazi na utawala wake unabaki ndani ya kamisheni ile. Mimi naishauri sana serikali, tume ile inabaki na viongozi wale wanabaki kama walivyo, lakini ndani yake kuwe kuna kamisheni ambayo itatusaidia na hii kamisheni itatoa wafanyakazi kama mapolisi ambao wametangulia kuwepo mnawahamisha hasa wanakwenda kwenye kamisheni. Lakini kama kuna wengine wa Intelligentsia mnawahamisha wanakwenda kwenye kamisheni, na maafisa wengine ile kamisheni inafanyakazi mtu wa operesheni analeta taarifa kwenye tume hii, lakini mtu wa upelelezi anatoa taarifa. Lakini na hawa wanakuwa na mamlaka wenyewe ya kukamata, kupeleleza na kupeleka mahakamani, tusisubiri huku tena polisi. Kwa hivyo, tutakwenda vizuri, na mimi lazima niipongeze serikali imetunga sheria nzuri kweli katika masuala haya ya madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, nimeipitia kidogo, ukitoka pale ukienda kumkamata mtu nyumbani kwa Mhe. Rashid kama taarifa hakutoa unaweza kumshtaki na yeye mwenyewe, ipo hiyo. Leo angebaki mtu ndani ya majumba yetu wasingetoa taarifa, wangetoa taarifa tu. Lakini usimamizi wake hauwezi kufikiwa kwa sababu nasema kuna tume ina wazee wengi huku juu ambao wao kila mmoja na shughuli zake, lakini tukiweka kati kila mmoja tukampa jukumu lake basi tutafika vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende na mimi niipitie tu kwa ufupi kabisa katika eneo la mapato. Mjumbe mwenzangu alilichangia, lakini katika kitabu kikubwa

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe una dakika tano.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Tatu.

Mhe. Mwenyekiti: Tano.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Aah! zinanitosha Mhe. Mwenyekiti, *hardly* nitatumia dakika moja. Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili la mapato ni kweli, kitabu kikubwa hiki kimetoa muhutasari wa mapato wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuna milioni 32,521,000. Lakini Tume ya Uchaguzi imewekewa shilingi 455,000/-, kwa hivyo jumla ndio iliyokuja kuripotiwa kwenye kitabu hichi cha Muhtasari wa hutuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Lakini ukirudi nyuma kwenye kitabu hichi utakuta mwaka uliopita kuna idara zilikuwa zinakusanya haya mapato na katika kuzinukuu zipo mbili, kuna Wakala wa

Serikali Upigaji Chapa Makadirio na Makusanyo yamewekwa, kuna Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya kitaifa fedha zake pia zimewekwa.

Lakini kitabu kikubwa hichi hakiwasomi hawa na siamini kama na wao wamefutika ndani ya eneo hilo wapo tupate maelezo yatakayotuwezesha basi kunako eneo hili la mapato tujiridhishe na kama kafutwa kafutwa nani kwa misingi ipi. Sasa Mhe. Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais mimi zaidi nilikuwa nataka ufafanuzi katika eneo hilo.

Lakini naomba nimalizie mwisho tu kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja mimi sina budi. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, naomba sana ushauri wangu Serikali wauchukue ili tufike kujenga nchi yetu kwa salama na amani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Miraji sasa anafuatia Mhe. Mwanaasha Khamis na huyu ndio atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho na baadae kwa jioni wataendelea kwa sehemu ya mawaziri Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri Naibu Waziri, Mhe. Waziri Said Soud MBM, Mhe. Mwanasheria Mkuu, Mhe. Rashid Ali Juma na Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohammed. Nimuombe Mhe. Mussa Ali Mussa ambae alikuwemo kwenye orodha nilitegemea muda utakuwepo na yeye aendelee kwa hivyo na yeye achangie kwa maandishi Mhe. Mussa Ali Mussa katika orodha niliyokuwa nayo.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Kwanza kabisa na mimi niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia niungane na wenzangu kuwapa pole wale waathirika wote waliokutwa na majanga hayo yaliyotokea yaliyotokana na mvua. Lakini pia niipe pole au niipongeze Wizara hii kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya na katika malengo yake makubwa ni kuona kuwa yale wanayoyasimamia yanafanya kazi kwa ufanisi. Lakini katika malengo hayo katika hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais malengo yake makubwa katika mwaka 2017 nimeona kuwa kupitisha sera ya mafuta au kupitisha sheria ya sera ya mafuta na gesi, pia wameandaa sera ya mafuta na gesi kwa kukamilika katika hatua mbali mbali niipongeze sana Wizara hii.

Lakini katika suala zima la mafuta na gesi nimeona kuwa katika malengo yake makuu kuendelea na maandalizi katika sekta hii maandalizi hayo katika sekta

hii Serikali imeanza kuwajengea uwezo kupitia msaada wa OFB Shirika hilo ambalo la Norway, Shirika hili limesaidia kutoa mafunzo kwa wataalam wetu mbali mbali, nilitaka kujua tu au kupata ufafanuzi ni wataalam wa aina gani na katika nyanja zipi katika eneo hili. Pia nilitaka nijue katika hao wataalam wanaojengewa uwezo katika msaada huu wanawake wako wangapi.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika *program* ya uratibu wa shughuli za Serikali wachangiaji wengi wamechangia katika suala hili lakini na mimi sina budi nione nichangie katika *program* hii kwenye malipo, kwenye ukurasa wa kumi na tisa kifungu cha (xiv). Kuna malipo kwa kaya masikini yamefanyika kiasi cha shilingi 5,552,368,000/= zimelipwa kwa wastani wa kaya 32. Pia juma ya shilingi milioni 397, 412,000,400/= zimelipwa kwa kaya 11 682 niwapongeze sana lakini kwa vile lengo ni kupunguza umasikini katika kaya masikini nilitaka kujua kabla ya kupitisha hivi vifungu katika buku kubwa hapa katika shughuli hii ya uratibu wa shughuli za SMZ kwa mfuko huu wa maendeleo ya jamii ni pamoja na kupunguza umasikini katika kaya masikini zimetengwa katibu bilioni nane na kitu.

Sasa nilitaka nijue kuhusiana na suala zima bajeti hii tunayopitisha nakumbuka tulipata mafunzo ni mpango wa PBB yaani ni bajeti inayoingatia matoke, kwa hivyo kama ni bajeti inayozingatia matokeo nataka kujua katika hizi kaya masikini ni kaya ngapi ambazo zimeondokana na ule umasikini, isijekuwa tunapitisha hivi vifungu lakini ile *impact* haijaonekana lengo letu kuondoa umasikini. Sasa ni kaya ngapi ambazo Wizara hii imezipitia tayari zimeshatokana na ule umasikini na hususan ukizingatia kaya nyingi ambazo ni masikini basi zinaongozwa na wanawake. Kwa hivyo tunataka tujue kaya ngapi zimeondokana na hiyo kadhia ya umasikini kupitia mradi huu na pia ni kaya ngapi za wanawake zimeweza kujikomboa na sasa hivi zimeondokana na ule umasikini katika changamoto mbali mbali ambazo zimekabili.

Lakini nirudi tena najua huu umasikini sisemi tu kwa jimbo la Chukwani nahisi zipo kaya nyingi ambazo katika kaya nyingi katika majimbo mengine, kuna kaya masikini Mhe. Mwenyekiti ni za watu wenye ulemavu, nimeratibu hilo katika jimbo langu la Chukwani unakuta watoto wenye ulemavu wazee wao ni masikini kupita kiasi uwezo wao mdogo na wanaongozwa kaya hizo na wanawake, kwa hivyo pia nilitaka nijue ni kaya ngapi masikini za watu wenye ulemavu wamenufaika na mradi huo.

Mhe. Mwenyekiti, nije tena katika *program* hiyo hiyo ya uratibu wa Shughuli za Serikali Namba (xix) Ofisi imeratibu vikundi 14 vya watu wenye ulemavu, katika azma ya kuwajenga uwezo nilitaka kujua Mhe. Mwenyekiti, azma ni

nzuri kwa vikundi hivyo 14 lakini ni vikundi vya maeneo gani na sehemu gani ukizingatia katika maeneo yote ya Zanzibar tayari watu wenye ulemavu na vikundi vyao vipo. Kwa hivyo nilitaka watubainishie ni vikundi gani ambavyo vimepata nafasi hiyo ya kujengewa uwezo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha (xx), jumuiya tano za watu wenye ulemavu zimepatiwa ruzuku ili ziweze kusaidia katika shughuli zao za kiutendaji. Kwanza pia niipongeze Wizara hii kwa kuona ipo haja ya watu wenye ulemavu au vikundi hivi au jumuiya hizi za watu wenye ulemavu kuzipatia hizo ruzuku. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Waziri akija atupe majibu kuhusiana na kuwa vikundi vingapi au jumuiya ni tano lakini ni maeneo gani ambayo jumuiya hizo zimepatiwa ruzuku hiyo.

Lakini vile vile baada ya kupatiwa ruzuku ile narudi tena pale pale katika huu mpango wa PBB wa kuzingatia matokeo tuone ni matokeo gani yamepatikana katika ruzuku ile imewafaidisha vipi hizi jumuiya tano ambazo zimepatiwa ruzuku hizo.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 28 *program* ya udhibiti wa dawa za kulevya. Mimi niipongeze Serikali au niipongeze Wizara hii kuona ipo haja ya kuwepo hili suala zima la udhibiti wa dawa za kulevya. Lakini nilikuwa naomba sana niishauri Serikali tayari wameanzisha *sober house* ambazo nyumba hizo za kurekebisha tabia, lakini bado naendelea pale pale nilikuwa naiomba sana Serikali hebu iangalie kwa umakini wake suala zima la hizi *sober house* zina faida gani. Kwa sababu nasema hivyo watu wengi au vijana wengi ndio wanaoathirika na haya madawa ya kulevya na isitoshe vijana hao hao wanapelekwa kule *sober house* wanawekwa pale na ruzuku zinatolewa na majumba hayo yapo mengi, lakini Je, wale vijana wanaokaa katika ile *sober house* wakitoka nje wanafanya nini au wana kazi gani.

Kwa hivyo nilikuwa naomba sana sana Wizara hii wapokee na ushauri huu ninaoutoa mimi hapa Mhe. Mwanaasha Muwakilishi wa Jimbo la Chukwani naomba sana Wizara ichukue ushauri huu ninaowapa kuwa katika hizi ruzuku wanazotoa wahakikishe ndani ya zile *sober house* waanzishe zile elimu amali yaani mafunzo kwa vitendo, wakitoka pale Mhe. Mwenyekiti wajue sisi tumepata mafunzo kupitia *sober house.* Kwa hivyo wakifika kule mitaani hata kwa kuwapa zile ruzuku wenyewe wakafungue mitaji yao na kujiendeleza na mambo yale yale. La si hivyo tutaongeza *sober* nyingi itakuwa kama tunawaonyesha wale kuwa nyie vuteni madawa ya kulevya, vuteni unga lakini *sober* zipo zitakulindeni, mnapewa dawa, mnapewa huruma pale mkitoka mrejee tena.

Lakini nilikuwa naomba sana Wizara inayohusiana na hili hebu waone wapange mpango wa makusudi mazima kuona vile vituo vya *sober house* vinawajengea uwezo na vifaa vya kuwafanyia utendaji ili wakitoka waachane na yale madawa ya kulevya lakini wawe na kitu ambacho kinaweza kuwaendelezea maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa hayo machache mengi yamechangiwa niliona nisimame nichangie na hili kuhusiana na suala zima la madawa ya kulevya, lakini pia nahisi ningekuwa sijawatendea haki watu wa Jimbo la Chukwani. Kwa sababu umasikini upo, kaya masikini zipo, watu wa madawa ya kulevya wapo, watu wenye ulemavu wapo na hii hotuba imetugusa sote. Kwa hivyo nipongeze sana lakini pia naunga mkono hotuba hii kwa asilimia tisini na tisa moja naiacha nije nipatiwe majibu kuhusiana na yale masuala ambayo nimeyagusia. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe, nashukuru kwa utulivu wenu na michango yenu yote ambayo mumeitoa na sasa nachukua fursa hii kuahirisha kikao hichi hadi wakati wa saa kumi na moja jioni. Ahsanteni.

(Saa 6.58 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhanah Wataalla kwa kutujaalia kufika tena jioni hii hapa pamoja na Inshaallah Mwenyezi Mungu atujaalie tuende salama.

Baada ya hapo Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa jitihada zake za kuboresha maisha ya Wazanzibari na kutekeleza vyema ahadi zake zile ambazo anazitoa kwa zile ambazo alizitoa wakati wa kujinadi na zile ambazo anazitoa katika harakati zake za kuitumikia nchi hii.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa ahadi yake ya kuwapatia wananchi wa Zanzibar asilimia 100 ya ongezeko la mshahara wa kima cha chini. Hili jambo halijapata kutokea katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Kila ambaye alikuwa akichukua nafasi hii basi alikuwa

anaongeza tumbaku, lugha kubwa ni kuongeza tumbaku. Kwa hivyo wafanyakazi wa nchi hii kila Mei walikuwa wanakwenda kwenye mikutano kwa ajili ya kusubiri ya kuongezewa tumbaku. Sasa basi yeye hakuongeza tumbaku, yeye ameongeza kamba kwa vile alikubali kwa namna moja au nyengine kuhakikisha Wazanzibari kwa pamoja tunakula keki ya Taifa, yaani uchumi wa Zanzibar kwa pamoja na hatimaye akaongeza mshahara kama huu. Hiyo ni hongera sana kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Inshaallah Mwenyezi Mungu akijaalia uchumi ukiongezeka naamini ataongeza zaidi na zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa hotuba yake ambayo imeitoa hapa jana, hotuba ambayo kwa kweli mimi nikasema *GPS*, yaani ni dira ya kuonesha maendeleo ya Wazanzibari yaliyopita na yanayokuja. Nadhani watu wengi mnaelewa *GPS* ni chombo ambacho kinaonesha moja kwa moja pale ambapo tunataka kwenda na ushahidi wa *GPS* hii Mhe. Spika, ni Magazeti haya yanatengenezwa Zanzibar. Sasa ahadi aliyoitoa Mhe. Waziri wa Nchi kwamba mashine za ku-*print* magazeti au vitendea kazi vya Zanzibar vitaanza mara moja, ni kweli kabisa magazeti haya yanatengezwa Zanzibar sasa. Hili la tarehe 10 na hili na tarehe 11 leo yanatengenezwa Zanzibar ni kwa sababu gani? Ni kwa sababu ya ahadi iliyotolewa ya kutekeleza masuala haya chini ya uongozi wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Makamu wa Rais wa Zanzibar.(*Makofi*).

Mhe. Spika, dalili hii inatuonesha kwamba sasa tuko tayari kutoa nafasi hii kwa wale wenzetu wa Tanzania Bara kuja Zanzibar kuchapisha magazeti yao na viwanda hivi ni viwanda ambavyo katika Afrika Mashariki hakuna, zaidi tunavyo sisi Zanzibar, na wale wanaosema labda kesho, kesho kutwa kinaweza kuchukuliwa labda kikapelekwa Bara si rahisi mashine hizi, zina uzito wa tani 36. Sasa haziwezi kwenda kubebeka kwa gari ya *carry*, huwezi kupeleka *carry* ukasema unabeba mashine hizi, si jambo ambalo haliwezekani kwa hizi ni mashine za Wazanzibari na tayari zinafanya kazi kwa mujibu wa maagizo ya Serikali.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kusema kwamba dira ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ambayo imeweza kutuwelekeza katika maendeleo ya harakati tunazoelekea, inaonesha wazi kwamba uongozi wake ni uongozi wa kupigiwa mfano. Mimi naweza nikasema ni jembe na kwani nasema hivyo kwa sababu Ofisi yake imeweza kusikiliza matatizo ya Wazanzibari ya aina mbali mbali zaidi ya hamsini na tatu, ndani yake ishirini na nane tayari yashapatiwa ufumbuzi. Ofisi yake imeweza kukaa mara ishirini na nane kusikiliza kero za

Wazanzibari zikiwemo za ardhi, kero za majumba, kero za aina mbali mbali katika mazingira ya kuweza kuwafanya Wazanzibari waondokane na dhana ile ya kwamba hawashughulikiwi.

Mhe. Spika, Ofisi imeweza kuratibu vikao kumi vya Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar kwa maslahi ya Wazanzibari. Sasa akitokea mtu akisema kwamba labda Ofisi ile imekaa mambo ya Muungano hayashughulikiwi si kweli, yanashughulikiwa, yanafuatiliwa na kero zitaondoka. Nimepata kusikia baadhi ya watu wakisema hapa kuhusu habari ya mafuta na gesi asilia. Napenda niwaeleze Wazanzibari wote kuchukua nafasi hii kuwaambia Wawakilishi wote kwamba sisi kama Wazanzibari, sisi kama Watanzania ni kauli za watu wawili tu ndizo ambazo zinapaswa kusikilizwa. Tumsikilize Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kama Rais wa Zanzibar na tumsikilize Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kama Rais wa Jamhuri ya Muungano kuhusiana na suala la mafuta. Hawa wengine wote naweza nikasema wapiga debe tu. mimi nikisema jengine kuhusiana na hoja hii ni mpiga debe. Lakini mwenye kauli ya mwisho katika nchi hii ni Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein na huu ndio mfano nataka niwaambie ndugu Wawakilishi. Mfano huu uko kwa Rais Trump pale Marekani, alisema mataifa sita hayana uwezo wa kuingia pale Marekani. Dunia nzima ilipiga kelele lakini hakuna mtu anayeingia pale. Kwa sababu ni kauli ya Rais. *(Makofi)*

Sasa sisi tumemshuhudia Rais Shein, sote tumekwenda pale akitia saini masuala ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na Rais wa Jamhuri ya Muungano amemuwakilisha, Waziri anayehusiana na hoja hiyo. Watanzania kuja pale na hoja hii imetiwa saini watu wote wameiona. Halafu leo mtu anatokea anakwambia ooh! maana yake mafuta mali ya Tanzania, bado yamo katika Katiba. Hawa ni wapiga debe na hawatutakii mema. Watu wanaotutakia mema ni watu wawili na hawajasema lolote zaidi isipokuwa wanaendeleza harakati zao za kuijenga Tanzania. Kwanza ni Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein na pili Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, hakuna kelele tena. Suala la mafuta ni mali ya Wazanzibari. Hoja imepita watu wanaendelea na kazi ndege zimeruka, watu wamepiga picha mafuta yako wapi, watu wameyaona. Sasa leo hii anakuja mtu anakwambia mafuta bado yapo katika Katiba. Katiba sio Msahafu, hakuna Katiba iliyokuwa Msahafu. Katiba ni makubaliano kati ya watawala na wanaotawaliwa na maridhiano yaliyopatikana kati ya Rais Kikwete na Dkt. Shein kuhusu mafuta ndio sisi tunayoyafuata. *(Makofi)*

Mhe. Spika, na hii ndio Ilani ya Chama cha Mapinduzi kuwaondolea kero Watanzania. Wazanzibari na Watanganyika anatekeleza sera ya Chama cha Mapinduzi Dkt. Shein katika mazingira haya ya mafuta. Sasa leo mimi nataka

nichukue nafasi hii Mhe. Spika, kuwaambia kwamba jamani eeh! Wazanzibari tuwache, tungojee mafuta tuchimbe, tujiaandae na utajiri uliokuwa Mwenyezi Mungu ametupangia miaka mingi, tujiandae na kumpongeza sana Rais wetu wa Zanzibar kwa maamuzi magumu kama haya ambayo ameyapitisha, tusiwe tayari kurudi nyuma, tuwe tayari kwenda na ngoma ya mdundiko mbele kwa mbele hakuna habari ya kurudi nyuma. *(Makofi)*

Mhe. Spika, narudia kusema kwamba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, imejiaanda katika mazingira mbali mbali. Sasa mimi jana nilipata mshangao mkubwa kuambiwa kwamba yeye anajenga zaidi katika jimbo lake la Mahonda. Mimi nilipata mshangao sana kwa sababu Ofisi yake ni sawa na Ofisi ya Waziri yeyote, na yeye anapewa *political voucher,* akipewa *political voucher* akijenga Mahonda katika vijiji mbali mbali, sehemu mbali mbali ni pesa ile ambayo amepewa yeye kwa matumizi ya wananchi na mimi napewa hivyo hivyo, na kila Waziri anapewa, kila Waziri anapewa *political voucher* kwa ajili ya kutoa huduma za wananchi. Sasa yeye akitoa huduma katika jimbo lake, sasa leo tunapiga kelele kwamba yeye anajenga Mahonda tu.

Haya mambo yako katika kitabu hiki yanahusu Mahonda. Maana hichi kitabu kinaeleza kwamba ametoa msaada Dar es Salaam, ametoa msaada Dodoma, ametoa msaada mpaka Chimori India. Chimori India watu wameweza kuwezesha kutoa milioni 45 zimetoka kwa ajili ya kuwasaidia Wazanzibari na Watanzania wote. Mahonda hiyo. Mimi nawauliza Chimori ni Mahonda. Maana lazima tunapozungumza vitabu hivi tuwe tayari kukisoma na kukielewa kwa maslahi ya taifa tusipotoshane. Tumepotoshana asubuhi jana magazeti haya hapa. Magazeti haya hapa yanatengenezwa Zanzibar, tumepotoshana kwamba yanatengenezwa Mahonda, kwani sisi Mawaziri sote tunapewa pesa kila mtu anatengeneza jimbo lake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nyinyi Wawakilishi mnaomba ruzuku ya jimbo. Mnapewa ruzuku ya jimbo na Mawaziri wanapewa *political voucher* kwa ajili ya kutengeneza majimbo yao. Sasa leo akitengeneza Mahonda iwe nongwa, kila mtu anasema huyu bado, huyu vile, hapana! Sisi Wawakilishi tuwe tayari kuhakikisha kwamba Serikali inakwenda mbele. Serikali hii inatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kwa maana hiyo Mhe. Spika...

Mhe Spika: Mhe. Waziri elekea huku ukizungumza unitizame mimi. *(Makofi)*

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Spika, nafurahi kwa kuniambia nikuelekee wewe sikatai lakini nataka niseme kwamba mambo ambayo yamezungumzwa si mambo ya kuyatilia maanani. Kwa sababu

ukweli ni kwamba Mhe. Spika, katika kitabu hichi nimegundua kwamba kuna mambo ambayo lazima Wazanzibari wayaelewe na wayaelewe kwa sababu gani? Kwa sababu ya juhudi na jitihada inayochukuliwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ukweli ni kwamba tumekuwa tumesikia watu wengi wakizungumza hapa kuhusiana na hoja ya Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi tulikutana hapa hapa, tukakubaliana kumpa nafasi Mhe. Rais aunde Tume ya Uchaguzi basi na kukutana na kiongozi yeyote wa upinzani hapa hapa. Leo inakuja tena hoja ile ile ooh! wapinzani wasipewe, tumeshapitisha, tukishapitisha maana yake tumeshapitisha. Sasa leo tunarudia tena suala lile lile, watu wakishapitisha wanakwenda wanasahau tumesema hapa hapa, Rais wa Zanzibar awe na mamlaka ya kuteua mwenyewe basi na kukutana na Kiongozi wa Upinzani hapa hapa ndani. Lakini hapa hapa ndani inakuja hoja nyengine kwamba lazima kwa nini Rais anakutana, Rais hakutani tena bwana, hakuna kiongozi yeyote wa upinzani atakayekutana naye hapa.

Hicho kitu kimeshafutwa na kimeshaondoka. Kimsingi ni kwamba Rais wa Zanzibar ataunda Tume ya Uchaguzi kwa kupitia vifungu vyake mwenyewe na maamuzi yake mwenyewe bila ya kushurutishwa na Chama chochote cha siasa.

Mhe. Spika: Una dakika mbili Mhe..

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Spika, nakubali kwamba dakika mbili lakini nilitaka niseme mambo muhimu kidogo kuhusiana na mambo ambayo yamejitokeza. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inahusika na mambo ya *TASAF*, Ofisi inahusika na mambo ya UKIMWI, Ofisi inahusika na dawa za kulevya, Ofisi inahusika na mambo mbali mbali ya kujenga nchi hii, na kweli yameelezwa vizuri sana katika kitabu hiki. Kwa hivyo nawaomba Wawakilishi mkakae pamoja au tukae mmoja mmoja, tusome kitabu hichi kwa umakini kabisa na hatimae tuipitishe bajeti hii kwa sababu moja muhimu ndio pahala penye dira ya hoja zetu. Dira ya hoja zetu ziko humu, bila ya kupitisha dira hii tutakuwa tumekwama wenyewe, tumejikwamisha. Sasa kimsingi ni kwamba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ameweza kufanya masuala ya msingi kabisa.

Mhe. Spika, ukenda kwenye *TASAF*, Unguja kaya 126, Pemba kaya 78, pesa ambazo zimetumika au watu ambao wamefaidia karibu 32,700, kaya hizo zimefaidika. Je, kaya hizi ziko Mahonda. Maana kaya 32,000 ziko Mahonda hizi. Hizi kaya zimo Unguja na Pemba. Na mimi nataka nimuhakikishie

Mjumbe mmoja mmoja humu ndani kwamba mimi mwenyewe binafsi niwapeleka watu kutoka Pemba kwa Makamu wa Pili wa Rais kwa ajili ya kuwatatulia matatizo yao. Mimi mwenyewe binafsi. Sasa ni mtu ambaye kwa kweli ni mtendaji mzuri na ninampongeza yeye mwenyewe pamoja na watendaji, Makatibu wake pamoja na wale wote walioshiriki kwa pamoja katika kufanya kitabu hichi.

Mhe. Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Nashukuru sana kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na wewe utupe mchango wako.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kupata nafasi ya kutoa mchango wangu lakini vile vile kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, nimpongeze pia Waziri na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, Wakurungezi wote Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Wakfu na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya uratibu wa shughuli za Kiserikali lakini vile vile kutekeleza majukumu iliyopangiwa Ofisi hii.

Mhe. Spika, mchango wangu utajikita zaidi katika suala hili la athari za mvua zinazoendelea kunyesha katika nchi yetu, na nianze kwa kusema kwamba natoa pole kwa wale wote waliopata athari kwa njia moja au nyengine. Lakini nitoe pole maalum kwa wazazi, ndugu na jamaa wa marehemu mtoto wetu Rahima Ramadhan Moh'd wa Chachani kule Pemba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi, Amin.

Mhe. Spika, naomba niseme kwamba Ofisi hii imefanya kazi kubwa sana. Kwanza ya kuandaa Sheria, Sera, Miongozo mbali mbali lakini hata kuandaa ule mpango wa dharura wa kukabiliana na maafa. Mwaka 2011 Ofisi hii ilitayarisha Sera ya Maafa ambayo kwa taarifa nilizokuwanazo Sera hii hivi karibuni itafanyiwa mapitio. Lakini vile vile mwaka 2015 kuliandaliwa Sheria lakini pia mwaka 2011 kuliandaliwa Muongozo wa Kitaifa wa Kukabiliana na Maafa lakini mwaka huo huo 2011 Mhe. Spika, kuliandaliwa mpango wa kitaifa wa kujiaanda na kukabiliana na maafa. Lakini mpango huu ulienda sambamba na kuandaa mipango ya kukabiliana na maafa ya Kiwilaya. Hadi sasa kuna Wilaya tano ambazo zina mpango huo nazo ni kama hivi:

- Wilaya ya Wete
- Micheweni
- Kaskazini (A)
- Mjini na Magharib

Mhe. Spika, pamoja na yote hayo Afisi hii ilitoa mafunzo maalum kwa watendaji mbali mbali na kwa taasisi mbali mbali, lakini katika ngazi ya Wilaya. Pia kulitolewa mafunzo katika Shehia zote za Unguja na Pemba. Haya ni mafanikio makubwa sana kwa sababu dunia nzima masuala ya maafa yapo. Yapo maafa yale ambayo tunayoyasababisha sisi na yapo maafa ambayo ni kudra ya Mwenyezi Mungu.

Mhe. Spika, maafa yanatokea mahala popote pale, kinachotakiwa kwa nchi kujiandaa. Kwa upande wa maandalizi niseme kwamba serikali yetu kupitia Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais imefanya kazi kubwa sana ya kufanya maandalizi haya. Suala la maafa ni suala ambalo linatugusa sote na sote tuna jukumu. Ukiusoma ule mpango wa kukabiliana wa maafa ya Kitaifa na Wilaya unaelezea majukumu ya taasisi zote za serikali pia na sekta binafsi. Ukenda ndani kuna na majukumu ya wananchi wenyewe na hata mtu mmoja mmoja. Sisi tuna majukumu ya kuhakikisha kwamba tunajiweka tayari katika hatua za kukabiliana na maafa.

Mhe. Spika, sisi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi badala ya kuifikiria Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa pekee ndiyo yenye jukumu la kufuatilia na kupambana au kukabiliana na maafa. Tujue kwamba sote tunalo jukumu hilo. Kupitia mipango ya Kiwilaya, Waheshimiwa Wawakilishi wana majukumu maalum na ningeomba Waheshimiwa Wajumbe tukawa tunafuatilia masuala hayo. Kwanza tuwe tunafahamu hizi sera, sheria na mipango tuliyonayo, pia kusimamia utekelezaji wake katika maeneo yetu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hilo niendelee kusema kwamba serikali kwa sababu hatua nyengine ya kukabiliana na maafa ni kuweka miundombinu sahihi na hasa katika suala hili la mvua. Nikiri kwamba katika kipindi cha siku tano nne hizi nchi yetu tumepata mvua kubwa ambayo haijawahi kutokea kwa miaka mingi kidogo iliyopita.

Mhe. Spika, serikali hii kwa umuhimu huo huo wa kukabiliana na maafa imeweza kuweka miundombinu kwa ujenzi wa mitaro katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba. Nikiyataja maeneo hayo moja ni hapo Uwanja wetu wa Mnazi Mmoja ambapo sote ni mashahidi maji yaliyokuwa yakikaa katika eneo lile, sasa hivi *Alhamdulillah* kutokana na juhudi zilizofanywa kupitia

mradi wa huduma za Miji (*ZUSP*), maji hayakai katika uwanja ule. Yapo marekebisho madogo ambayo yanafanyika hivi sasa kuhakikisha kwamba suala lile limepata ufumbuzi wa kudumu.

Mhe. Spika, Mtopepo na Karakana ambapo mitaro hii imejengwa pia, sasa hivi hakuna maji. Nikienda Karakana kila mwaka, mimi bahati nzuri nilikuwa nikifanya kazi katika Afisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais kwa miaka mitano. Miaka yote mvua kubwa kama hizi tulikuwa tunakwenda kuwaondosha watu katika maji. Mtaro huu umesaidia sana sasa hivi maji hayapo na wale watu waliokuwa kila mwaka wanahama katika maeneo yale sasa wanashukuru. Ukitizama pia kama unakwenda Darajabovu upande wa mkono wa kushoto wanapopita kwa Mzushi, napo maji yameondoka. Maeneo haya ya Jang'ombe kwa Binti Hamrani, Magomeni, Meya nayo juhudi zinakamilika mtaro mkubwa umeshatayarishwa. Kilichobaki sasa ni kuunganisha ule mtaro na mitaro midogo midogo inayomwaga maji katika mtaro mkubwa ili nalo eneo lile liweze kupata ufumbuzi wa kudumu.

Mhe. Spika, kuna hili suala la Mwanakwerekwe. Awamu ya pili *ZUSP* ambapo tayari fedha zake zimeshapatikana ili kutoa mtaro kutoka kwenye lile eneo linalotuama maji Mwanakwerekwe huunganishwa na Sebleni, kupitia hapa Makaburi Msafa, huyashusha chini mpaka kwa Juma Pweza, baadae tuyapeleke kwenye msingi ule wa Saateni kwa Abass Hussein. Kazi hiyo inafanyika. Sasa hivi wapo katika kufanya *design* ya michoro ya kuhakikisha kwamba hakutokuwa na hasara kubwa au gharama kubwa ya kulipa fidia. Kazi hiyo nayo ipo njiani kutekelezwa.

Mhe. Spika, kuna msingi mwengine utakaounganishwa hapa Posta pamoja na Kiwanja chetu cha Kariakoo ambapo kwa mwaka huu pia tunashukuru maji hayakukaa baada ya ule mtaro uliokuwepo pale kufanyiwa matengenezo vizuri. Nataka niseme tu kwamba serikali ipo *serious* na imeshafanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba athari za mvua haziendelei kutuathiri katika nchi.

Mhe. Spika, kwa upande wa Pemba hivyo hivyo eneo la Mkoani kuna misingi imejengwa, zipo *infrastructure* ambazo zinafanyiwa kazi na zimetengenezwa makusudi kuondoa tatizo hilo. Naamini kwamba wananchi wote wanakiri katika maeneo hayo matatizo ya mafuriko ya maji katika maeneo yao baada ya ujenzi ya mitaro hii, matatizo hayo yamepungua kwa kiasi kikubwa sana.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nitoe ufafanuzi katika baadhi ya maeneo mawili au matatu ambayo Waheshimiwa Wajumbe waliyazungumzia. Eneo moja lilizungumzwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi la kuwa na vigezo katika

ukomo wa mapato. Niseme tu kwamba huwa hatuna ukomo katika mapato. *Ceiling* inawekwa katika matumizi siyo katika mapato. Kinachowekwa pale ni makadirio kwa maana *estimate.* Tunachofikiria kwa mwaka huu hichi kinaweza kukusanywa kutokana na chanzo hichi ni makadirio, lakini unaweza kukusanya hata ikipindukia mara tatu. Makisio yale huwa yanawekwa kutokana na *actual figures* za ukusanyaji wa mwaka ama unaomalizika au miaka iliyopo. Ndiyo inayotupa kigezo cha kuweka makadirio yale kwa mwaka unaofuata wa fedha. Hapo hakuna kikomo ambacho tunakiweka.

Mhe. Spika, tunakubaliana na ushauri wake na Wizara yetu ya Fedha na Mipango inakusudia kufanya tathmini ya kina *assessment* ya vyanzo vyetu vyote vya mapato ili kuweza kujua uwezo wa vipato hivyo katika ukusanyaji wa mapato. Hiyo kazi tunakusudia kuifanya ndani ya mwaka wa fedha wa 2017/2018.

Mhe. Spika, suala jengine lilizungumzwa na Mhe. Miraji Khamis Mussa, yeye alisema ukuaji wa uchumi umeongezeka kwa kiwango kidogo sana, akitolea mfano kwamba 2016 uchumi wetu ulikuwa kwa asilimia 6.8 wakati mwaka 2015 ulikuwa kwa wastani wa asilimia 6.5 na yeye akasema kwamba hicho ni kiwango kidogo. Napenda nimtoe wasi wasi kwamba hicho ni kiwango kikubwa sana cha ukuaji. Kwanza inategemea ile *percentage* ndogo anayoiona inategemea ukubwa wa Pato la Taifa lenyewe na kuliongeza hilo sio kazi rahisi. Nchi zilizoendelea ambao wana uchumi mkubwa na pato lao kubwa tarakimu inayoongezeka ya pato inakuwa ni ndogo sana. Kwanza ule uchumi wenyewe unakuwa umeshafikia karibu ya *pick*. Lakini vile vile *size* ya uchumi wenyewe kukua labda kwa nukta moja ni ukuaji mkubwa sana.

Mhe. Spika, asiwe na wasi wasi uchumi wetu umekua vizuri. Tuna matarajio kwamba uchumi wetu tena utaongezeka kukua kwa mwaka 2017/18. Juzi wakati natoa *budget highlight*, nilieleza kwamba uchumi wetu tunatarajia utakuwa katika mwaka wa 2017 kwa asilimia 7.2. Hilo ni ongezeko kubwa sana na wala asiwe na wasi wasi nalo.

Mhe. Spika, vile vile alizungumzia suala la kuwa na *convention center* na hili pia nimtoe wasi wasi. Ndani ya mipango ya serikali, tayari tuna utaratibu huo na katika miradi ambayo tumeipa kipa umbele katika zile *flagship project*, ni mradi wa ujenzi wa *convention center* katika eneo la Fumba. Hata hii leo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alikuwa akizungumzia suala hili hili na baadhi ya wawekezaji kutoka India. Kwa maana ya kwamba hili ni suala linalopewa kipaumbele cha hali ya juu.

Mhe. Spika, sambamba na suala alilozungumzia la *shipping hub* serikali ina mpango wa kujenga Bandari (*Container port*)katika eneo la Mpigaduri na tupo katika hatua kubwa sana za kusaini mikataba na wenzetu wa CHEC kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya biashara. Naamini tutakuwa tunakwenda hatua kwa hatua na haya ni maelekezo yaliyotolewa pia na Mhe. Rais mwenyewe Dkt. Ali Mohamed Shein ya kwamba katika ku-*improve gateways* kwa watalii na mizigo na kukuza fursa za biashara katika nchi yetu, lakini azma yetu ni kuchangia uchumi basi suala la bandari nalo limepewa kipaumbele.

Mhe. Spika, lipo suala ambalo limezungumzwa na Mhe. Hassan ambaye alizungumzia suala la "*VAT return"*. Hapa ningeomba niseme. Kwa sababu hili suala tumeshalizungumza mara nyingi sana lakini naomba nilitolee ufafanuzi zaidi. Kwanza suala la *VAT* siyo suala la Muungano. Tanzania Bara wana Sheria yao ya *VAT* ya mwaka 2014 na Zanzibar tuna Sheria yetu ya mwaka 1998. Sisi tuna haki wakati wowote wa kufanya mabadiliko ya Sheria yetu, kwa sababu siyo suala la Muungano. Ndio maana *VAT* kwa hapa inakusanywa na *ZRB*. Bara na wao wana nafasi hiyo hiyo kwa suala ambalo sio la muungano kufanya marekebisho ya Sheria yao. Mazungumzo ya pande mbili hayafungiki lakini pia hatufungiki kuwafanya wenzetu wasibadilishe Sheria yao kutokana na matakwa ya mazingira yao, sawa na tulivyo sisi hapa.

Mhe. Spika, kilichotokea kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2016, wenzetu walifanya mabadiliko katika Sheria yao. Hapo kabla pande zeto mbili zilikuwa zinafanya kazi kama wakala wa upande mwengine katika ukusanyaji wa *VAT*. Bidhaa zilizokuwa zikitoka Bara zilikuwa zinatozwa *VAT* kule, na sisi huku tunachukua zile risiti zao baadae tunakwenda ku-*claim VAT* yetu kwa upande wa bidhaa zilizotumika Zanzibar kutoka Bara, zikahaulishwa hapa. Kilichofutwa hapa na mabadiliko ya Sheria hii ni kuondosha ule uwakala na kwamba kila upande sasa ukusanye mapato yake. Bidhaa zinazotoka kule sasa hazitozwi *VAT,* zinatakiwa zitozwe *zero rate,* ziwe *zero rate.* Kwa maana ya kwamba *VAT* yote tuikusanye hapa Zanzibar. Kwa bidhaa zinazotoka hapa nazo vile vile hapa hatutakiwi kuzi-*charge,* zinatakiwa ziwe *charged* kule walipe *VAT* yao kwa upande wa Tanzania Bara.

Mhe. Spika, ili uweze kufaidika na hiyo *zero rate* ni kwamba wewe mnunuzi, wewe mfanyabiashara kwanza uwe umesajiliwa kuwa mlipa kodi wa *VAT* na kule unapokwenda kununua wende kununua kwa *local manufacture* ambaye na yeye ni *VAT register.* Ukinunua kutoka kwao na uhakikishe kwamba bidhaa hiyo sasa haitotumika pale Tanzania Bara, inaletwa Zanzibar kwa matumizi ya Zanzibar. Hiyo inakuwa kule *zero rate the same* na sisi tunavyofanya hapa tutakuwa tuna *zero rate* kwa bidhaa zinazotoka hapa, zinazozalishwa hapa,

zinazohaulishwa kupelekwa upande wa Tanzania Bara. Hicho ndicho kilichobadilika.

Mhe. Spika, wafanyabiashara wetu tumekaa nao, tumewashauri, tumewaelimisha juu ya matakwa haya na kuwataka sasa lazima wa *comply* na sheria zilizokuwepo katika katika kipindi hiki. Kwa wale ambao watanunua nje ya utaratibu huo bila ya shaka yoyote *double taxation* itawakumba, maana atakuwa kenda kununua kwa mtu ambaye siye *VAT registered*, sio kwa *manufacturer*, akileta huku sisi hatutokuwa na njia ya kujua kama huyu mtu tayari keshalipa upande wa pili. Kwa hivyo na hapa atatozwa ushuru.

Mhe. Spika, Afrika Mashariki ni "*trading block"*, wafanyabiashara wetu wadogo wadogo tunawashauri pia wakiona kwamba kuna ugumu wa kununua kutoka upande wa Tanzani Bara, basi waende katika nchi nyengine ndani ya Jumuia ya Afrika Mashariki wanaweza kufanya biashara au wajiunge pamoja, waweke *dealer* wanunue kwa kupitia utaratibu wa *dealership.* Nalo hilo linawezekana.

Mhe. Spika, tungewaomba sana wabadilike kufuatana na mazingira ya sasa hivi ya kisheria. Lakini hata tukilizungumza sana hapa Mhe. Spika, bado ni suala la kisheria na suala la *VAT* siyo suala la muungano, wenzetu wameshaweka marekebisho yao. Hata tukizungumza pale wataamua kubadilisha kuja kwenye utaratibu wa zamani. Hiyo itakuwa ni matakwa yao kutokana na mazingira watakayoyaona yanafaa.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha na naomba kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Sasa naomba nimpe nafasi hii Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili na yeye atoe mchango wake. Mwanasheria Mkuu karibu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa fursa angalau kusema machache na hasa baada ya mchango wa Mhe. Said Soud Said, amezungumzia na ameyazungumza yote na ametufilisi. Lakini kwa vile na sisi tunao wajibu wa kuchangia hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais basi na sisi tutachangia kwenye yale maeneo ambayo ameyaacha ili na sisi tuyachangie.

Mhe. Spika, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kama ambavyo wenzangu wote wamefanya tokea jana na leo asubuhi, kwa kutoa mkono wa pole kwa

familia za ndugu zetu wa Arusha ambao wamefikwa na msiba mkubwa wa watoto 32, walimu wawili na dereva mmoja. Leo tumefarijika kuona pia baadhi ya wenzetu wametuwakilisha kwa niaba yetu sisi hapa kwenda huo Arusha. Nadhani hilo ni jambo jema na tunawapa pole na Mwenyezi Mungu atawapa subra.

Pili nitoe mkono wa pole kwa wale wenzetu wa hapa ambao na wao wamefikwa na maafa ya mvua hizi zinazoendelea kunyesha kwa kipindi kikubwa. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango amelizungumza vizuri jambo hili. Sote tunafahamu mvua hizi zinaponyesha zinapokuwa za ziada basi hata miundombinu nayo inazidiwa na maji ambayo inakuwa mengi. Haya tumeyaona nchi nyingi hata huko Marekani wenye miundombinu iliyoendelea, lakini utakuta mvua inaponyesha kwa wingi basi hata ile miundombinu yao wenyewe huzidiwa na maji yanavyokuwa mengi.

Mhe. Spika, kama Waziri wa Fedha na Mipango ameeleza jitihada za serikali zinahitajika, sina haja ya kuyasema hayo mengi. Lakini pia ni vyema kukumbushana kwamba na sisi tunao wajibu wa kuwakumbusha wananchi ambao tunawasimamia na kuwaongoza kuacha kujenga kwenye maeneo ambayo yanapita maji. Hilo ndilo jambo la msingi ambalo inabidi tukumbushane. Waheshimiwa Wajumbe kwenye maeneo yao nadhani hili liwe ndio jambo kubwa la kukumbushana na kuhimizana. Kama sasa tabia hii nadhani tuiwache ili maji ya mvua yapate nafasi yake ya kutoka kupitia mitaro ambayo imewekwa.

Mhe. Spika, pili nichukue fursa hii kumpongeza sana mtoa hoja Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na wasaidizi wake wote kwa kazi yao kubwa na nzuri waliyoifanya. Kwanza kumsaidia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, lakini pili kumsaidia Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Afisi hii ndiyo kiungo cha Wizara zote za Serikali. Kazi zao na juhudi zao tunazithamini sana, wanafanya kazi nzuri. Tunaomba tuwahakikishie kwamba tutaendelea kushirikiana nao katika kutimiza majukumu yetu ambayo tumekabidhiwa na Mhe. Rais.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii kuwapongeza wale wote ambao wamechangia na mimi nitakwenda kwenye maeneo machache. Waheshimiwa Wajumbe wengi wamechangia kwenye maeneo ya Muungano na hasa eneo la mafuta. Lakini la pili ni eneo la muundo wa Tume ya Uchaguzi. Waheshimiwa wameyazungumza na ni vyema tutoe ufafanuzi.

Mhe. Spika, kwanza ni vyema sote tukubaliane na tutambue kwamba kwenye muungano huu sote tuna haki sawa, hatujaungana kwa sababu ya udogo wetu na wala wenzetu Watanzania Bara hawakuungana na sisi kwa sababu ya ukubwa wao. Sote tumeungana kwa hiari hatujaungana kwa nguvu. Sasa sote tuna haki sawa kwenye muungano yasije mawazo hapa yakaonekana sisi wenzetu labda wanatukandamiza au wenzetu wakaona sisi tunawakandamiza wao, sisi sote tuna haki sawa na yale ambayo tumekubaliana kwenye orodha ya muungano tumekubaliana pia kwa hiari. Na pale mmoja anaponyanyuka akasema sasa baada ya miaka hamsini hii nadhani kwenye jambo hili basi tuachiane kila upande ulisimamie wenyewe nalo hilo pia linafanyika kwa hiari na hakuna upande utakaoweza kumkatalia upande mwenzake kwa sababu hayo ni mambo tumekubaliana kwa hiari na yanaongozwa kisheria sasa.

Sasa kwenye hili jambo la mafuta Mhe. Spika. Hili kwanza sote tunalijua na mimi sina haja ya kuzungumzia hiyo historia lakini nisema wala Katiba si kikwazo, ukisoma kuanzia ibara ya 1 mpaka ibara yote nadhani ya 157, ukiacha ile orodha ya muungano huoni pahala popote ambapo Katiba imeelezea utaratibu wa kusimamia mambo ya mafuta na gesi asilia imeyataja tu kwenye orodha ya muungano. Maana nini, maana yake Katiba imetoa fursa kwa Bunge sasa kutunga sheria ya kuweza kusimamia mambo hayo huo ndio utaratibu ambao unatumika. Na sisi sote tunafahamu sheria ya awali iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1980, ilikuwa sheria ambayo ndiyo kikwazo na ndiyo ilikuwa sababu ikatupelekea hata na sisi tuamue kama sasa jambo hili litoke kwenye orodha ya mambo ya muungano.

Sheria ile Mhe. Spika, ilitungwa bila ya kutafakari kwamba kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuna sehemu mbili na unapozungumza mambo ya mafuta kuna mambo mengi ambayo hayagusi muungano:-

1. Ni usajili wenyewe wa makampuni ya mafuta, makampuni yanapokuja kutaka kuwekeza inabidi yasajiliwe na yanasajiliwa kupitia sheria za makampuni na sheria za makampuni si jambo la muungano, kila upande una jambo lake.

2. Sheria pia haikuzingatia kama unapotaka kuchimba mafuta lazima ufanye *Environmental Impact Assessment* na hiyo siyo moja ya jambo la muungano. Lakini kubwa zaidi ni lazima uwekeze kwenye ardhi na ardhi si jambo la muungano kila upande unasimamia ardhi yake. Sasa ile Sheria ya mwaka 1980 ilitungwa bila ya kuzingatia hayo yote ambayo nimeyaeleza. Sasa huwezi ukawa na sheria ambayo inakwaza upande wa pili wa muungano katika utekelezaji wake. Ndio tukaamua kama Sheria hii

haitufai tuanze kwanza kushughulikia na hii Sheria kwanza na hili ndio ambalo tumelifanya na namshukuru sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, mwaka 2015 kwa jitihada kubwa iliweza sheria ile kufutwa. *(Makofi)*

Mapendekezo yaliyokuwepo ilikuwa kwanza tuifanyie marekebisho ile sheria lakini baadae viongozi wakakubaliana kama ile Sheria ni vyema ifutwe kabisa na ikafutwa ikatungwa Sheria Namba 21 ya mwaka 2015. Niwaombe sana Waheshima Wajumbe hebu wazisome hizi sheria, wasome ile ya mwaka 1980 halafu wasome na hii ya mwaka 2015, halafu waone tofauti ya sheria mbili wazisikilize tu maneno yanayosemwa mitaani, vijiweni, wasome halafu waje kujenga hoja. Natambua *sentiment* ambazo zipo kwa Waheshimiwa Wajumbe kama pamoja na kwamba haya yote yamefanyika lakini Katiba ya Jamhuri ya Muungano inalitaja jambo hili ni miongoni mambo ya muungano.

Sote tunakubaliana Mhe. Spika, kama lazima tuanze pahali lazima tuanze pahali na pahali penyewe pa kuanza ilikuwa ni hapa pa kushughulikia hiyo sheria na sote tunatambua kama Zanzibar ilishaamua kama jambo hili litoke kwenye orodha ya mambo ya muungano. Uamuzi ulishatoka yaliobaki ni utekelezaji ingekuwa sisi tuna uwezo wa kulitekeleza hili peke yetu basi nadhani sasa hivi tusingekuwa tumekaa hapa na kuanza kulijadili jambo hili.

Mhe. Spika, lakini kwa sababu ili tulitekeleze inabidi na wenzetu pia tuwashirikishe. Sasa hicho ndio kinachofanyika lakini suala la kusema jambo hili libaki kwenye orodha wa mambo ya muungano, nadhani hili limeshamalizika zamani tena hata kabla Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein hajawa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kilichobaki ni utekelezaji. Sasa tumeanza na sheria, inayofuata sasa ni uendelezaji wa kuhakikisha jambo hili linaondoka kabisa kwenye orodha wa mambo ya muungano. Sasa ni mambo mawili ama iondoke kupitia Katiba hii iliyokuwepo au liondoke kupitia Katiba ambayo pendekezi ambayo bado inasubiri kupigiwa kura ya maoni.

Lakini hili kwa upande wa Zanzibar halina mjadala naomba hilo niwahakikishe Waheshimiwa Wajumbe hili kwa upande wa Zanzibar halina mjadala. Natambua hofu kama pamoja na sheria hiyo Namba 21 ya mwaka 2005 kuwepo, lakini bado Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limepewa uwezo wa kutunga sheria au kuibadilisha sheria iliyokuwepo, wanaweza kesho wakaamka wakaenda kuibadilisha ile Sheria iliyokuwepo. Sasa utaratibu bora na utaratibu ambao sote tunakubaliana nao ni vyema bila ya kuwa na *suspicion.*

Huyu anamka atafanya hivi au huyu kesho atafanya hivi, ni vyema jambo hili litoke kabisa kwenye orodha ya mambo ya muungano.

Mhe. Spika, sasa hilo tunaendelea kulifanyia kazi lakini wakati bado tunaendelea kulifanyia kazi ni vyema Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi wajuwe kama Katiba haikukataza kukasimu kisheria madaraka kwa pande mbili za muungano kushughulikia jambo ambalo ni la muungano. Katiba haikukataza. Utaratibu huo lazima uwepo kisheria. Sasa niwaombe sana wakaisome hii Sheria Namba 21 ya mwaka 2015 baadae sasa watu waje kujenga hoja zao. Bila ya kuwa na hofu hivi ambazo nimezieleza, natambua hizo hofu zipo na zitaendelea kuwepo kama jambo hili halijaondoka kwenye orodha ya muungano. *(Makofi)*

Natambua sasa na sisi ndo tunalihangaikia hilo hilo, tumeanza na ile Sheria na sisi hatutosimama mpaka tuhakikishe hili linaondoka kwenye orodha ya mambo ya muungano. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa taratibuni sana kwa sababu unachanganya mitambo yetu huko ndani.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Waheshimiwa Wajumbe watupe nafasi haya mambo tuyashughulike kwa sababu haya mambo kwa sababu mambo haya yanataka ridhaa za pande zote mbili. Mhe. Spika, ingekuwa tutunge Sheria kama tulivyotunga yetu ya mafuta au tufanye marekebisho ya Katiba kama tunavyoyafanya yetu, basi nadhani *by now* tungekuwa tushamaliza. Lakini inabidi tuzungumze na wenzetu, wenzetu wana *sentiment* zao, wenzetu wana mawazo yao lakini maamuzi ya upande wa Zanzibar yameshatoka. Sasa tupeane muda na hili jambo litoke Mhe. Spika.

La pili Mhe. Spika, ambalo ningeomba kulizunguza ni jambo ambalo Mhe. Hassan na baadhi ya Waheshimiwa wamelizungumza jambo la muundo wa Tume ya Uchaguzi. Mhe. Spika, muundo wa Tume ya Uchaguzi umewekwa Kikatiba chini ya sura ya 9 kuanzia kifungu cha 119 mpaka 120 na uzuri wake kama kifungu hichi si miongoni mwa vifungu ambavyo vimewekewa kinga na Kifungu cha 80 (a). Kwa hivyo marekebisho yake hayataki yaende kwenye kura ya maoni. Marekebisho yake yatafuata utaratibu uliowekwa na Katiba kupitia kifungu cha 80.

Sasa nimtoe hofu Mhe. Hassan kama hili jambo halihitaji kwenda kwenye kura ya maoni kwa sababu halijawa, kupitia kifungu cha 80 (a) yaliobaki ni maamuzi. Sasa niwasihi sana Waheshimiwa Wajumbe na wengi watakumbuka

tulipoleta marekebisho ya Katiba ya kifungu cha 66. Kila mtu alikuwa na marekebisho yake ya muundo wa Tume ya Uchaguzi. Kila mtu alikuwa na *schedule of amendment* yake katika watu 80 kuna *schedule of amendment* karibu 80 kila mtu ana muundo wake.

Mhe. Spika, sasa hatuwezi kwenda hivyo lazima ifike pahala tukubaliane kama kweli ndiyo dira hii ya Baraza. Kama kweli ndiyo dira hii ya Serikali kuendelea huko basi lazima tukubaliane na hayo maamuzi yatakapotoka, basi utaratibu wake ni kufuta kifungu cha 80. Hakuna haja ya kuitisha kura ya maoni. Sasa nadhani nimelitolea ufafanuzi iliobaki itumike stara na uamuzi. Na utaratibu wa kuleta sina haja ya kuzungumzia, najua kila mtu anaujua uko Kikanuni na Kanuni hizi mpya ndio zimetoa fursa kubwa zaidi. Lakini nasema mambo haya lazima tukubaliane kwa pamoja ili sasa maamuzi yatakapotoka yasiwe tu maamuzi ya Mjumbe mmoja.

Mhe. Spika, pamoja na kutambua kama Wajumbe wana fursa na haki ya kuleta Mswada binafsi lakini lazima tutambue kama jambo hili marekebisho yake hayakufanywa tu kiwepesi wepesi, sote tunajua muundo wa Tume ulivyoanza. Tume kwanza Mwenyekiti wake alikuwa ni Spika lakini ikabadilika mwaka 2002 ndiyo tukatia Muundo wa Tume ndani ya Katiba. Sasa nadhani ufafanuzi huo utamtosha Mhe. Hassan ku-*make up his mind* kwa utaratibu gani ambao anautaka aufuate kabla hakuamua kwenda kuchukua fomu mwaka 2020. *(Makofi)*

Baada ya kusema haya Mhe. Spika, naomba niungane na wenzangu wote kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwanasheria Mkuu. Sasa naomba nimwite Mhe. Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mihayo Juma N'hunga.

Mhe. Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fura hii kuchangia na kutoa maelezo machache kwa zile baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wajumbe walikuwa wakitoa juu ya Taasisi na Idara mbali mbali kama ambavyo ilivyokuwa katika hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ya mwaka 2017/2018.

Kabla sijaanza huko Mhe. Spika, nami naomba kuruhusu nitoe salamu zangu za pole kwa wenzetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania upande wa Tanzania

Bara kwa yale maafa yaliyowakuta kwa kupata ajali na kupoteza ndugu zetu, watoto wetu vijana takriban 32, walimu wao 2 na dereva 1.

Lakini pia Mhe. Spika, na mimi nitumie fursa hii kuungana na Wajumbe takribani ya wote ambao walikuwa wakisimama hapa kwa namna moja ama nyengine, lakini hata pia ambao wamechangia kwa maandishi, kuhusiana na kuwapa pole ndugu zetu, wananchi wetu, wenzetu ambao wako katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba, wamefikwa na kadhia kubwa ya mvua ukiamini iliyotokea si mipango ya Serikali au si mipango yetu sisi, kilichotokea ni kudra za Mwenyezi Mungu. Lakini jambo zuri kama bado Serikali iko pamoja kila siku ipo vizuri na tathmini ya awali tayari imeshafanyika utaratibu sasa utafuatia itabakia hatua za utekelezaji ili kuweza angalau kutoa *relief* kwa watu wetu.

Mhe. Spika, na mimi nianze kutoa angalau ufafanuzi wa zile hoja ambazo Waheshimiwa Wajumbe walizoziitoa. Tukianza na Mhe. Musa Foum Mwakilishi wa Jimbo la Kiwani ambaye katika hoja ya Mfuko wa Jimbo alipendekeza ama alitoa rai kwamba sasa ameona imefika haja ya Serikali kuongeza fedha hii kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo.

Mhe. Spika, sisi kama tukiwa ni Wizara na Serikali tunakiri kwamba tunaamini kiwango hiki ambacho wanapewa Waheshimiwa Wajumbe ni kidogo, inawezekana hakikidhi haja kwa hatua kubwa. Lakini siamini kinapunguza matatizo yetu kwa namna moja ama nyengine pale ambavyo tunakubaliana na wazo lake. Lakini tunaomba atustahamilie pake kadri ambavyo mfuko wetu utakuwa unaimarika. Naona itakapokuwa kuna haja kubwa ya kufanya hilo ambalo Mheshimiwa Mjumbe amelizungumza hatutosita kufanya hivyo.

Lakini pia ilitoka hoja hapa hapa katika mfuko huu wa jimbo kutoka kwa Mhe. Yussuf Hassan Iddi Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni ambaye na yeye alizungumzia suala zima la Kamati hizi kupata semina. Mhe. Spika, bahati nzuri sana Ofisi yetu ya Makamu wa Pili wa Rais bado iko wazi, ipo huru muda wote na imetoa fursa kwa Wajumbe wote ambao bado wataendelea kupata ukakasi wa jambo lolote kuweza kufika. Lakini kwa hatua ambazo ilianza kuzichukua kwa majimbo yote ya Unguja na Pemba angalau kutoa elimu stahiki kwa baadhi ya Wajumbe ambao tulikuwa tunaamini nao watakaporudi katika kamati za watatoa elimu ile ya kutosha kwa baadhi ya Wajumbe wengine. Lakini Mhe. Mjumbe huyu amekuja na rai ameona ipo haja na wao sasa na wao sasa wengine kuweza kupata semina hiyo ili kuweza kuleta ufanisi zaidi, rai yake tumeipokea tutaifanyia hilo.

Lakini Mhe. Spika, tutumie fursa hii sana kulipongeza na kulishukuru Jimbo la Tunguu ambalo kwa dhati kabisa baada ya kupata mkanganyiko ule waliona ipo haja ya kufika katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupata elimu na kujifunza vya kutosho. Tumshukuru sana Mhe. Mwakilishi alikuja yeye na Kamati yake ili kuweza kupata maelekezo ya ziada.

Mhe. Spika, tulikuwa tunaomba Waheshimiwa wengine waione tabu kuja katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais watendaji wetu wapo. Sisi wenyewe tupo na tupo kwa dhamira ya kutaka kupunguza matatizo kwa wananchi wetu, tupo kwa dhamira ya kutaka kusaidiana, sisi viongozi ili tukienda kwa wananchi wetu angalau tuwe tumepunguza baadhi ya matatizo mengine.

Mhe. Spika, lakini pia hapa hapa ilikuja hoja kutoka kwa Mhe. Asha Abdalla Mussa Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa ambaye na yeye alizungumzia katika suala zima la Wawakilishi wa Viti Maalum kwamba nao pia waliona iko haja ya kupata mfuko maalum kwa dhamira ya kwenda kusaidia Taasisi zao ama Jumuiya zao ambazo wanaziwakilisha hapa Barazani.

Mhe. Spika, sisi tumeiona baadae haja ya kuzingatiza ushauri huo. Hata na sisi tunakubaliana na wazo lake kwamba ipo haja sasa ya kuanza kuwafikiria na kuwatoa. Lakini wazo hili tutalichukua na kulifanyia kazi la viongozi wetu wa Kitaifa hawa wana dhamira ya kusaidia watu wote katika makundi yao na maeneo yao walikotoka. Sasa tunaomba watustahamilie kidogo lakini dhamira ya Serikali ni kutaka kuwasaidia watu wote katika maeneo yao.

Mhe. Spika, nende moja kwa moja sasa katika Taasisi za Idara ya Walemavu ambayo tunashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe ambao wapo wengi waliotoa michango yao katika kuchangia katika suala hili. Lakini nianze na Mhe. Shehe Hamad Mattar ambaye alikuwa na hoja nzuri kuhusiana na Idara ya Watu Walemavu ambao yeye alitaka kujua ni kesi ngapi sasa ambazo mpaka hivi sasa Idara hii imeshazishughulikia ama imezipatia ufumbuzi.

Mhe. Spika, naomba sasa nitoe maelezo mafupi ili kwa faida ya Wajumbe wote na Wazanzibari ambao wanatusikia. Kwa mwaka 2016/2017 jumla ya kesi za udhalilishaji zilizowagusa watu wenye ulemavu zilizofuatiliwa na Ofisi yetu. Tulikuwa tuna jumla ya kesi 10, Unguja kesi 5 na Pemba kesi 5. Kati ya kesi hizo ambazo zimeripotiwa katika Ofisi zetu, kesi moja tu ndio ambayo imeweza kutolewa hukumu katika Mahakama ya Mkoa Mfenesini na Mhe. Hakimu Nassor Khamis. Kesi hii imetolewa hukumu kwa kosa la kutoroshwa na kubakwa ambapo kutoroshwa ilitolewa hukumu ya kumfunga miaka mitatu na ya kubaka miaka saba pamoja na faini ya 500,000/=.

Mhe. Spika, nilisema niseme hili angalau tuoneshe ile namna ambavyo tumekuwa tukiwajibika na kwa namna yoyote kuweza kulinda haki za wenzetu ambao wamepata kadhia hii ya ulemavu. Tukiamini sisi sote kama ambavyo tumekuwa tukitambua na baadhi ya wachache walisema hapa katika michango yao. Sisi sote tukitambua kwamba bado ni walemavu watarajiwa hakuna mtu ambaye anajua hali yake kwa sasa na ndio maana serikali iliona ipo haja ya kuwa na taasisi na idara maalum ambayo itakuwa inashughulikia kesi za walemavu.

Mhe. Spika, pia namshukuru sana Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis ambaye kwa uelewa mkubwa amekuwa akitusaidia sana katika masuala ya shughuli hizi za walemavu. Kwanza namshukuru na kumpongeza kwa jitihada zake binafsi, yeye sambamba na kusaidia Jumuiya za Watu Wenye Ulemavu kwa kile ambacho amekuwa akifanya. Na tunaendelea kutoa wito kwa Waheshimiwa wengine angalau tuwe tuna wigo wa Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis ambaye amekuwa akijitolea sana katika shughuli hizi za walemavu.

Mhe. Spika, pia Mheshimiwa huyu alikuja na hoja ambayo alikuwa anakumbushia ile sheria iliyokuwepo katika kitabu chetu cha bajeti ya 2016/2017, alikuwa anauliza sheria ile sasa imefikia katika hatua gani. Jibu la kumwambia mpaka sasa tumefikia katika hatua za mwisho kabisa za kukamilisha Kanuni zile ambazo zilikuwepo katika hotuba ya bajeti ya 2016/2017. Mara baada ya kukamilisha hili Kanuni hizi zitaanza kufanya kazi na zitasambazwa katika Jumuiya zote za watu wenye ulemavu kwa dhamira ya kuendelea kujenga uelewa mpana wa kutaka kusaidiana juu ya jambo hili la walemavu.

Mhe. Spika, katika ibara hii hii Mhe. Mwanaasha Khamis Juma naye pia alikuwa ni miongoni mwa watu ambao wametupa ushauri. Mhe. Spika, tukiri kwamba tunapokea ushauri wake, tunapokea maelekezo yake. Lakini pia ilikuja hoja kwamba ni jumuiya ngapi za watu wenye ulemavu ambao zimepatiwa ruzuku na wamezitumia vipi.

Mhe. Spika, naomba nitoe maelezo kwa ufupi kabisa katika kumsaidia Mhe. Mjumbe kwamba jumuiya zinazopatiwa ruzuku huwa zinajipangia matumizi kulingana na mahitaji husika ambao wenyewe walikuwa wakiyahitaji. Lakini pia Mhe. Spika, jumuiya zote tano moja ilikuja na mpango wake wa matumizi ikiwemo kuyatanabahisha mpango kazi wa jumuiya hizo sambamba na kufanya uchunguzi ili kupata viwango vipya vya malipo ya pango na ofisi.

Mhe. Spika, naomba nizitaje hizi jumuiya ambazo idara yetu imekuwa ikizisaidia kwa dhamira ya kutaka kusaidiana kazi baina ya Serikali na Jumuiya nyengine ambazo ni za binafsi na taasisi nyengine. Tuna Jumuiya ya JUWAZA, Kituo cha Walemavu na Maendeleo ya Jamii, pia tuna Chama cha Viziwi Zanzibar sambamba na jumuiya kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa akili *ZAPDB.*

Mhe. Spika, tulikuwa pia tunaupokea mchango kutoka kwa Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele Mhe. Ali Suleiman Ali ambaye na yeye alizungumzia kuhusiana na kadhia hii ya walemavu kwa namna moja ama nyengine. Yeye alitaka kujua watu wenye ulemavu wanaotakiwa kujumuishwa na kujuulikana popote walipo.

Mhe. Spika, kwa kumjibu Mhe. Mjumbe hili nataka kuwasaidia Waheshimiwa wengine kwamba tayari taasisi yetu kwa kushirikiana na Masheha imeshafanya utafiti wa kutosha kujua ni idadi ya watoto wangapi ambao wamekuwa na ulemavu katika maeneo yetu ya Shehia. Tuna takriban watu 16,000 ambao wapo katika jamii zetu, katika Shehia zetu na mitaa yetu na nyumba zetu ndani ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba ambao wamekumbwa na tatizo hili la ulemavu.

Mhe. Spika, pia tunapokea na kuthamini mchango wa Mhe. Omar Seif Abeid ambaye yeye alitushauri katika Ofisi yetu ya Uratibu iliyokuwepo Dar es Salaam. Mhe. Omar alizungumzia kuhusiana na kadhia kubwa ya jengo letu la Ofisi ya Uratibu iliyokuwepo pale Dar es Salaam. Na sisi kwanza tukiri kwamba kwa kipindi kirefu tulikuwa na jengo ambalo hatukulikarabati wala kulifanyia ukarabati kwa kipindi kirefu. Lakini kwa hatua za awali na tunawashukuru sana wenzetu wa Kamati ya Kudumu ya Ofisi ya Viongozi Wakuu kwa jitihada zao na ushauri wao ambao wamekuwa wakituelekeza mara kwa mara kwa yale ambayo wamekuwa wakiyasema katika Ofisi yetu iliyopo Dar es Salaam.

Mhe. Spika, mpaka kufikia sasa wizara imeshafikia hatua nzuri kwa yale ambayo walikuwa wametuelekeza na tumeshayafanyia kazi kwa asilimia takriban 70. Kilichobakia sasa tumekabiliwa na jukumu kubwa la kutaka kufanya ukarabati wa kina katika jengo letu lile lilokuwepo pale Dar es Salaam. Sisi tumuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba kadri ambavyo bajeti yetu itakuwa inaruhusu, na kadri ambavyo hali ya uchumi wa taifa itaruhusu na sisi tuna tamani sana, tuwe na jengo zuri ambalo lenye kurahisisha mambo mengi katika Ofisi yetu ile ya uratibu.

Mhe. Spika, vile vile Mhe. Omar hakusita pia kutuelekeza na sisi tunapokea ushauri wake wa kuja kufanya semina kwa wale watendaji wetu ambao wapo katika Ofisi yetu ya Uratibu Dar es Salaa. Tunapokea huo ushauri mzuri ambao una dhamira ya kujenga na kuboresha taasisi zetu hizi tulizokuwa nazo.

Mhe. Spika, sasa nakuja kwa hoja ya Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Mwakilishi wa Viti Maalum kutoka Wilaya ya Magharibi "B". Yeye alizungumzia kuhusiana na Baraza la Wawakilishi. Sisi kama Wizara na kama serikali tukiri kwamba kweli katika hizi siku za karibuni tumekuwa na hii hali na kadhia ya baadhi ya maeneo machache katika jengo letu kuwa lina uvujaji. Tutalitizama hilo na tutafanya marekebisho kadri pale ambavyo tunaweza kujitahidi na katika bajeti yetu hii tutajitahidi katika maeneo yote ambayo yamekuwa na hali iliyokuwa si nzuri na ya kupendeza hasa katika jengo tukufu kama hili kuwa katika hali kama hizo. Lakini tutatizama itakavyowezekana wataalamu wetu watakapokuja namna watakavyotushauri ili kuweza kupafanyia marekebisho katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, ilitoka hoja kwa Mhe. Tatu Mohammed Ussi kuhusiana na jengo la Ofisi ya Baraza la Wawakilishi la Pemba, ili nalo kulifanyia ukarabati kuweza kutoa shughuli zetu za Baraza kutoka Unguja kuwa zinafanyika Pemba. Wazo hili Mhe. Mwakilishi ni la muda mrefu na niwaambie tu Waheshimiwa Wajumbe bado dhamira ya serikali ipo pale pale na bado dhamira ya wizara ipo pale pale kwa hatua za awali tumeanza kufanya maboresho makubwa katika zile Ofisi za watendaji zilizokuwepo pale Wete Pemba. Kilichobaki sasa ni kukaa na kuanza kufanya tathmini mpya na nyengine ambayo itakuja na mapendekezo mapya ya kutaka kuboresha jengo letu hili kwa kuweza kutusaidia sisi kurahisisha shughuli zetu. Siku moja moja tutakuwa tunatoka Unguja tunakwenda Pemba kupata mambo mengine mazuri zaidi.

Mhe. Spika, pia ilikuja hoja kuhusiana na Mfuko wa Maendeleo wa *TASAF* ambao nao upo katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Ninawashukuru Wajumbe wengi waliochangia katika hili lakini ilitoka hoja pia kwa Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, Mwakilishi wa Jimbo la Chaani kwamba mpaka sasa katika jimbo lake la Chaani je, ni Shehia ngapi ambazo zimenufaika na mradi huu wa *TASAF*. Lakini je, tumekuwa tukijitahidi vipi katika kukabiliana na changamoto ambazo zimekuwa zikijitokeza.

Mhe. Spika, naomba nimsaidie tu Mhe. Mjumbe kwamba katika Jimbo la Chaani mpaka hivi sasa tumeweza kuzipa Shehia tatu ambazo zimeshaingia kwenye mpango wa moja kwa moja wa kunufaika na *TASAF* na Shehia

zenyewe ni Shehia ya Chaani Masingini ambayo imekuwa na walengwa 212. Shehia ya Bandamaji imekuwa na walengwa 102 na Shehia ya Kinyasini imekuwa na walengwa 149. Jumla ya walengwa katika Shehia hizi ni walengwa 463 katika Shehia hizi ndani ya Jimbo la Chaani, lakini mpaka hivi sasa wamenufaika nini. Jumla ya Shehia zote hizo tatu tumetumia takriban shilingi 218,000,000 ambazo zimelipwa kwa Jimbo la Chaani ikiwa Shehia ya Bandamaji imepata milioni 88,213,297/- lakini pia Shehia ya Kinyasini imepata jumla ya shilingi 55,888,000/- na Shehia ya Chaani Masingini imepata takriban milioni 74,772,000/-.

Mhe. Spika, hii ni namna ambavyo serikali imekuwa ikiweka jitihada za kutosha kabisa katika kuhakikisha inaweza kuwasaidia na kusaidia hali za kiuchumi za wananchi wetu…

Mhe. Spika: Umebakiwa na dakika mbili mheshimiwa…

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Huu ni upana ambao ni mdogo tu uliokuwepo katika Jimbo la Chaani…

Mhe. Spika: Dakika mbili mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Dakika mbili?

Lakini ukiacha hivyo Mhe. Spika, tuna miradi mingi ambayo bado imekuwa ikiendelea katika Jimbo la Chaani. Nimuombe tu Mhe. Mwakilishi sambamba na Waheshimiwa wengine ambao Shehia zao zimekuwa zikinufaika katika mfuko huu wa *TASAF* warudi katika viongozi wao wa Shehia kupitia Masheha watakuta mabuku yetu pale ya *TASAF* na mabuku yale yataonesha kaya zote ambazo zimekuwa wanufaika wa *TASAF*.

Mhe. Spika, zilitoka hoja nyingi za *TASAF* kutoka kwa Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, Mhe. Mussa Foum Mussa na Waheshimiwa wengine kwa haraka haraka tu lakini endapo utaturuhusu tutawapa majibu kwa njia ya maandishi ili wapate kujibu maana tumeshayaandaa yote kwa pamoja.

Mhe. Mwanaasha alitoa hoja ya kaya ngapi zilizoondokana na umaskini katika jimbo letu. Mhe. Spika, tuna kaya nyingi ambazo mpaka hivi sasa zimekuwa wamenufaika na mradi huu wa *TASAF*. Kama ambavyo tumetoa mfano katika Jimbo la Chaani tujue katika Jimbo letu la Chukwani ambalo Baraza lako

tukufu lipo hapa, pia na wenyewe wamekuwa na watu wanaonufaika kama watu wa Chaani namna ambavyo tumekuwa tukijitahidi.

Pia Mhe. Mussa Foum Mussa alizungumzia suala zima la kuwepo kwa watu ambao hawakustahiki kupokea fedha hizi. Jambo ambalo tunaiomba jamii na tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe tuwe wazuri wa kutoa taarifa, maana wakati mwengine taarifa zetu tunapozitoa ndio ambazo zinaturahisishia sisi kuingia katika mpango huu wa *TASAF*. Lakini wale ambao hawakuwepo katika mradi huu tunatizama utaratibu kwa sababu mradi huu bado tunao tutatizama huko mbele namna ambavyo tutakuja…

Mhe. Spika: Mheshimiwa naomba uunge mkono hoja.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa na mimi naomba niunge mkono hoja hii ya hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa 2017-2018 kwa asilimia mia.

Nakushukuru Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili aje ahitimishe hoja. Karibu mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele yako ili kuunga mkono hoja aliyowasilisha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, baada ya kukushukuru wewe kwa kuniruhusu naomba uniruhusu kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa namna ambavyo anaiongoza nchi yetu kwa hekma kubwa na busara na kuiweka katika hali ya amani na utulivu, umoja na upendo kitu ambacho kimetuwezesha kupiga hatua kubwa za maendeleo katika nchi yetu. Kwa hivyo tuna kila hali ya kumshukuru na kumpongeza na Mwenyezi Mungu amjaalie yeye na familia yake mafanikio zaidi ili aweze kutuongoza vizuri zaidi.

Aidha, nichukue fursa hii Mhe. Spika kumshukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa namna anavyomsaidia Mhe. Rais katika kuongoza nchi yetu. Lakini pia kwa namna anavyotuongoza katika Ofisi yetu ya Makamu wa Pili wa Rais.

Kwa mfano, mzuri, mtendaji hodari, ni mtu anayekusikiliza sisi tulio chini yake tunafanya kazi kwa mashirikiano makubwa tunamshukuru sana.

Mhe. Spika, pia naomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe na viongozi wote mnaoliongoza Baraza hili akiwemo Naibu Spika na Wenyeviti wetu kwa umahiri wenu wa kuongoza, mnatuongoza vizuri na kulisimamia vyema Baraza letu, tunakushukuru sana na tunakupongeza wewe na viongozi wenzako.

Aidha, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa yeye na Wajumbe wenzake kwa mashirikiano makubwa sana wanayotupa katika wizara yetu. Kwa kweli Kamati hii imekuwa ni dira ya utendaji kazi katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, nawashukuru sana viongozi. Aidha, niwashukuru Wajumbe wote wa Baraza hili tukufu kwa namna ya mashirikiano yao kwetu kwa ofisi na kwa serikali, kwa kweli Mhe. Spika mashirikiano wanayotupa Wajumbe wako ni makubwa na ni ya kupigiwa mfano, tunawashukuru sana.

Aidha, naomba uniruhusu nitoe shukurani maalum ziende kwa Mhe. Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa namna anavyoshirikiana na mimi na anavyonisaidia, na mfano hai tumeona hapa sasa namna alivyokuwa akishiriki kwa ukamilifu kujibu hoja mbali mbali za Wajumbe. Nimshukuru sana Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mashirikiano makubwa wanayotupa na kwa kuweza kuikamilisha vizuri hotuba yetu ya bajeti na kazi nyengine zote ambazo zinakuwa mbele yetu. Mheshimiwa nawashukuru sana.

Mhe. Spika, kabla ya kuanza kujibu hoja naomba uniruhusu nipokee katika kitabu chetu karatasi hizi mbili ambazo zina muhtasari wa makadirio ya mapato, kikasma katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika fungu C01 ambalo linazungumzia Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa na Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, inaeleza pale kwa kina mapato na makadirio. Naomba tena uniruhusu niwasilishe mezani muhtasari wa makadirio na mapato katika buku lile kubwa la Tume ya Uchaguzi katika kifungu C03 utawala Unguja baada ya kupoteza vitambulisho. Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba niwasilishe rasmi ili iwe ni sehemu ya buku lile.

Mhe. Spika, kwanza naomba uniruhusu nitoe salamu za pole kwa wale wote waliokubwa na maafa yaliyotokana na athari za mvua ambazo zimenyesha. Ndugu zetu hawa wamepata mtihani nawaombea dua Mwenyezi Mungu awapokee vizuri katika matatizo yaliyojitokeza, naamini *Inshaallah* Mwenyezi

Mungu atatuweka katika hali nzuri ili mvua hizi ziendelee kuwa za salama na kila aliyeathirika apate manusura.

Aidha, nitoe mkono wa pole kwa Marehemu Rahika, mtoto wetu huyu mdogo aliyefariki dunia kutokana na kuangukiwa na ukuta wa madrassa yao pale Chanjaani, Chake Chake Pemba. Aidha, nitoe mkono wangu wa pole kwa watoto waliopata msiba wa kufariki dunia kule Arusha pamoja na walimu wao na dereva ni msiba mkubwa na wa taifa kwa jumla.

Mhe. Spika, licha ya kuwashukuru Wajumbe wote waliochangia ambao Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atakuja kuwatambua na kuwataja mmoja baada ya mmoja wale waliochangia kwa maneno na wale waliochaangia kwa maandishi. Naomba uniruhusu niwashukuru sana Mawaziri waliosimama mbele ya Baraza lako tukufu kusaidia kujibu hoja mbali mbali. Kwanza nimshukuru sana Mhe. Said Soud Said, Waziri asiye na Wizara Maalum, Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi kwa maelezo yake mwanana na fasaha, namshukuru sana Mhe. Said. Aidha, nimshukuru Mhe. Waziri wa Fedha kwa maelezo yake mazuri naamini Waheshimiwa wameelewa, amesaidia sana katika kueleza na kutoa ufafanuzi katika hotuba yetu hii.

Vile vile nimshukuru Mhe. Rashid Ali Juma, Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ambaye ametoa mchango wake kwa maandishi, naamini watakaposoma Wajumbe wataona ufafanuzi mzuri ambao ameuelezea.

Pia nimshukuru sana Mhe. Mwanasheria wetu Mkuu Sheikh Said Hassan Said kwa maelezo ya kina, naamini Wajumbe wameridhika nayo sana na shukurani za kipekee ziende kwa Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa namna alivyojibu hoja kwa ufasaha sana.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba nianze kwa ushauri. Mhe. Spika, sisi viongozi wa humu ndani tunafaa sana kuelewa kauli zetu tunazozitoa hapa. Maana kauli zetu hizi tunazitoa katika chombo kikubwa na zinasikikana na wengi, zinaweza kuleta taathira kubwa ama zinaweza kuleta manufaa makubwa kwa maendeleo ya nchi yetu. Kwa hivyo ni vizuri sana lugha zetu tunazotoa katika chombo hiki kikubwa ziwe ni lugha zenye kujenga, zenye maendeleo, zenye heshima na nidhamu ili kila mmoja anayeshiriki katika chombo hiki aweze kuona kwamba sote tuko pamoja, tuna lengo moja tunajenga nchi kwa maelewano na mashirikiano makubwa sana.

Kwa kiongozi yeyote ni lazima kujua uongozi ni busara na hekma, kukataa neno busara na hekma kwa kiongozi ni mtihani kidogo, lazima tukubali

kwamba hekma na busara ni sifa kubwa ya uongozi na inatupasa sote kwa pamoja. Mhe. Spika, katika uongozi wetu kutumia maneno hayo. Hekma na busara ambazo Mhe. Rais wetu amezitumia ndio ameweza kupata mafanikio makubwa na kupita katika kipindi kigumu ambacho kilitokea baada ya uchaguzi wa marudio ni kutokana na hekma zake, busara zake na uvumilivu wake ndio nchi yetu imebaki katika hali ya amani na utulivu mkubwa. Nampongeza na namshukuru sana. Kwa hivyo, tuna wajibu huu wa kuiga mifano hii.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo vile vile kwa kiongozi kusema atapambana na Polisi si lugha nzuri hata kidogo. Maana Polisi mimi nimefanya kazi nao nawajua, licha ya kwamba wana uwezo kwa mujibu wa sheria, wana kitabu chao, *Police General Order;* kile ndicho wanachokifuata kinawapa nguvu kisheria kusimamia utekelezaji wa sheria. Sasa si vizuri kusema baadhi yetu tunaweza kupambana na Polisi, ni vizuri unapoona Polisi amefanya kosa ikiwa la rushwa ama jengine zipo taratibu za kisheria, zipo taratibu za kiutawala, zipo taratibu za kiuongozi ambazo tutachukua hatua ili kama kiongozi uendelee kuwa na heshima yako, uendelee kuheshimiwa na uendelee kutekeleza wajibu wako kwa kukemea maovu yanapotokea. Lakini kupambana si msingi wa kuendeleza sheria bali ni uvunjaji wa sheria pia.

Mimi napenda niwashauri hususan ndugu zangu Wawakilishi wapya wajue yako mambo ya kuendelea kuwa na subra, hekma, kupima kauli na ni vizuri sana katika kusema ujue unasema na nani, unasema nini na unasema wapi. Maana matokeo yake yanaweza kuleta athari kubwa sana. Kwa hivyo sisi Waheshimiwa Wawakilishi tuelewe tuna *immunity* yetu kweli lakini *immunity* yetu imo humu ndani unapotoka nje ukavunja sheria *immunity* ile inaruka na taratibu nyengine za kisheria zitakuandama. Kwa hivyo mimi sishauri hata siku moja kwa kiongozi yeyote kupambana na Polisi. Ninachoshauri kwa kiongozi yeyote kuchukua hatua zinazofaa kisheria na kufanya mambo vizuri ili tujenge nchi yetu ili tuwe kitu kimoja na ili twende pamoja.

Mhe. Spika, vile vile kauli hasa za kuwasema viongozi wetu wakuu kama humu ndani, kumsema kidogo kwa kauli kali, kauli ambayo haifurahishi, lugha iliyokuwa si nzuri kwa Makamu wa Pili wa Rais. Kama liko jambo hujalielewa Mwakilishi unayo haki ya kutaka kulielewa, unayo haki ya kushauri, unayo haki ya kukosoa na ungojee majibu. Kiongozi wetu huyu Makamu wa Pili ana imani na sisi Wawakilishi wote, anatutakia mema sote, anahitaji tufanye kazi kwa pamoja, ana dhamira kubwa ya kuona Chama chetu cha Mapinduzi katika mwaka 2020 kinapata ushindi mkubwa. Kwa hivyo ni kiongozi ambaye ukimtazama anakuwa baba kwa namna anavyotulea, kwa namna

tunavyoshirikiana naye. Kwa hivyo kuna baadhi ya mambo yanapojitokeza ni vizuri tukazungumza kwa lugha ambazo sote kwa pamoja tukazielewa vizuri, tukajenga nchi yetu kwa pamoja kwa mafanikio yetu kwa pamoja. *(Makofi).*

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba katika *page* ya 15 ni kweli ilionesha ahadi alizotekeleza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika jimbo lake. Hapa nataka niseme Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ana kofia mbili, ni Makamu wa Pili wa Rais lakini pia ana jimbo lake, ni mwakilishi wa jimbo, ana wajibu katika jimbo, ana wajibu katika taifa letu na kazi zote hizo anazifanya kwa umakini mkubwa, kwa umahiri mkubwa, kwa uadilifu mkubwa sana. Hongera sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. *(Makofi)*

Mhe. Spika, limezuka suala kubwa katika ukurasa ule wa 15 namna alivyopeleka madeski jimboni kwake. Suala la madeski kwa sasa ni suala la kitaifa hakuna Wilaya, hakuna Jimbo halijapata mgao wa madeski. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwenye eneo hili ametumia fedha zake binafsi katika kusaidia jimboni kwake. Vile vile wafadhili waliojitolea kumsaidia ndio ambao alishirikiana nao katika suala zima la kusaidia shughuli mbali mbali za maendeleo katika jimbo lake, huwa hachanganyi fedha za serikali na fedha anazozitoa kwa ajili ya kusaidia jimboni kwake. Mimi nilidhani kwa Wawakilishi ni mfano mzuri sana anaoutoa na ni vyema tukaiga juhudi anazozifanya katika kusaidia jimbo lake. Naamini sana Wawakilishi wengi wanafanya hivyo katika kusaidia majimbo yao. Kwa hivyo kusaidia kwake sidhani kuwe nongwa zaidi ya kumpongeza kwa kufanya kazi nzuri katika kuwatumikia wananchi wa jimboni kwake na kwengine. Kama alivyosema Mhe. Said Soud Said kwamba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais misaada yake huwa haisimami kwa jimboni kwake, inasimama kila pale anapohitajika na uwezo unapokuwepo anachangia, anasaidia, anashiriki.

Kwa mfano, katika kitabu chetu hicho pia kilieleza mchango wake katika Mfuko wa Siti Binti Sadi. Kilieleza mchango wake katika Jumuiya ya ZANAB. Kilieleza mchango wake katika kuchangia maafa yaliyotokea Mkoa wa Katavi, alikwenda kule kwenye sherehe za mwenge na akachangia baada ya kupata maelezo na alikwenda kumuwakilisha Rais wa Zanzibar, alipokwenda pale alijitutumua vizuri katika kutoa msaada. Kinaeleza namna ya kusaidia huduma mbali mbali za afya kama vile Hospitali ya Mnazi Mmoja, Hospitali ya Kivunge, Hospitali ya Makunduchi na kadhalika, amesaidia zaidi ya shilingi 45 milioni kwa wananchi mbali mbali wanaokuja na matatizo yao kumuona Ofisini kwake na pahala pengine panapotokea matatizo, amesaidia mambo mbali mbali ya kusaidia katika kutatua migogoro mbali mbali ikiwemo ya ardhi na mengine. Kama alivyosema Mhe. Said Soud hata anapokwenda nje katika

ziara zake wakati wote anasimamia misimamo ya kusaidia taifa letu, kusaidia nchi yetu, kusaidia na wananchi wake.(*Makofi*).

Kwa hivyo, viongozi wa namna hii wanaojitolea kwa ajili yetu ni lazima tunza yao iwe ni kuwaheshimu na kuwapa maneno ya kuwatia moyo ili waendeleze wawe na moyo na ari ya kuendelea na jitihada hizo kwa manufaa yetu sote. Kwa hivyo ni vizuri sana baadhi ya maneno yetu tunayoyazungumza humu ndani tukayapanga vizuri ili yasilete taathira ya kuleta mfarakano au kutoelewana wenyewe kwa wenyewe, ni vizuri sana kujenga lugha za nidhamu, heshima ndio silka yetu Wazanzibari.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mimi nitaendelea tena leo kumuomba ndugu yangu Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwa utaratibu wangu huo huo, maana ndio niliolelewa nao wa kuweka nidhamu na unyenyekevu, kumuomba atusaidie tushirikiane kuipitisha bajeti yetu hii kwa salama na kwa furaha kubwa. Ni mila yetu Wazanzibari kuweka mbele heshima, nidhamu na unyenyekevu wakati unapoomba ni wajibu wetu kuomba, tumekuja hapa kuwasilisha hotuba yetu ya bajeti kuomba fedha ili Waheshimiwa Wajumbe mtupitishie tukafanye kazi za maendeleo ya nchi yetu. Naamini mtatuunga mkono tukafanye kazi hiyo. Hivyo tutaendelea kushirikiana, tuendelee kufanya kazi kwa pamoja ili tupate manufaa makubwa katika maendeleo ya nchi yetu.*(Makofi).*

Mhe. Spika, yako mambo mengi yamezungumzwa na moja lilizungumzwa sana la kuhusu maafa. Nashukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha, Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Mawaziri wengine waliotangulia na baadhi ya Wajumbe walilizungumzia vizuri suala hili la mipango yetu katika kukabiliana na maafa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Fedha alichukua muda vizuri kwa kulieleza kwa ufasaha sana mipango na mikakati ya namna gani tunakabiliana na maafa. Si suala kama lilivyosemwa na wengi kwamba ni suala la zima moto, hatufanyi kazi kwa zimamoto. Tatizo la msingi kabisa ni kwamba mipango hii na mikakati hii ya kukabiliana na maafa inahitaji fedha nyingi. Kwa hivyo lazima twende hatua kwa hatua, hatuwezi mambo yote haya kuyafanya kwa wakati mmoja. Kuna mambo hapa yanahitaji kama nchi kuipima nchi yetu yote kuweko utaratibu mzuri wa matumizi ya ardhi, kujua sehemu gani tutafanya shughuli zetu za makaazi kwa maana ya ujenzi, sehemu gani tutumie za kilimo, sehemu gani za viwanda, sehemu gani tutumie kwa ajili ya shughuli zetu za kibiashara na uwekezaji. Lazima mpango unakuwa mkubwa sana mambo hayo yote yanafanywa.

Mhe. Spika, vile vile kuna mpango wa kuimarisha miundombinu kwa ajili ya kukabiliana na maafa. Kuna mpango wa kuwa na zana, vifaa vikiwemo boti, ndege, helikopta na kadhalika kwa ajili ya mambo ya maafa. Kuna mpango mzima unaoendelea katika suala zima la mtandao wa maji ili kupata maji safi na salama. Kwa hivyo si suala la kwamba ni la muda wa dharura, ni suala linakuwa na mipango ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ili tupate majibu mazuri. Kwa hivyo si suala la zimamoto, ni suala linajulikana na mipango mingi ipo na kama alivyosema Waziri wa Fedha kuwa vitabu kama hivi vipo kila Wilaya vinavyooneshwa mpango wa kujiandaa na kukabiliana na maafa. Katika kila Wilaya kwa mazingira yake na hali yake yapo hayo mambo na wenyeviti wa kamati hizo katika Wilaya, ni Wakuu wa Wilaya na sisi Wawakilishi, ni Wajumbe wa Kamati hizo na kwenye Shehia Madiwani ni Wajumbe wa Kamati hizo. Kwa hivyo sote ni sehemu ya mapambano ya kukabiliana na maafa.

Mhe. Spika, kuna mpango wa mawasiliano alieleza vizuru Mhe. Waziri wa Fedha na kadhalika. Kwa hivyo ni jambo kubwa lazima kwa pamoja tukubaliane nalo, yanapotokea ya dharura tunayakabili kidharura. Hiyo yote inaonesha wazi kwamba elimu ya kukabiliana na maafa imetolewa vizuri. Ndio maana kila mmoja anashiriki katika kulikabili tatizo linapotokea, ndio maana hata wananchi wenyewe baada ya kupata taaluma hii linapotokea haraka haraka wanafanya utaratibu wa kusaidiana kukabili hali ilivyo na mambo kwa kiasi kikubwa sana yanakwenda vizuri. Juu ya hali yetu ilivyo ya kiuchumi, juu ya uwezo wetu wa mambo mbali mbali kimiundombinu na kadhalika, lakini ukitulinganisha na wengine katika ukanda huu wa Afrika Mashariki tunapongezwa sana namna tunavyochukua jitihada, namna tunavyoyakabili maafa yanapotokea. Kwa hivyo lazima tujipongeze na sisi wenyewe kwa namna tunavyofanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna suala kubwa sana wakati wa mvua namna hii zinapotokea. Suala la kupata maradhi ya mripuko. Jitihada kubwa zimechukuliwa na nyote mashahidi hata kabla ya mvua kutokea. Wizara ya Afya, Halmashauri zetu, Wilaya, Mikoa, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na wahusika wote walifanya jitihada za kutoa taaluma mbali mbali ili kuonesha athari zinazoweza kutokea wakati wa mvua. Kwa hivyo elimu kubwa imetolewa, mafunzo yametolewa na mambo mengi yametayarishwa ndio kwa kiasi fulani kwa mujibu wa hali yetu ya uwezo tukaweza kufikia hatua hii ambayo tumefikia na tukakabiliana na hali ilivyo na tumshukuru Mwenyezi Mungu tumepoteza kijana wetu mmoja aliyeangukiwa na ukuta wa nyumba kule Chanjaani lakini mahala pengine kote salama.

Mhe. Spika, matatizo yalikuwa makubwa maana kwa mara ya kwanza milima imeporomoka. Mmeona banda letu la *ZSTC* dongo limeingia ndani, miti imeingia ndani, imeangukiwa Misikiti, zimeangukiwa nyumba. Sasa kwa sababu ya taaluma wananchi wamewahi kutoka kwa salama na tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kupata salama hiyo. Naamini sana Waheshimiwa mtakubaliana na mimi kwamba hatua mbali mbali zimechukuliwa katika kuimarisha vikosi vyetu vya uokozi, Kikosi chetu cha KMKM na kila mdau katika kuhakikisha usalama unapatikana. Hata suala la kununua meli mpya ni sehemu ya kupambana na maafa.

Kwa hivyo haya yote serikali yetu inayafanya na tutaendelea kutoa elimu kwa umma ili tuzidi kuepukana nayo na kila shauri ambalo Waheshimiwa Wajumbe mmelisema hapa tutalithamini, tutalichukua tukalifanyie kazi, maana ndio tunavyofanya kwa muda wote na inatusaidia sana katika kuendeleza kupambana na hali hii na inatusaidia sana katika kupiga hatua za maendeleo katika nchi yetu.

Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe mnayotwambia tunayasikiliza kwa umakini mkubwa, tunayaheshimu na tunayafanyia kazi na matokeo yake ndio hatua kwa hatua yanaonekana majibu ya maendeleo katika nchi yetu. Nataka niwapongeze sana wale majirani ndugu na jamaa waliowasaidia wale wote waliathirika na maafa. Hatua za awali zilichukuliwa katika ngazi zetu za Wilaya na Mikoa na sasa Kamati ya Kitaifa ikiongozwa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais imeshatoa maelekezo kwa wahusika na utaratibu mzima unafanywa baada ya kupata tathmini ya namna gani kusaidiana na wenzetu hawa ili kupunguza machungu ya maafa haya. Serikali itatupa kila jitihada kuhakikisha kila mmoja wetu anabaki salama wakati tunaendelea kushirikiana katika kufanya kazi zetu kwa pamoja.

Mhe. Spika, kwa sababu hili suala la maafa lina maeneo mengi napenda niishie hapo nisiendelee kusema zaidi kwa sababu kuna mambo mengine na wakati unakwenda ili niweze kutolea maelezo na maeneo mengine ambayo yaliulizwa na Waheshimwa Wajumbe. Mheshimiwa ukiondoa suala la maafa, suala jengine ambalo lililozungumzwa kwa upana mkubwa ni suala la madawa ya kulevya. Ni kweli hii ni kadhia kubwa inayoikabili nchi yetu lakini suala sugu si kwa nchi yetu peke yake ni kwa dunia nzima.

Mhe. Spika, mapambano yake ni makubwa, mapambano yake yanahitaji sote kushirikiana kwa pamoja katika kulikabili jambo hili. Ziko hatua zimeanza kuchukuliwa, ziko zimechukuliwa mwazo na sasa tunaziendeleza kwa kasi zaidi na matokeo ya hatua hizo zimeanza kuonekana na nitayaeleza hapo

baadae. Lakini Wajumbe walikuwa na kila sababu ya kulisema jambo hili kwa lugha ambayo wameisema kutokana na hali ambayo inaathiri sana vijana wetu. Hakuna asiyeguswa na athari za madawa ya kulevya kwa vijana wetu na ndugu zetu na watoto wetu na kadhalika.

Kwa hivyo ni jambo ambalo linatugusa sote. Kwa hivyo kwa vyovyote vile kila mmoja mahala alipo ni lazima ashiriki kwa ukamilifu wake katika kupambana nalo. Tukiamua kwa pamoja kwa sababu yanafanyika ndani ya mitaa yetu, yanafanyika ndani ya vijiji vyetu, yanafanyika ndani ya Shehia zetu, yanafanyika ndani ya Wilaya zetu, yanafanyika ndani ya Mikoa yetu. Huwezi kulifanya hili bila ya mmoja wetu kuwepo, yanafanyika ndani ya nyumba zetu. Cha msingi tukiamua sote tukakubali kwamba jambo hili lina athari kwa jamii yetu, naamini sana tutaliondoa na tutapiga hatua kubwa. Lakini tukiwavumilia yuko Mhe. Abdalla Maulid Diwani alisema tusiwe na muhali hapa ni mahala ambapo tusiwe na muhali. Lazima tupambane na waletaji wasambazaji, wauzaji na hata wanaotumia, lazima tuwape ushauri mzuri waache kutumia maana ikiwa hakuna wa kutumia kutakuwa hakuna biashara.

Kwa hivyo lazima kwa pamoja tushirikiane Tume yetu hii ya Madawa ya Kulevya kazi yake kubwa ni mbili, ni kuratibu masuala ya kinga, tiba na marekebisho ya tabia. Kazi ya pili ni kuratibu mapambano dhidi ya madawa ya kulevya. Lakini vipo vyombo vya utekelezaji. Mtekelezaji Mkuu wa kwenye jambo hili ni Polisi, lazima ndugu zetu askari wa Polisi wafanye kazi ya ziada ya kuwakamata wahusika. Maana wananchi wanapeleka taarifa wawakamate na wasitoe siri za wale wanaotoa taarifa. Lazima tuchukue kila jitihada kwa kila mmoja katika sehemu yake kuhakikisha tunapambana nalo suala la madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, ni kweli Waheshimiwa Wajumbe wametaka tuongeze bajeti mwaka huu ukilinganisha na mwaka jana bajeti yake imeongezeka kwa asilimia 79. Tutajitahidi kila mwaka kwa kadri ya uwezo kuongeza bajeti, kuna wako waliodiriki kusema bajeti ya Tume ya Ukimwi ikatwe iwekwe katika bajeti ya madawa ya kulevya. Lakini ningependa niwakumbushe na huku nako kuna tatizo japo tumepiga hatua. Kwa hivyo tatizo likuwa kubwa tukilipunguza sisi wanadamu tuna kawaida ya kusahau tukaona limekwisha. Tume ya Ukimwi ina wafanyakazi wengi kuliko Tume ya Madawa ya Kulevya tabaani bajeti yao itakuwa kubwa.

Bajeti ambayo Tume ya Madawa ya Kulevya wamepewa kutoka na *activity* zao zile *activity* ziliopo, ndio maana wamepewa fedha kutokana na uwezo wetu wa kibajeti lakini ushauri mliotoa Waheshimiwa Wajumbe ni mzuri na tunaukubali

kadri ya uwezo wa serikali utakavyowezekana ndivyo tutakavyoongeza fedha katika Tume hii ya Madawa ya Kulevya. Lakini hapa mkazo uwekwe katika suala zima la mashirikiano kati ya Polisi, Afisi ya *DPP* na Mahakama katika kushughulikia kesi hizi ili zipate majibu mapema na zipate hukumu inayofaa. Kama hukumu hii ya sheria tuliyonayo itakwenda vizuri hakuna haja hata ya wale wengine waliosema kuwe na adhabu ya kifo. Hii iliyopo baada ya kwisha kufanya kazi vizuri watapata adhabu ya sawa sawa na hao wenye nia ya kufanya shughuli hii watawaacha, tunataka mashirikiano makubwa. Hatua zilizochukuliwa kwa sasa kwanza inafanywa kila jitihada kwamba sheria iweze kutekelezeka kwa wepesi.

Jengine kutoa taarifa kwa wanaohusika na madawa ya kulevya. Sasa taarifa ya vyombo vyetu vinafuata kwa utaratibu mzuri hatuitangazi ile hadharani lakini kila ambaye anajulikana huyu yumo anatajwa na vyombo vinaambiwa na kazi imeanza katika kila Mkoa, katika kila Wilaya operesheni hiyo inaendelea. Polisi wana operesheni maalum katika kufanya kazi hiyo. Tumeimarisha ulinzi wetu katika maeneo muhimu ya bandarini na *Airport* na hata katika maeneo ya bandari bubu tunafanya kila njia kila anayehusika na jambo hili mkondo wa sheria umkute.

Mhe. Spika, hivi sasa nathubutu kusema hapa kwamba watuhumiwa 312 wamekamatwa na kuhojiwa kati ya hao wamo wasambazaji maarufu 40 na wanaendelea kushikiliwa na Polisi na wanahojiwa na tunawaomba sana Waheshimiwa msije kuwaombea watoke huko waliko na tutakayembamba tutaendelea naye kwa utaratibu huo huo. Yamekamatwa madawa haya *cocaine* na *heroin* zaidi ya gramu elfu tatu na mia nne, zaidi ya gramu mia nne tisini na tatu za bangi, zaidi ya kilo mia mbili na tatu mirungu, zaidi ya kilo arobaini na sita na jumla ya kesi mia moja thalathini na mbili zimefunguliwa na zipo katika hatua mbali mbali na jitihada zitaendelea na vile vile yako magari mawili, pikipiki tatu na fedha taslimu milioni nne zimekamatwa kama ushahidi katika mapambana.

Mhe. Spika, naamini tunaendelea zaidi na mapambano katika Mkoa wa Mjini/Magharibi. Nataka niupongeze sana ukiongozwa na Mkuu wa Mkoa huo. Mapambano haya wamefanyakazi kubwa wana operesheni maalum wanayokwenda nayo, tunaiunga mkono naamini kabisa kwa jitihada hizo pamoja chini ya Mwenyekiti wetu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na Kamati hii ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Madawa ya Kulevya. Naamini sana Mwenyezi Mungu atatusaidia tuweze kushinda kadhia hii ngumu inayowakabili vijana wetu, ndugu zetu na watoto wetu.

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakika tano.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mheshimiwa nitamalizia dakika tano kwa haraka haraka lakini yako mengi na naamini Waheshimiwa Wajumbe watatuunga mkono kwa sababu wanajua sababu ya muda.

Nimalizie kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia kwa wale waliathirika kile cha pale Kidimni. Wajumbe wengi walitaka kujua gharama za matumizi. Kituo kile mpaka hali ile ya hatua iliofikia zimetumika shilingi bilioni moja na milioni mia nne. Kwa maana ya 1.4 bilioni kwa ujenzi ambao uko sasa. Hizi fedha milioni mia sita tisini na tano zimetengwa bado hazijatumika kwa ajili ya kazi zifuatazo:-

(1) Kujenga jiko na mambo yanayohusiana na hayo.
(2) Kujenga uzio kwa maana ya *fence* katika eneo.
(3) Kujenga sehemu ya kufulia
(4) Kuweka mazingira mazuri kwenye eneo lote lile la kituo chetu sio eneo dogo ni eneo kubwa.

Waheshimiwa Wajumbe mna haki ya kwenda mkaona ili muweze kujua *value for money*.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda na kwa kuwa bado yako mengi ya kueleza lakini naamini kwa kuwa Wajumbe wako hawa watakuwa na imani kubwa na Afisi yetu, naamini watashirikiana kuipitisha Afisi hii kwa kauli moja ili tumalize mapema leo hapa na kesho tuanze na shughuli nyengine.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja hoja hii na namtakia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aje kutoa maelezo ili baadae na kuwatambua Waheshimiwa Wajumbe Baraza hili, ili baadae Wajumbe hawa watupitishie tuweze kwenda kuwatumikia wananchi tushirikiane kujenga nchi yetu kwa maendeleo yetu kwa pamoja.

Mhe. Spika, nakushukuru na Waheshimiwa Wajumbe nakushukurini ahsanteni sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Waheshimiwa Makatibu wangu wanashangaa hapa hukutoa hoja. Lakini wamesahau kwamba mtoa hoja mwenyewe atakuja yeye ndiye atakayetoa hoja.

Sasa kabla sijamwita, Waheshimiwa labda nitanabahishe tu nimekuwa napokea vibarua vingi sana kutoka kwa Waheshimiwa hasa wanaotokea Pemba wakiomba ruhusa kwa kipindi hichi kwenye ziara ya Makamu wa Pili wa Rais kesho Pemba. Lakini sasa nimeanza kuwa na wasi wasi kwa sababu kila mmoja analeta kwa wakati wake na wako ambao nimewaruhusu mapema leo asubuhi kwamba waende. Lakini sasa naona mshakuwa wengi karibu nyote mnaotokea Pemba mnataka muwepo Pemba kesho.

Sasa nina wasi wasi kuruhusu watu wote wasiwepo kwa maana ya kuja kusimamisha shughuli zetu za Baraza kwa kukosa *quorum*.

Kwa sababu kesho ni Ijumaa nadhani kuna Jumamosi na Jumapili ambazo mngeweza kuzitumia hizo. Lakini kesho mkashiriki hapa mkaendelea hizi shughuli za serikali na baada ya hapo tena Jumamosi mkaenda mkashiriki katika ziara au kwenye majimbo yenu kwa sababu ya dharura iliyopo inaeleweka na umuhimu wake wa kuweko kule nyinyi pia unafahamika. Lakini ningekuombeni sana kwa kesho tukae pamoja hapa tumalize hizi shughuli baada ya hapo kama wapo watakaowahi kuondoka jioni au siku ya Jumamosi asubuhi basi muende mkafanye zile shughuli kwenye majimbo yenu.

Baada ya maelezo hayo machache sasa naomba nikuite Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ili uje uhitimishe hii hoja, karibu sana. (*Makofi*).

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, na mimi nianze kama walivyoanza wenzangu walionitangulia kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaali uhai na uzima mpaka leo kuanzia jana tulipoanza Baraza letu hili.

Lakini pia na mimi niungane na wenzangu kutoa tena pole zangu za dhati kabisa kwa maafa yaliyotokea kule Arusha na vile vile kwa athari zilizotokea kwa wenzetu wa Unguja na Pemba kutokana na mvua kubwa zilizonyesha na zinazoendelea kunyesha, tunawapa pole sana na *inshaallah* serikali itajitahidi kuhakikisha kwamba inatoa kila msaada kwa wale wote walioathirika na mvua hizi.

Mhe. Spika, pia niwashukuru Wajumbe wote waliochangia hoja ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, wamechangia vizuri wametupa muelekeo wametupa changamoto na naamini kabisa michango yao yote walioitoa kwa namna tofauti ililenga kuisaidia Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kufanya kazi zake kwa ufanisi. Niwahakikishie kwamba yale yote waliyoyachangia waliyotuelekeza, waliotukosoa tutayafanyia kazi ili kazi zetu katika Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ziende vizuri zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mhe. Spika, kwanza niwatambue basi wale wote waliochangia hoja ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

1. Mhe. Omar Seif Abeid
2. Mhe. Shehe Hamad Mattar
3. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
4. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
5. Mhe. Saada Ramadhan Mwenda
6. Mhe. Simai Mohammed Said
7. Mhe. Suleiman Sarahan Said
8. Mhe. Mussa Foum Mussa
9. Mhe. Mwantatu Baraka Khamis
10. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
11. Mhe. Mohamed Mgaza Jecha
12. Mhe. Nassor Salum Ali
13. Mhe. Suleiman Mohd Ali
14. Mhe. Rashid Makame Shamsi
15. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
16. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
17. Mhe. Miraji Khamis Mussa
18. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
19. Mhe. Ussi Yahya Haji
20. Mhe. Ali Suleman Ali
21. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
22. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango
23. Mhe. Mwanasheria Mkuu
24. Mhe. Naibu Waziri Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ...
25. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Mhe. Spika, hawa walichangia kwa kusema. Sasa nawataja waliochangia kwa maandishi.

1. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo
2. Mhe. Shaib Said Ali
3. Mhe. Panya Ali Abdalla
4. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
5. Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame Mwadini
6. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ
7. Mhe. Naibu Waziri wa Afya

8. Mhe. Said Omar Said
9. Mhe. Ussi Yahya Haji
10. Mhe. Asha Abdalla Mussa
11. Mhe. Ali Khamis Bakar
12. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
13. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
14. Mhe. Zaina Abdalla Salum
15. Mhe. Mussa Ali Mussa
16. Mhe. Hidaya Ali Makame na
17. Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo

Mhe. Spika, wote hawa nawashukuru kwa michango yao na kwa ufafanuzi waliotoa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri kwa ufafanuzi waliotoa juu ya mambo mbali mbali ambayo yalichangiwa katika kikao hiki.

Mhe. Spika, kuna suala zima la uwezo wa Zanzibar kuchimba mafuta. Suala hili limeshaelezwa na Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kirefu sana, sina haja ya kulirejea. Lakini mimi niseme tu kwamba kwa sababu ya nia nzuri waliyonayo wenzetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Mwaka 2015 nakumbuka Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete alimpigia simu Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein na kumwambia kwamba nataka tulimalize suala la mafuta na gesi asilia kabla sijaondoka madarakani. Kwa hivyo naomba tutunge sheria tuipeleke Bungeni ili kutoa nafasi kwa Zanzibar kushughulikia suala la mafuta na gesi asilia yake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, na ninakumbuka vizuri sana kwamba wakati huo Mhe. Mwanasheria wetu alikuwa safarini Uholanzi, akaitwa aende Dar es Salaam kuungana na Mhe. Mwanasheria Mkuu mwenzake, ili kuandaa hiyo Sheria ambayo itapelekwa Bungeni itungwe na ipitishwe na Bunge kutoa sasa nafasi kwa Zanzibar kushughulikia mafuta na gesi asilia, hata kabla ya hiyo Katiba mpya haijapitishwa. Kwa sababu hiyo ndio Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikapata nguvu ya kutengeneza sheria yake ambapo humu ndani tumeipitisha sisi.

Kwa hivyo sisi Zanzibar tuna nguvu na ndio maana tumeanza sasa hivi *study* ya kuona hivi kiasi gani tuna mafuta, kiasi gani tuna gesi. Wenzetu wa Ras Al Khaima wanaendesha shughuli hiyo ili baadae ndio tutajua kiasi gani cha mafuta na gesi asilia tulikuwa nayo hapa Zanzibar. Kwa hivyo tusiwe na hofu tuko pazuri kuliko tulivyokuwa huko mwanzo. Huko mwanzo hata kusema

kulitaja mafuta na gesi asilia tulikuwa hatuwezi, kwa sababu ilikuwa ni jambo la Muungano. Sasa hivi sio la Muungano tena, tungojee tu wakati ufike ipitishwe Katiba mpya, *automatically* suala hili litakuwa halipo katika orodha ya mambo ya Muungano. Kwa hivyo tusiogope tusiwe na wasi wasi tusiulize maswali mengi kuhusu suala zima la mafuta na gesi asilia, ni mali yetu. Tunaweza kuchimba hata leo kama ipo na makampuni yameshaanza kuomba kuja kuwekeza katika mradi huu. Kwa hivyo tusiogope wala tusiwe na wasi wasi. Lakini kama nilivyosema suala hili limeelezwa sana na Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, jengine lililoulizwa na Mhe. Omar Seif Abeid ni kwamba serikali haitilii uzito suala la kutatua hoja za Muungano. Serikali hizi mbili zimefanya jitihada kubwa, tunayo kamati ya SMT na SMZ kutatua matatizo ya Muungano. Tumefanya mengi katika kamati hii na leo yamebakia mambo machache sana, isipokuwa kuna mambo madogo madogo tu ndio tunayafanyia kazi kwa kushirikiana na pande mbili za Muungano. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sio kweli kwamba serikali hii haitilii uzito kwa hatua za hoja za Muungano. Kwa kupitia vikao vya kisekta na hivi sasa pande mbili za Muungano zinashirikiana sana. Sasa hivi Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa amealikwa kwenda mahali, na akiwa hana nafasi basi anampigia mwenzake wa huku akamwakilishe. Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amealikwa kwenda mahali kwenye mkutano fulani, ikiwa hawezi kwenda basi anamwambia Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein akamwakilishe. Hii inaonesha namna gani sasa hivi tuko karibu zaidi katika utekelezaji wa shughuli zetu kama Watanzania. Kwa hivyo mimi nimuhakikishia Mhe. Omar Seif Abeid kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inajitahidi mara kwa mara kuhakikisha kwamba mambo yote ya kero za Muungano zinatatuliwa.

Mhe. Spika, pia kuna suala la Mhe. Simai Mohamed Said ambaye alisema viongozi wa Kimataifa hawafiki Zanzibar wanapotembelea Tanzania, wanaishia Dar es Salaam. Ni kweli na hili tumekuwa tukilipigia kelele sana na tukizungumza na wenzetu kwamba jambo hili sio jambo tulioachiwa na waasisi wetu.

Mhe. Spika, waasisi wetu baada tu ya Muungano ilikuwa wakija tu wageni kama Marais, nakumbuka kabisa Rais Nyerere alikuwa anafuatana na mgeni kuja naye hapa, haya ndio yalikuwa yanafanywa na waasisi wetu ndio waliotuachia. Lakini sasa hivi kwa sababu ya shughuli nyingi, huko nyuma Marais walikuwa wanapewa Mawaziri kuwaleta Zanzibar kufanya ziara rasmi,

hata kwa siku moja. Lakini ni kweli kwamba kwa muda mrefu kidogo kitu hiki hakifanyiki na tumekuwa tukikipigia kelele sana na wenzetu.

Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein mwenyewe alizungumza kwa muda mrefu na Naibu wa Mambo ya Nje juu ya suala hili na masuala mengine. Mimi mwenyewe nilizungumza sana na Waziri wa Mambo ya Nje juu ya suala hili na bado naendelea kuzungumza naye kwamba utamaduni tulioachiwa na waasisi wetu ni kwamba Rais mgeni anapotembelea Tanzania ni lazima aje na Zanzibar ndio Tanzania yenyewe. Isipokuwa na mimi hili nina uzoefu nalo, nilipokuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje.

Mhe. Spika, kuna mara moja alikuja Rais wa China kutembelea Tanzania, tukatengeneza ratiba, ratiba ile iliingiza na ziara ya Zanzibar. Tulipompelekea balozi wa China akaipeleka kwao. Jibu lililotoka kwao akawaambia waambie kwamba Rais hatoweza kwenda Zanzibar kwa sababu ya muda. Nikamwita tena Balozi wa China, nikamwambia bwana tafadhali sana wanasihi Serikali yako Rais huyo anayekuja aende Zanzibar la sivyo itatuletea matatizo ya kisiasa.

Mhe. Spika, akasema basi napeleka tena taarifa, akapeleka tena taarifa kwao. Jibu likaja lile lile kwamba Rais hatoweza kuja Zanzibar kwa sababu ya muda mfupi, isipokuwa anamkaribisha Rais wa Zanzibar aende Dar es Salaam kwenda kukutana naye na kwenda kufanya mazungumzo. Sasa ndio nikasema isipokuwa mgeni mwenyewe ana-*resist* kuja, kwa sababu yoyote, kwa sababu ya muda mfupi au kwa sababu nyengine yoyote. Kama si hivyo hakuna sababu nyengine yoyote kwa nini mgeni yule asije Zanzibar.

Mhe. Spika, leo kwa mfano kuna Rais wa Afrika ya Kusini yuko Dar es Salaam, inawezekana ziko sababu kwa nini hawezi kuja Zanzibar, inawezekana na yeye vile vile muda anaona mfupi. Lakini sasa huwezi kumbishia mgeni wako ukamwambia lazima lazima, hiyo sio demokrasia. Mnazungumza mnafika pahala mnaelewana basi, unamuachia na maamuzi yake. Lakini hili kama nilivyosema tunalipigia kelele sana. Rais mwenyewe Dk. Ali Mohammed Shein ameshalizungumza na Rais John Pombe Magufuli mwenyewe. Kwa hivyo, hili tunalishughulikia, msifikirie kwamba serikali imekaa kimya hapana na sisi hili kidogo linatukereketa kwa sababu tunaacha ule utamaduni ambao waasisi wetu walituachia.

Mhe. Spika, kuhusu suala la wafanyabiashara ambalo limeletwa na Mhe. Omar Seif Abeid, Mhe. Waziri wa Fedha kishalijibu vizuri tu na sina jengine tena la kuongeza. Lakini Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Spika,

Mhe. Simai Mohamed Said na Mhe. Hassan Khamis Hafidh wamenialika kutembelea kwenye majimbo yao. Natamka mbele yako Mhe. Spika, kwamba nimekubali. Zikimalizika mvua nitakwenda kutembelea kwenye majimbo yao wala hilo halina tatizo kwa sababu ni sehemu ya kazi yangu. *(Makofi)*

Lakini vile vile Mhe. Spika, nilitaka nirudie kusema yale ambayo aliyasema Mhe. Mohammed Aboud Mohammed Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Juzi tulipokutana kwenye *caucus* tulielezana juu ya nidhamu ya ndani ya Baraza hili. Hiki ni chombo kikubwa lazima tukiheshimu na tuwaheshimu viongozi waliomo ndani ya chombo hiki, lugha zetu tuzichunge na midomo yetu.

Mhe. Spika, niseme kweli kwamba jana Mhe. Nadir Abdul-latif hakuwa mstaarabu, alisema maneno ya ovyo sana. Yaani kusema haogopi chochote, hata akifukuzwa. Sio lugha nzuri ile, ni lazima tuchunge midomo yetu tukiwa humu ndani. Tukisema huko nje sawa lakini tukiwa humu ndani lazima tuchunge, watu wengi wanatuona na wengi wanatusikia, tukianza kusema maneno ya kutoheshimu wenzako kuna sababu gani wewe kuitwa mheshimiwa na watu wataanza kukufikiria hivi kweli huyu mwana CCM, kwa sababu sio kawaida mwana CCM kutomuheshimu mwana CCM mwenzake. Kwa hivyo mimi Mhe. Spika, nasisitiza sana ni lazima tuchunge midomo yetu tukiwa humu ndani, kama si hivyo watu watatufikiria vyengine.

Mhe. Spika, mengi yamesemwa na wenzangu waliozungumza wameelezea mengi. Limezungumzwa sana humu ndani suala la *diplomatic passport* na Mhe. Nadir Abdul-latif ameniambia nikija hapa nimuhakikishie kwamba nijitahidi *passport* zipatikane. Namjibu kwamba sijitahidi kwa sababu uamuzi wa serikali umeshatolewa siwezi kwenda kinyume na uamuzi wa serikali. Hilo moja.

Lakini la pili sioni kwamba suala la *diplomatic passport* kama lina tija. Mtu akiwa na *diplomatic passport* atasafiri na aliyekuwa na passport atasafiri. Ukiwa na *diplomatic passport* huongezewi na ukiwa na *diplomatic passport* hupunguziwi. Kwa hivyo hili niseme wazi Mhe. Spika, silifanyii kazi maana sioni kama lina tija, siwezi kwenda kinyume na maamuzi ya serikali, tena kutoka ngazi ya juu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa nawaomba Wajumbe wenzangu waiunge mkono hotuba ya bajeti hii, ili tuweze kwenda kutekeleza majukumu yetu kama ilivyo kawaida na kama tunavyotegemea tukafanye kazi zetu. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imepewa jukumu kubwa kushughulikia madawa ya kulevya, walemavu na kadhalika na watu wenye Ukimwi, kwa hivyo tuna

kazi kubwa. Lakini bila ya kupitishiwa bajeti yetu hii utekelezaji wa kazi hizi utakuwa ngumu. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Spika, Wawakilishi wenzangu wapitishe bajeti hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili tuweze kwenda kufanya kazi zetu vizuri.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Umetumia dakika 20 juu ya alama kwa maelezo yako.

Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa naomba hoja iamuliwe, naomba niwahoji wale wote wanaokubaliana kwamba tupitishe bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wanyanyuwe mikono yao. Wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe kabla ya hatua inayofuata sasa hivi na kabla sijamwita Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili tuweze kwenda kwenye hatua inayofuata ya kuingia kwenye kamati, naomba nimuombe yeye Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa sababu ya muda tulionao, ili atutengulie ile Kanuni ya Muda tuziendeshe hizi shughuli mpaka tutakapofikia mwisho.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tafadhali.

KUWEKA KANDO KANUNI YA MUDA

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa muda uliobaki mbele yetu hautoshi kukamilisha shughuli za kuendelea na kupitisha bajeti hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kwa hivyo naliomba Baraza lako tukufu iweke Kanuni ya Muda kando ili tuweze kumaliza shughuli zetu hizi kama zilivyopangwa katika *order paper*. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe hoja iliyopo mbele yetu ni ya kutengua kando Kanuni ya Muda. Sasa naomba niwahoji wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Kwa hatua hiyo sasa namuomba Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa hatua inayofuata tafadhali.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Naomba sasa Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi vya Wizara ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Naomba kuwasilisha.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU C 01 - AFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Kifungu C0104 Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa 32,521,000
Jumla ya mapato **32.521,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU C 01 - AFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Kifungu PC0101 Program Kuu ya Uratibu wa Shughuli za Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais
Kifungu SC010101 Program ndogo za uratibu wa shughuli za Makamo wa Pili wa Rais 1,024,217,000

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipati nafasi katika mchango wangu pamoja na ufafanuzi wa kina uliotolewa na Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais bado nimekamata shilingi katika ukurasa ule wa 15 na nina sababu zangu za kusema hivyo. Hichi kitabu nilichochukua hapa ni Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Sasa kuna mambo yamefanyika mengi sana pamoja na wachangiaji wamechangia kwa muono wao humu, demokrasia kila mtu anasema vile anavyoona yeye.

Kuna mambo yaliyofanyika asilimia kubwa sana. Je, ni pesa za kwake kama mfuko wa jimbo. Je, ni pesa ambazo yeye mwenyewe tu katunukia wananchi wake na kama pesa zile haikupaswa kuingia humu, kwa sababu hichi ni kitabu chenye bajeti ya Wizara au Afisi. Sasa nataka ufafanuzi zaidi hapo ili niweze kufahamu ijapo kwamba nilikuwa sijafahamika lakini nataka ufafanuzi zaidi katika hicho. Ingekuwa ni za kwake yeye *private* basi angefanya kimya kimya

tukajua tu anafanya na zaidi ya hizo pengine hata zaidi ya hizo alizofanya. Lakini kinapokuja humu hichi kitabu ni cha Makadirio ya bajeti ya Taasisi, Serikali ambayo yeye anaisimamia. Naomba ufafanuzi zaidi kwa kina zaidi ili niweze kufahamu.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, tizama hoja anayosema Mheshimiwa ya ukurasa wa 15 *paragraph* ya 8, utaona imeeleza kama lengo na utekelezaji wa kazi za kawaida na miradi ya maendeleo kwa kipindi cha miezi 9 Julai, March, 2016/2017. Bajeti tunayozungumzia hapa 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, hili jambo lilikuwa linaelezwa kwamba ni ahadi kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alizozitekeleza kwa upande wa jimbo lake. Pia imeoneshwa hapa, yaani kutoa pesa zake sio pesa za Serikali hatujaziombea fedha hapa. Haya ni maelezo ya ahadi alizotekeleza haihusiani na bajeti ya 2017/2018. Kwa hivyo unatuzuiaje hapo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Spika: Ameridhika tunaendelea.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Kwa kweli kaeleza lakini mimi bado sijamfahamu. Mimi Abdalla Diwani Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe bado sijamfahamu. Naomba ufafanuzi zaidi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuongezea maelezo aliyotoa Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kwa hoja ya Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwamba kilichoelezwa hapa ni utekelezaji wa ahadi na hakina mahusiano na matumizi ya fedha.

Hivyo hivyo kama Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atafanya safari nje ya nchi au mahali pengine popote pengine, iwe safari iliyodhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania humu itaripotiwa, lakini fedha si kwamba zimetoka kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hivyo hivyo kwa utekelezaji wa ahadi hizi Mheshimiwa akubali kwamba iliwekwa hapa kama ni utekelezaji lakini sio matumizi ya fedha za SMZ.

Mhe. Spika: Mhe. Abdalla Maulid Diwani nafikiri umefahamu vizuri.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Sasa hivi nashukuru Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo ya Dokta nimemfahamu naomba tuendelee.

Mhe. Spika: Ahsante tunashukuru Mhe. Suleiman Makame Ali.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Mwenyekiti, sipo kwenye kukwaza sana na wala sina buti kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti mimi nataka kujua kwa sababu ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais aliahidi kompyuta mbili kule Ndagoni na *printer* moja. Je, nikitaka kujua kwenye kifungu hichi ahadi hii itakamilishwa.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mheshimiwa ndio hayo hayo anayosema Mhe. Abdalla Maulid Diwani, kwa kuwa haya ni maelezo tu yaliyotolewa na humu hata hayo maelezo ya kompyuta mbili na *printer* moja hayamo. Sasa utayatekelezaje hapa ndio hayo tunayoyasema kama ni ahadi binafsi ya Mhe. Mohammed Aboud, haihusiani na utekelezaji wa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mwenyezi Mungu akimjaalia uwezo wa kupata fedha za kununua kompyuta mbili na *printer* moja atafanya hivyo na atazipeleka jimboni. Lakini namuomba kwa sababu Mhe. Mwakilishi ndugu yangu na kwa sababu najua hali yake kwa sasa ni nzuri angetoa hizo fedha akaninunulia kompyuta mbili na *printer* moja, na mimi namhakikishia nitamrudishia pesa zake hizo kabla ya kwisha mwaka huu.

Ahsante sana Mheshimiwa *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante tunaendelea

Jumla **1,024,217,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Kifungu PC 0102 Program kuu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali
Kifungu SC 010201P Program ndogo ya kukabiliana na maafa 1,506,233,000

Mhe. Hassan Khamis Khafidh: Ahsante sana Mhe. Spika, nilipokuwa nikichangia nilisema kwamba Idara ya Maafa inafanya kazi nzuri nashukuru sana…..

Mhe. Spika, Kuwa *brief* kidogo usihutubie.

Mhe. Hassan Khamis Khafidh: Inafanya kazi nzuri nashukuru sana lakini niliuliza ina mkakati gani kwa sababu ina subiri kukabiliana na maafa, ina mkakati gani wa kuya-*protect* na kuya- *prevent* maafa yasitokezee Zanzibar na nikatoa mifano mbali mbali. Katika kujibiwa ina mkakati gani kwa sababu nilisema imekaa kama mchimba makaburi inasubiri maafa lakini lazima iwe na mkakati wa kuyalinda na kuyafanya yasitokee.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ahsante nakushukuru sana na pia nimshukuru ndugu yangu Mhe. Hassan Khamis Hafidh, nadhani katika maelezo ambayo Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango alieleza tangu mawasiliano katika kukabiliana na maafa, mipango hiyo haikuishia kwenye kiwango cha taifa. Ndio maana kuna mpaka vitabu vya kwenye Wilaya. Lakini kama nilivyosema mimi kwamba tatizo la msingi ni uwezo wa kuikamilisha hiyo mipango na mikakati mengine. Kuna mengine ya muda mfupi, mengine ya muda wa kati na mengine ya muda mrefu. Lakini tungependa tuyafanye yote kwa wakati mmoja, lakini kuna mengine yanahitaji fedha nyingi, kuna mengine yanafanyika sasa hatua kwa hatua.

Kwa hivyo mkakati wetu mkubwa kwa haya mambo ambayo unaona yanafanyika, mipango mbali mbali ya elimu kwa umma inafanyika kuanzisha Kamati za Maafa kuanzia Shehia, Wilaya mpaka Taifa ndio mipango yenyewe ya kukabiliana na maafa. Na hizi Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa si watekelezaji wa moja kwa moja, ziko nchi duniani Kitengo hicho kinakuwa na mambo yote kwa pamoja. Lakini sisi tunafanya kwa mashirikiano. Kwa hivyo taasisi moja baada ya nyengine zina wajibu katika utekelezaji.

Kwa mfano uokozi wana wajibu wao wakati wanapotokea kufanya shughuli za uokozi, KMKM ikitokea ajali baharini wanafanya wajibu wao katika kuokoa, *ZMA* wanafanya wajibu wao pale ambapo mambo yanapotokea katika usafiri wa baharini. Kila mmoja kisekta ana wajibu wake na mipango inapangwa. Katika hizi bajeti zetu tunazozipanga kila mwaka iko mipango mle ndani yake inayowezesha utekelezaji wa kukabiliana na maafa. Kwa hivyo kuna mipango ya muda mfupi, muda mrefu na muda wa kati, imetekelezwa vizuri na imeandikwa vizuri kwa maandishi. Upo mpango wa mawasiliano, upo mpango mkakati kwa kila hatua inaonesha katika kitabu.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Waziri na nampenda sana lakini nafikiri hakufahamu suala. Najua Idara ya Maafa inafanya vizuri kweli kweli kukabiliana na maafa, Wallahi ninajua.

Mimi hoja yangu wana mkakati gani kuyalinda maafa yasitokezee Zanzibar yasitokezee Zanzibar…….

Mhe. Spika: Mheshimiwa hata mimi nimekufahamu lakini naona kama tunajipa sijui niseme vipi ni mambo ya Mwenyezi Mungu haya. Mambo yanapotokezea tusiwapeke huko wenzetu mheshimiwa, gharka zinatokea sehemu mbali mbali, vimbunga vinatokezea ni mambo ambayo hawezi kuya-*control* kama Serikali.

Lakini maelezo ambayo aliyatoa Mhe. Waziri wa Fedha kama ulimsikiliza vizuri wakati anatoa mchango wake yalikuwa mazuri sana yangekutosha.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nakubali lakini Wahenga wamesema, "Kinga bora kuliko tiba".

Mhe. Mwenyekiti, nakusudia kusema hivi hakuna asiyejua pale Mwanakwerekwe kama pamejengwa, maji hayaendi. Ndio hoja yangu iliko watu wamejenga maji hayaendi hayana pa kupita, hakuna asiyejua kule Welezo kuna mito, watu wameruhusiwa wamejenga maji hayendi hayana pa kupita. Ndio hoja yangu iliko ndio kulinda yenyewe huko.

Mhe. Spika: Sasa hivi limekaa vizuri zaidi kuliko pale mwanzo suala lako.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mheshimiwa kama nilimsikiliza vizuri Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango alipokuwa akitaja ile mipango na mikakati akaeleza *ZUSP* awamu ya pili namna ambavyo wamejipanga kuyandosha maji kutoka katika lile bwawa la Mwanakwerekwe kuja Sebleni, likashuka mpaka Kwa Pweza mpaka likashuka chini huku kuja baharini. Kwa hivyo alieleza vizuri namna ya kuyaondosha maji yale pale. Na lile linatokana na uchimbaji wa mchanga wa miaka mingi ndio matokeo ya pale. Lakini hata hivyo Serikali imeunda timu ya wataalamu kufanya tathmini ya kina kuona namna gani hatua nyengine zitakazosaidia, lakini wa mwanzo ni huu mradi wa *ZUSP* ambao maji yale yataondoshwa.

Si vizuri kwa kufanya maamuzi kusema zile nyumba zilizojengwa pale ndio sababu pekee, zipo sababu hizo zinazoonesha kama ujenzi wa *petrol station* pale na mwengine unasababishwa kwa kiasi fulani kutuwama kwa maji hayo. Lakini ukweli pale lipo shimo na maji yapo hata ukivunja bado lile shimo litaingia maji, njia nyepesi ambayo wataalamu wetu wametushauri na huu mradi wa *ZUSP* yale maji yatoke pale yafike mpaka baharini ndio uzuri.

Mhe. Spika: Mhe. Hassan Khamis Hafidh nadhani utakuwa umeridhika sana.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Amejitahidi kujaribu kujibu naomba tuendelee.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi langu litakuwa ni dogo tu. Kwanza nimshukuru Waziri ametoa maelezo mengi kuhusu kwamba Idara ni mpya na katika kujenga na masuala ya raslimali na vitu vyote. Lakini pia natambua na nikatoa wazo kwamba kwa hili nataka nifuate kauli yake na kauli ya Serikali kwamba suala la kutumia *message* kuwapelekea wananchi, hasa hawa wavuvi wetu kwa kutumia makampuni ya simu ili kuwapa angalau utabiri wa hali ya hewa. Kitu ambacho tayari tunakuwa tumeshajua ili wale wenzetu wapate kufahamu kwa kutumia hizi *messages* kwa kutumia makampuni ya simu. Sasa nataka kujua kauli je, wazo hili watalifanyia kazi.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti jambo lote la kheri na jema kwa wananchi wetu. Kama nilivyosema awali michango hii inasaidia sana michango inayotolewa na Waheshimiwa Wajumbe hapa katika utekelezaji wa majukumu yetu. Kwa hivyo jambo zuri kama hilo tutawasiliana na wenzetu. Kwa sababu kama tunawatumia wenzetu wa hali ya hewa kwa nini tusiwatumie na wenzetu wengine wote watakaosaidia kulinda maisha ya watu wetu.

Jambo la msingi sana kwa sababu hayo matatizo yakitokea hujui yatamkuta nani na wakati gani. Sote yanaweza kutukuta wakati wowote. Mwenyezi Mungu atupishie mbali atunusuru lakini ni jambo ambalo lipo na linaweza kutokea wakati wowote. Kwa hivyo ushauri tunaupokea Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nina masuala yangu niliyouliza lakini kwa kweli sijajibiwa, zaidi ya kujibiwa madongo na *message send*.

Lakini ninachoomba kusema kwamba nilizungumza ni lini kwa kuwa mafuriko yanatokezea kila mwaka zaidi wakati wa mvua Unguja a Pemba, watajenga maeneo ya wanawake na wanaume ya kuwahifadhi, wengine wanao jamaa, wengine hawana jamaa wanakwenda kukaa wapi sijajibiwa.

Nikazungumza vile vile wanaopata mafuriko wanawahifadhi kwenye maskuli, skuli ndio wanaokwenda kuwaweka, wanawaweka kama watu wa kipindupindu na watu wengine ambao wanaopata mafuriko sijajibiwa. Lakini Makombora tumejibiwa yale ya muhimu hatujajibiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nalazimika kutokuruhusu hata kujibiwa hata hili ambalo unahoji sasa hivi na utakuwa umechukua hata mpaka hiyo nafasi. Sababu ningeweza kumpa mtu mwengine akaleta jambo hapa tukaleta, kwani ukihoji kwa lugha ya kistaarabu kuna tatizo gani? Bila ya kuwa na hasira taratibu tu, Mhe. Waziri niliuliza kuhusiana na jambo la kuhifadhi watu kwenye maskuli bila ya kuwa na hasira, yaani *message* itakuwa imefika vizuri zaidi, kuliko ukionesha kwamba uko kwenye hasira.*(Makofi)*

Waheshimiwa, haya mnayoyahoji hapa, mnahoji kwa niaba ya wananchi na ndio waliokutumeni. Lakini sidhani kama wamekutumeni kwamba mtumie lugha ambazo haziko sahihi katika kuleta hoja zenu, leteni kwa lugha za kistaarabu kidogo, tumia lugha nzuri tu. Kwa hivyo hili nalikataa na nina kihoji hiki kifungu kinakubaliwa? *(Makofi).*

Wajumbe: Ndio.

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee. *(Makofi)*

Kifungu SC 010202	Programu Ndogo ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi	
	Viongozi wa Kitaifa	1,081,976,000
Kifungu SC 010203	Programu Ndogo ya Shughuli za SMZ, SMT Utafiti na Masuala ya Muungano	

Mhe. Abdalla Maulidi Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, katika maelezo yangu wakati nachangia hotuba hii nilikopi bajeti iliyopita kwenye suala zima la utafiti katika eneo langu la shimo pale Jang'ombe, ilikuwa siku ya Jumatatu tarehe 30/05/2016 mwaka mmoja uliopita nilizungumza hapa hapa.

Lakini Mhe. Waziri akanipa majibu mazuri tu yale ya kunilainisha na bado nilikuwa ndio kwanza najifunza kwa kuwa kidogo nimeanza kuelewa. Naiomba tena sana narejea pale pale, kwa hili swali langu la Jang'ombe Mhe. Mwenyekiti, limefikia wapi? Anijibu vizuri ili na mimi kuridhia kwa upole kabisa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili la Rais: Mhe. Mwenyekiti, mimi napata tabu kidogo suala la Mhe. Abdalla Maulid Diwani kuanzia suala la utafiti, SMZ, SMT na masuala ya Muungano na Jang'ombe kidogo na amekusudia utafiti vipi. Lakini kama nimemuelewa ni kufanya utafiti kwa

namna ya kutokea ile kubomokeza kwa ardhi, kwa baadhi ya maeneo ya Jang'ombe kama kakusudia jambo hili.

Sasa hapa kilichofanyika ni kuundwa ile Kamati ya wataalamu, na kutoa ushauri gani kwa utaratibu mzima kwa namna ambavyo maji yanakaa chini kwa chini na kuona vipi athari yake. Na moja katika kutatua athari hizo ni huu mradi wa *ZUSP* kwa upande wa Jang'ombe umesaidia ule mtaro unaotokea kwa Binti Hamrani na ule mtaro uliotoka Mnazi Mmoja.

Nadhani kwa upande mwengine na ule mtaro alioeleza Waziri wa Fedha na Mipango hapa unaotokea Kariakoo kuelekea Kilimani mpaka baharini. Na tunadhani itasaidia zaidi katika mtaro huo mwengine wa kuondosha maji ya Mwanakwerekwe. Suala hapa ni namna ambavyo tumejenga nyumba zetu na njia za maji zile tukazizuiya. Matokeo yake ndio yamesababisha kutuwama kwa maji.

Hili jambo la muda mrefu la miaka mingi, tunachokifanya katika awamu hii ni kutafuta namna gani tunaondosha maji hayo na kuweka utaratibu ulio bora zaidi. Ndio maana Serikali kila wakati inatoa matangazo ya wananchi kutokujenga katika njia za kupita maji, kujenga mabondeni na kadhalika. Kwa hivyo hilo ni jambo letu kwa pamoja Wawakilishi tusaidie katika kuwaelimisha wananchi katika maeneo yao. Serikali haipendi na wananchi wengine waathirike katika ujenzi, lakini sasa ujenzi umetokea ndio maana maji yamekwama, ndio hali halisi inavyoonesha.

Mhe. Abdalla Maulidi Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi swali langu sikulizungumzia juu ya ujengaji wa mitaro Jang'ombe. Nimezungumzia utafiti yaani ufunguzi. Pale pashazama nyumba, pashazama Msikiti, pashazama mnazi, pashazama nyumba tena. Sijazungumzia mtaro kuondosha maji, kitu tofauti nilichokizungumza mimi na Mhe. Waziri.

Kidogo Kiswahili chetu nafikiri kiko tofauti. Mimi nazungumzia Kiswahili cha mjini zaidi mwenzangu anazungumzia cha Wawi. Mimi nimezungumza utafiti ni upi uliofanyika kuona kadhia ile pale ya kuzama. Je, kama kule chini kula ghuba, ardhi iko wazi, panapobomokea tukachunguze. Sijazungumza suala la maji kuondoshwa. Sasa naomba Mhe....,

Mhe. Mwenyekiti: Lishafahamika Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili la Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Sheikh Abdalla ni mtoto wa mjini wana mambo mengi, mimi ni mshamba wa Wawi.

Lakini kwenye suala moja nililieleza wale wataalamu ndio wanaofanya utafiti na katika utafiti wa awali ndio uliosaidia kufikia maamuzi ya kujenga hiyo mitaro ili kusaidia kuondoa maji na vyovyote si jambo jepesi. Hivyo wataalamu wetu wanaendelea kufanya utafiti zaidi tuone kama kuna sababu nyengine zaidi. Lakini kwa sasa suala kubwa ni lile kwamba tunaloelewa maji haya yametokana na kutuwama. Kwa msingi huo ndio ardhi inabomokeza.

Mimi Kiswahili changu cha Kipemba kidogo, kinabomokeza inakufanya pafanye chimo nyumba ididimie au ibonyee, yote haya yanatokea. Kwa hivyo nadhani Sheikh Abdalla atanifahamu.

Kwa hivyo kwa ufupi Mhe. Mwenyekiti, timu yetu inaendelea kufanya kazi hiyo na hiyo kazi ya awali walioifanya ndio inayosaidia kujenga mitaro, kwa kiasi fulani pale ambapo panapojengwa mitaro unafuu unapatikana. Naamini pia tukiondosha tatizo la Mwanakwerekwe basi pia tutaweza. Kama nilivyosema kwamba mambo haya ya kupambana na kukubaliana na maafa ni miradi mikubwa inayohitaji fedha nyingi, si suala jepesi. Maana miundo mbinu yake inahitaji fedha nyingi katika kutengeneza.

Hata mtandao wa maji katika kupambana na maradhi haya ya miripuko umesikia tumepata karibu milioni 92 kwa Mkoa wa Mjini/Magharibi. Dola milioni 92 wenzetu wa India tunasaidiana nao katika kuongezea jitihada zetu kwa Mkoa wa Mjini/Magharibi peke yake. Mamilioni ya fedha yashatumika kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa hivyo si jambo jepesi sana. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, sasa nitakwenda hivyo unavyotaka wewe kidogo dogo. Mimi nilizungumzia suala kweli la Polisi lakini ninachotaka nijibiwe hivi wanavyofanya Polisi kupiga watu mikwaju njiani, kupiga waya wa umeme mtu anayetembea na vespa au honda, wanampiga waya wa umeme, wengine wanakunja watu mashati, wengine wanawavamia boda boda na kuwawekea gari mbele. Kama ni jambazi wakati wao kumbe wanataka *road licence,* hajabibu hatua gani watachukuliwa. Hivyo wanachofanya nini kitaendeleka lakini kajibiwa Nadir.

Mimi nilichosema akija kunipiga mkwaju, akija akinipiga waya hapo sitokubaliana naye kwa sababu vile atakuwa keshaniumiza na kuna Polisi amesha uwa pale Kilimani, kamsukuma mtu na pikipiki miaka ya nyuma, kuna Polisi washapiga watu washawavunja mikono humu humu. Lakini nikija kufanyiwa mimi kwa suala kama hili la kupigwa njiani nimesema hapa sitokubali.

Lakini hapa sitokubali, kuna kisheria na kuna maungoni. Sasa hapo mimi sikutamka kama nitampiga. Sasa nitaomba nijibiwe hatua gani wachukuliwe Polisi wa namna hii na wapo wengi Unguja.

Mhe: Mwenyekiti: Suala la Muungano Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili la Rais: Mhe kwanza napenda twende kwenye vifungu. Kifungu chini Mheshimiwa hakizungumzii Polisi.

Kifungu hichi shughuli za SMT, utafiti na masuala ya Muungano, kuna TASAF 111 na Shughuli za Uratibu wa SMZ. Sasa hapa kuna fedha zinashughulikia kaya maskini haihusiani kabisa na Polisi. Na yeye kama anao ushahidi Polisi wanapiga watu ovyo, upo utaratibu wa kisheria, yeye alichosema atapambana. Mimi nikamwambia si vizuri kupambana na Polisi, fuata taratibu za kisheria, chukua hatua kwa sheria, kuna taratibu za kisheria za utawala na pia za kinidhamu kwa kuona kiongozi unapoona una ushahidi wa mambo hayo.

Hakuna anayetaka apigwe, hakuna anayetaka kuonewa. Hii ni nchi huru, kila mmoja ana haki yake. Mimi namueleweshe lugha nzuri ambayo isimpe yeye matatizo na nikasema Polisi wana utaratibu wao wa kufanya kazi, wana *istrument* yao kisheria. Kwa hivyo ukipambana naye, sijui utapambana nao vipi. Mimi nimemueleza kupambana nao vizuri ni hivi.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al--Wardy: Mhe. Mwenyekti, sijamaliza na mimi Muungano...,

Mhe. Mwenyekiti: Lishakwisha hilo Mheshimiwa. Lishakwisha naomba ukae kwa sababu Mhe. Waziri ameeleza uzuri hilo fungu halihusiani kabisa na Polisi ni kaya maskini. Yaani usingeweza kuleta hoja. Hoja yako huwezi

kuileta kila pahali tu, alimradi watu wamepiga buti wamesimama na wewe upige buti. Usimame ulete tu jambo lako lolote hata kama halihusiani na hapo. Nadhani tumemalizana na wewe Mheshimiwa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Sawa Mhe. Mwenyekiti, hapa kwenye uratibu ndio kwenye kitu kinachoratibiwa na SMZ na tumechangia mambo mengi sana yote hayo kwenye uratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa sio hoja hiyo. Naomba ukae. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Lakini na mimi napenda maelekezo yako Mhe. Mwenyekiti, kwamba hapa ni penye uratibu wa masuala ya muungano. Mimi nina mambo mengi hapa, sijui ndipo pahala pake au pana pengine basi niendelee.

Mhe Mwenyekiti: Naomba moja tu lile mpe Waziri.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, kwenye neno utafiti na utafiti ni kumi na nane katika mambo ya muungano, hasa nimekuwa nikiuliza katika nilivyochangia hapa Zanzibar Ofisi inavyoshughulikia...

Mhe Mwenyekiti: Kidogo ngoja Mheshimiwa. Mhe. Abdalla Diwani ungekaa kimya ili tusikie huku. Tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nauliza hili ni suala la Muungano hapa Zanzibar, Ofisi inayoshughulikia masuala ya utafiti kwa upande wa Zanzibar, ofisi yake iko wapi? Na ina waajiriwa wangapi? Na tafiti gani zimefanywa ziko wapi. Nilitaka kujua hivyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili la Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa maana ya Taasisi ya Muungano iliyoko hapa ni *COSTECH* na iko pale Maruhubi. Ipo Maruhubi pale karibu na Kiwanda cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, wao wapo pale wanashirikiana na Taasisi zetu za Zanzibar, kwa maana ya kushirikiana kwenye masuala ya utafiti. Lakini zipo taasisi mbali mbali kwa maana ya SMZ zinazofanya tafiti. Wizara yetu ya Makamu wa Pili wa Rais inaratibu masuala haya kwa wale wanaotoka nje au hata wa ndani wakiomba tunawapa vibali kwa kuwasiliana na taasisi hizo. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hassan Khamis Hafidh usharidhika.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante tuendelee.

Kifungu SC 010203	Programu Ndogo ya Shughuli za SMZ, SMT Utafiti na Masuala ya Muungano	13,673,209,000

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea ni nafasi tatu tu kwa kila kifungu. Kifungu kinakubaliwa.

Wajumbe: Ndio

Kifungu SC 010204	Programu Ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dar es Salaam	542,930,000
Kifungu SC 010205	Programu Ndogo ya Usimamizi wa Masuala ya Watu Wenye Ulemavu	498,832,000
Jumla Kuu	**Programmu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali**	**17,303,181.000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PC 0103	Programu Kuu ya Usimamizi Shughuli za Upigaji Chapa	2,068,089,000
Kifungu SC 010301	Programu Ndogo Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa	2,068,089,000

Mhe. Abdalla Maulidi Diwani: Ahsante sana Mhe. kwa kulipa fursa hii katika mchango wangu nilichangia sana suala zima la uchapaji na ninilinukuu bajeti iliyopita, tukaona kwamba yale maelezo yaliyoyaomba yale hajatuainishia pamoja na yote yale lakini kwa mapenzi tu Mhe. MBM ali *trash*, yapo hakutana kufanya hivyo anambie Mhe. Waziri ni lini mimi nafahamu kuwa leo ameanza, nilini Kiwanda cha Uchapaji kimeanza kuchapisha Gazeti la Zanzibar leo hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwemyekiti Mhe. Said Soud Said alilieleza vizuri jambo hili, na kwa sababu ya muda sikupata nafasi ya kulieleza lakini kuanzia jana Kiwanda kilianza kazi ya uchapishaji, magazeti naomba Waziri ni hili hapa lililotoka leo. La Zanzibar Leo Mungu akitujalia nia na dhamira ni kuendelea na uchapiji huo, sawa na shughuliza kibiashara zinakwendaje na linasaidia hivi kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti nashukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Abdalla Diwani

Mhe. Abdalla Maulidi Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimefurahi kuwa Mhe. Waziri kakiri kwamba kopi ya mwanzo imekuja kutoka leo tofauti na Mhe. aliopita kuchangia hoja na tuendelee ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea fungu hilo linakubaliwa.

Wajumbe: Ndio

Jumla Kuu	Programmu Kuu ya Usimamizi wa Upigaji Chapa	2,068089,000
Kifungu PC0104	Programmu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.	
Kifungu SC010401	Programmu Ndogo ya Uongozi na Utawala	1,129,794,000

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, hapa palipo uongozi na utawala najua pana mshahara mpaka wa Waziri...

Mhe. Mwenyekiti: Pana mambo yote ya mishahara na mambo yote.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii. Mhe. Spika, nilipokuwa nachangia nilionesha kutaka kujua suala la mafuta nimekamata hapa kama niko *wrong* niambiwe.

Mhe. Mwenyekiti: Nikikaa hapa uni-*refer* kama Mwenyekiti tuko kwenye kamati ya Matumizi.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Sawa Mhe. Mwenyekiti, kama niko *wrong* nakubali kukoselewa. Sasa nilipokuwa nachangia nilisema suala la mafuta na gesi asilia.

Nilisema Mhe. Mwenyekiti naomba niseme kidogo. Tumeshuhudia kazi kubwa nzuri inayofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuhakikisha kutaka kuyachimba mafuta yetu. Kazi aliyofanywa Makamu wa Pili kaeleza uzuri, Mhe. Mwanasheria Mkuu kaeleza vizuri lakini pia tumeshuhudia kauli za viongozi mbali mbali wa Tanzania Bara kuhusu suala la

mafuta. Sasa hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, ipo hapa, nikasema lini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakaa na Serikali ya Muungano kuandaa Mswada wa kupeleka kule kuliondoa katika orodha ya masuala 22. Suala la mafuta la gesi asilia, tusikae tukasubiri Katiba mpya.

Kama haijapita jee, tukaliondoa. Nimeambiwa kuna Sheria imeundwa lakini imeundwa, sheria si Katiba na tumewasikia viongozi juzi wanasema wazi wazi, madamu limo ndani ya Katiba na Mwanasheria Mkuu kasema lipo katika mbio za kuondolewa, lakini lini litaondolewa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Hassan Khamis Hafidh na nadhani na yeye ufafanuzi ambao tumeutoa ameusikia na ameridhika nao. Nimjibu kama ambavyo nimemjibu Mhe. Mwenyekiti, kama tunaendelea kuhakikisha kuwa suala hili linaondoka kabisa kwenye orodha ya mambo ya muungano.

Na nilisema ama litaondoka kupitia Katiba hii iliopo sasa hivi au litaondoka kupitia Katiba mpya ambayo imependekezwa, lakini jambo hili Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshalitolea uamuzi na Baraza hili la Wawakilishi tayari nalo likaazimia mambo hayo hayo. Kwa hivyo kwa Zanzibar jambo hili lishamalizika Mhe. Mwenyekiti, lililobaki ni utekelezaji wake. Nakushukuru

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, najua Mwanasheria Mkuu si mwanasiasa ni mtaja vifungu vya sheria. Sasa suala langu lipo *very easy na very simple* yeye ndio aliyesema suala hili lipo kabla Dkt. Ali Mohamed Shein hajaingia madarakani na suala langu *is very simple question.*

Lini tangu Dkt. Shein hajaingia madarakani mpaka sasa hivi, ina maana mpaka kaingia sasa hivi karibu ni mwaka wa saba au wa nane, suala hili bado lipo. Hoja yangu aniambie lini mwaka huu, mwakani, mwaka kesho, mtondogoo. Hivyo tu basi naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Unayo tarehe Mheshimiwa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Sisi sote ni sawa sawa na yeye. Ukitaka hili litoke jana wala sio leo. Sasa tarehe ni lini. Mhe. Mwenyekiti, sina la kusema kweli.

Mhe. Mwenyekiti: Tarehe hawezi kuwa nayo, Mheshimiwa acha tuendelee.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mheshimiwa namruhusu tuendelee kwa sababu kakiri kwamba hana tarehe. Kwa hivyo hajui ni lini na tuendelee kwa kukiri kwamba hajui.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa rafiki yangu Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf

Mhe. Nadir Abdu-latif Yussuf: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakwenda kidogo kidogo hivyo hivyo unavyotaka wewe.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sasa hivi nakwenda kwenye lila swali la Polisi. Maana yake kule mliona Muungano ndiyo Polisi na Polisi ndiyo Muungano. Sasa nitakwenda hapa nitaomba nijibiwe. Hatua gani watawachukuliwa Polisi hawa wanaoudhi watu wanyonge.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, najua ulilijibu wakati ule, lakini naomba lijibu tena kwa faida ya Wajumbe.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, hapa kwa maana ya kifungu hakuna habari ya Polisi, kuna suala la Uongozi na Utawala wa Kusimamia Maslahi ya Wafanyakazi na Matumizi Bora ya Raslimali, ndicho kifungu kilichokuwepo hapa. Lakini nimjibu tu Mheshimiwa kwa faida ya wote.

Mhe. Mwenyekiti, hakuna askari yeyote anayeruhusiwa kumpiga mwananchi, siyo Polisi, siyo askari mwengine yeyote. Hata askari anachukuliwa hatua za kisheria anapokwenda kinyume na utaratibu. Cha msingi Mhe. Nadir kama ana ushahidi kuna mambo mawili. Kwanza anaweza kutumia utaratibu wa kisheria au anaweza kumuona Kamishna wa Polisi akatoa ushahidi wake, ama anaweza kutafuta utaratibu wa kuonana na Afisi yetu akaeleza ule ushahidi wa nani aliyefanya hivyo au yote hayo anaweza kutumia.

Mhe. Mwenyekiti, ndiyo nilipomwambia Mhe. Nadir unaweza kutumia utaratibu wa kisheria, utaratibu wa kiutawala na utaratibu wa kinidhamu, kwa maana ya kuwaona viongozi wakubwa. Mhe. Mwenyekiti, anaweza akamuona Kamishna, wewe ni mtu mzito kumuona RPC na wengineo. Muhimu aeleze Polisi kampiga wapi, tarehe na kampiga nani, hatua za kisheria zitachukuliwa kwa wahusika.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir nafikiri majibu mazuri.

Mhe. Nadir Abdu-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Waziri mzoefu hakosi la kujibu nampongeza sana.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nimesimama kulikamata fungu hili. Najua hili ni fungu la Uendeshaji, Uratibu, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kwenye mishahara nilisema kwamba nitazuia mshahara wa Mhe. Waziri katika hili. Swali langu linakuja je, Wizara yake najua inaratibu, naomba inieleze iliratibu kiasi gani na kwa kipimo kipi hata kupelekea baadhi ya nyumba kule Kianga ambazo zinasadikiwa kwamba ziko eka zimevunjwa na nyengine zimebakishwa. Wale watu wanasikitika, wengine wamekopa, miongoni mwao ni majeshi ambao wamestaafu. Lakini imeamuliwa nyumba zao zikavunjwa tu. Mimi ninavyojua hata kwenye Serikali Kuu hili jambo halipo. Je, yeye kama ndiyo mratibu aniambie ilikuwaje au wameratibu vipi mpaka ile hatua ikafikiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, hapa bado tunazungumzia suala la Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Afisi hii haijenda kuvunja nyumba wala haijagusa nyumba ya mtu yeyote na wala haina taarifa hizo rasmi kwa kuandikiwa. Sisi tunasikia kama Mkuu wa Mkoa amechukua hatua hizo. Ni vizuri Wizara husika ipo, siku itakayokuja na bajet wataeleza na pia Mkuu wa Mkoa yupo anaweza kumuuliza akapata taarifa kwa upana wake. Hili kwa sababu kila mmoja anafanya kazi katika misingi yake na mipaka yake kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana pamoja na majibu ya Mheshimiwa hii Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni Afisi kubwa. Vitu vyote vinaratibiwa pale, wana Ofisi nzima ya kuratibu shughuli za SMZ, miongoni mwa hayo. Ina maana hata kama Mkoa ulivunja basi walipasa Afisi itambue. Hayo ni mawazo yangu lakini kama sivyo hivyo Mheshimiwa utaweza kunikosoa.

Mhe. Mwenyekiti, anaratibu kwa sababu kazi yake ni kuratibu na ana Idara nzima ina ratibu mambo hayo. Sasa leo jibu alilotoa mwanzo kwamba yeye kwenye Afisi yake hajui lakini hapataki kusoma Chuo Kikuu wala darasa la kwanza, ukenda pale zinaonekana nyumba zile pale zimevunjwa nyengine zimebakishwa. Katika hilo naomba Mheshimiwa kaka yangu, rafiki yangu, mwenzangu sana aniambie jibu la serikali katika hili kwa sababu kuliko hata tukisubiri Wizara husika, lakini yeye ni mratibu wa shughuli za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nimekuwelewa lakini mimi nitatoa rai tu. Hili jambo serikali ilichukue kwa sababu kuna Wizara kweli itakuja kujieleza hapa

kwa suala hilo hilo. Lakini nyinyi kama wasimamizi wakuu basi muweze kujua kimejiri nini mpaka nyumba za watu zimebomolewa na Waheshimiwa ndio wanahoji. Hili mlichukue kwa sababu majibu kuyatoa hapa huwezi kwa sababu huna habari kama ulivyosema.

Ningeshauri hilo Mhe. Waziri nakupa na wewe ujibu juu ya hili pia.

Mhe. Waziri wa Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, mimi naheshimu sana kiti chako, naheshimu busara za Waheshimiwa Wajumbe. Kwa maana ya taarifa ya Mhe. Mjumbe kuleta kwangu nimeipokea na nitawasiliana na Wizara husika ili wajitayarishe watakapokuja hapa watoe majibu sahihi kupitia Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kifungu hicho kinakubaliwa.

Waheshimiwa Wajumbe: Ndiyo.

Kifungu SC010402	Programu Ndogo ya Mipango Sera na Utafiti	803,138,000

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia nilizungumzia suala ambalo lipo ukurasa wa 18. Kwenye wa hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais nilizungumza kwamba Afisi imeratibu utoaji wa vibali 61 kwa ajili ya kufanya tafiti zinazohusu maeneo ya mazingira, ustawi wa jamii na maeneo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kufahamu kwamba tafiti hizi zinazotolewa vibali zinaishia wapi na kama ni raia wa kigeni ambao wao wanafanya hizi tafiti, zinatunufaisha vipi sisi pamoja na serikali pamoja na wizara husika. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kuna utaratibu mzuri kwa wanaokuja kufanya utafiti.

Kwanza huomba ruhusa rasmi kupitia Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Ikisha inawasiliana na sekta husika na tukijiridhisha huwa tunamruhusu mtu huyo kufanya utafiti. Mhe. Mwenyekiti, mtafiti anatakiwa aweke ama baada ya utafiti wake alete *copy* serikalini ili kuwa na kumbukumbu za kujua aina ya utafiti na kilichoonekana katika utafiti huo. Hiyo huwa ndiyo faida kubwa na masuala ya utafiti.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza awali kwa kuwa hizi tafiti zina malengo mazuri ndani ya nchi yetu ni kiasi gani au faida gani sisi kama serikali au nchi tunafaidika na zinatumikaje na serikali mbali ya kuweka kumbukumbu. Kuweka kumbukumbu maana zinaishia kwenye mafaili ya serikali au kwenye masjala. Lakini ni faida gani ambazo serikali wanafaidika na hizi tafiti ili ziweze kutusaidia sisi katika utekelezaji wetu kwa mambo ya kila siku. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, tafiti zinazofanywa zinasaidia sana serikali, zinasaidia sana jamii, kwa kuleta maendeleo ya kiuchumi, kisiasa, kilimo, inategemea aina ya utafiti. Utafiti wowote na nchi yoyote ili ipate maendeleo inahitaji utafiti. Kwa hivyo wale wenye dhamira njema ya kuja kufanya tafiti kwa jambo zuri serikali inaona kwamba hawa wapewe fursa hizo na wanafanya hivyo na yale matokeo mazuri yanatusaidia sote. Ahsante sana.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilionesha nia ya kutaka kujua kuhusu Elimu ya Juu ambayo ipo katika Nam 14 katika orodha ya Muungano. Swali langu lipo hapa, niliuliza kwamba wana mpango gani na wana sera gani na mkakati gani wa kuona kwamba Elimu ya Juu Zanzibar inaanzia wapi. Nikauliza kwa nini hawalipwi na Muungano na imo katika orodha ya muungano. Tumezowea Usalama wa Taifa Jeshi, Polisi, Idara zote za Muungano zinalipwa na Muungano na wana mkakati gani ianzwe kulipwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza hapa hilo halipo, lakini kwa faida yake Mheshimiwa, mambo yale ambayo tunayokubaliana kuyafanya ya kimuungano tunakubaliana wenyewe kama haya tuyafanye kwa pamoja. Kwenye suala la Chuo Kikuu chetu cha *SUZA* pale awali tulipokuwa tukitumia Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam kama ndio Chuo Kikuu pekee kwa Muungano, bado fursa hizo Wazanzibari wanazitumia sana. Wale wote *lectures* pale wakitoka Zanzibar, wakitoka wapi watalipwa na Jamhuri ya Muungano. Lakini Chuo Kikuu cha *SUZA* tumekitoa kwenye shughuli hizo, ni chetu wenyewe, tunakihudumia wenyewe, tunafanya tunavyoona inafaa, tunachagua wenyewe ma-*lectures* na wengine. Kwa hivyo hichi ni chetu tunakihudumia wenyewe, kama tukitaka leo tukiunganishe na Chuo cha Dar-es-salaam tutapata fursa hizo, lakini tusitegemee tena kuwa atakuja yule unayemtaka wewe awepo pale. Mhe. Mwenyekiti, utachaguliwa kwa utaratibu wa uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. Ahsante.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri Mhe. Waziri mzoefu. Hoja yangu ni Elimu ya Juu, sisemi kuchanganywa hapana, chetu lakini kunako kero za Muungano ni Elimu ya Juu. Sasa hoja yangu ipo hapo, hizi Taasisi za Elimu ya Juu kwanza zinaanza wapi na kwa nini hazilipwi na Muungano. Kulipwa na Muungano haina maana kuwa sio chetu. Uhamiaji wapo hapa wanalipwa na Muungano na wetu, wanaripoti kwa Mamlaka ya Zanzibar. Sasa haina maana kwamba hawalipwi na Muungano sio wetu. *No that's not the point*. *Point* yangu kwa nini hawalipwi na muungano, bado kitakuwa chetu vitu vyote vya Muungano vipo hapa Zanzibar na vinapokea amri ya Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ningependa Mhe. Hassan afahamu Uhamiaji hawaripoti kwa SMZ. Ila wanaheshimu utawala tu, wanafanya kazi kwa misingi ya Jamhuri ya Muungano. Polisi hivyo hivyo, *TRA* hivyo hivyo tofauti, wanaajiriwa kwa utaratibu wa Jamhuri ya Muungano. Hivi vyetu sisi tunavyovianzisha tumevitaka wenyewe kwa utaratibu wetu na kwa maslahi yetu ya Zanzibar. Kama kuna ushauri mwengine Mheshimiwa anao kwamba Vyuo vyetu na taasisi zetu zote tuziunganisha kwenye Jamhuri ya Muungano basi atushauri na Baraza hili liamue. Lakini utaratibu wa sasa tunauona ni mzuri, unasaidia taasisi zetu na mambo yetu. Ikiwa kama ana ushauri anatupa ili tutumie fursa zaidi ya Muungano tunaupokea.

Mhe. Mwenyekiti: Nashawishika sana kumnyanyua Mwalim Haroun.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, suala ni zuri lakini labda nitoe historia kidogo ya kuanzishwa *SUZA*.

Mhe. Mwenyekiti: Nakuruhusu Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Sheria ya *SUZA* ilianzishwa mwaka 1999 na tukaipitisha kwenye Baraza la Wawakilishi wakati ule kwenye Baraza la zamani liliopo pale Mnazi Mmoja. Wakati Rais Amani anaingia kwenye Madaraka mwaka 2000 akaniteuwa mimi nikawa Waziri wa Elimu. Tukashauriana kwamba sheria imeshatungwa ni tatizo gani kwamba mpaka leo hatujaanzisha Chuo Kikuu. Mhe. Mwenyekiti, akaniuliza tunaweza? Nikamwambia tunaweza kwa nini tusiweze. Chuo Kikuu hakihitaji kuwa *sky scraper* kwa maghorofa 20 au 30, ni majengo ya kawaida, uwe na walimu na vifaa tu basi. Ndio tukaanzisha

Faculty ya *Education*, yaani tukaanza na *faculty* ya ualimu tu tena tukaanza na masomo ya Kiingereza na Kiswahili.

Mhe. Mwenyekiti, Elimu ya Juu tafsiri yake ni masomo ya elimu ambayo yanayoanzia *degree* ya kwanza na kuendelea, lakini inategemea utakavyotafsiri. Mtu aliyemaliza darasa la saba elimu ya juu kwake yeye inaanzia *form one* ndiyo zaidi ya pale inategemea vile utakavyoitafsiri. Lakini elimu ya juu yetu sisi ni suala zima la *university education* na kuendelea juu, *degree* ya kwanza, ya pili ya tatu mpaka unafika unapomaliza.

Mhe. Mwenyekiti, suala la msingi ni kwamba jambo lipo la Muungano lakini *in good will* tulifanya mazungumzo kati yetu sisi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Waziri anayehusika wakati ule alikuwa ni Dkt. Pius Luwando. Tukazungumza kwamba tuanzishe Chuo Kikuu. Mhe. Mwenyekiti, yakaja maswali, mtaanzishaje na kwamba suala hili ni la Muungano. Bahati nzuri sana kwa maelewano mazuri ya Waziri na Rais mwenyewe akazungumza na mwenzake tukakubaliana na ikaonekana kama Tabora, Mwanza, Dodoma wameanzisha Vyuo Vikuu, kwa nini Zanzibar tusianzishe Vyuo Vikuu na vipo hapa hapa Tanzania. Kwa hivyo tukaweza kuanzisha Chuo Kikuu.

Mhe. Spika, lakini kama hilo halitoshi nikurudisheni nyuma kidogo hata haya masuala ya michezo Zanzibar. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri na timu yake yote ya Wizara ya Utamaduni na Michezo. Masuala ya Michezo, shirika au Taasisi inayotambulika ni *TFF* wakati ule ilikuwa inaitwa *FAT*.

Mhe. Mwenyekiti, wakati ule tulipokuwa tunaomba ruhusa hatushirikishwi katika mashindano ya Klabu Bingwa ya Afrika mwaka 2003. Zanzibar ilichukua muda kidogo na tumeomba siku nyingi haya mambo. Lakini 2003 tukaruhusiwa tuwe washiriki kama ni *observers* katika mashindano ya Klabu Bingwa. Zanzibar ikawa inashiriki, inakwenda na bendera na wimbo wa taifa unapigwa kwa timu ya Zanzibar kwa vilabu.

Mhe. Mwenyekiti, leo hii tumepata faraja kubwa timu yetu ya taifa sasa nayo itashiriki kikamilifu kama Zanzibar. Masuala ya muungano kuna mambo *in good will* huwa tunafahamiana katika serikali zetu mbili. Jambo lolote hakuna lisilowezekana. Kama suala la mafuta limewezekana kulitoa kwenye muungano hakuna sababu na mambo mengine tusiweze kuyazungumza ni utaratibu tu. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana lakini leo kwa kupata darasa. Kweli mwalimu ni mwalimu. Lakini nimesikitishwa kidogo na kauli ya Mhe. Waziri kuniambia kwamba chombo cha Uhamiaji kwamba hakiripoti katika mamlaka ya Zanzibar. Hoja yangu kwamba yeye akimwita Kamishna wa Uhamiaji hawezi kwenda.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hilo kalitoa kama mfano siyo hoja. Sasa usiende kwenye jambo jipya ungerudi kwenye lile lile na hapo hiyo ni nafasi yako ya mwisho, yaani ukimaliza hapo tunaendelea.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Sawa, sasa nimefahamu lakini ninavyojua mimi kwamba vyombo vya Muungano vilivyokuwepo hapa Zanzibar bado vinaripoti katika Mamlaka ya Zanzibar. Lakini kwa kuwa yeye ni Waziri anajua zaidi sina pingamizi na hilo. Naomba tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu SC010402	Programu Ndogo ya Mipango Sera na Utafiti	803,138,000
Kifungu SC010403	Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba	635,858,000
	Jumla Kuu	**2,568,790,000**
	Jumla Kuu ya Fungu	**22,964,277,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU C02 - BARAZA LA WAWAKILISHI

Kifungu PC0201	**Programu Kuu ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali**	
Kifungu SC020101	Programu Ndogo ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali	6,595,520,000
	Jumla Kuu	**6,595,520,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PC0202 Programu Kuu ya Uongozi na Utawala Baraza la Wawakilishi

Kifungu SC020201	Programu Ndogo ya Uongona na Utawala Baraza la Wawakilishi	916,932,000
Kifungu SC020202	Programu Ndogo ya Afisi Kuu Pemba	349,248,000

Mhe. Nadir Abdu-latif Yussuf: Mimi nilikuwa naomba kujua ni lini Baraza hili tutaweza kufanya vikao Pemba badala ya Unguja kwa baadhi ya siku.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kufanya vikao Pemba inategemea na mazingira ya jengo liliopo Pemba. Kutokana na hali ilivyo ya jengo kwa sasa si rahisi kufanya vikao Pemba. Huko nyuma tulifanya wakati jengo lilipokuwa katika hali nzuri. Sasa hivi linahitaji matengenezo makubwa.

Mhe. Mjumbe kwa taarifa yake tumefanya tathmini gharama ni kubwa kwa kulitengeneza jengo lile na kurudisha katika hali ya ukawaida wake. Uwezo utakapowezekana katika miradi yetu tutakayopanga ya kimaendeleo kwa mujibu wa *priorities* zetu, basi tukimaliza matengenezo hayo tunaweza tukafanya mikutano Pemba.

Jumla Kuu	Programu ya Uongozi na Utawala Baraza la Wawakilishi	12,066,180,000
Jumla Kuu	**Fungu C02 Baraza la Wawakilishi**	**18,661,700,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU C03 - TUME YA UCHAGUZI

Kifungu C0301	Utawala Unguja	455,000
Jumla Kuu		**455,000**

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU C03 - TUME YA UCHAGUZI

Kifungu PC0302	Programu Kuu ya Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi Zanzibar.	
Kifungu SC030201	Programu Ndogo ya Uendeshaji wa Shughuli za Kiutawala wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar	1,477,750,000
Kifungu SC030202	Programu Ndogo ya Uendeshaji wa Shughuli za Kiutawala Tume ya Uchaguzi Pemba	217,750,000
Jumla Kuu	Programu ya kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi Zanzibar	1,695,500,000
Jumla Kuu	**Fungu C03 Tume ya Uchaguzi**	**1,695,500,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU C04 - TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA MADAWA YA KULEVYA

Kifungu PC0401 Programu kuu

Mhe: Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mwenyekiti katika mchango wangu niligusia juu ya 1.4 bilioni kwa ajili ya nyumba ya kurekebisha tabia madawa ya kulevya kule Kidimni. Ni ukweli usiofichika kwamba zile pesa ni nyingi zaidi nyingi na hivi sasa zimeombwa pesa nyengine za milioni 695,000,000. Nitaomba sana Mhe. Waziri anipe ufafanuzi wa kina juu ya pesa hizi za 1.4 bilioni matumizi yake ili niliombe Baraza hili tena liidhinishe fungu hili ambapo mna Shs.695,000,000 kwa ajili ya ile nyumba.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, anachosema ni 1.4 bilioni tunachozungumzia hapa ni fungu hili lote lote mpaka jumla kuu ni 598,900,000. Sasa sioni 1.4 bilioni hapa nitaitolea maelezo vipi.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante hii nyumba imeanza kuanzia 2011 bajeti yake imekuja mpaka 2014 na hata 2015/2016 tulikuta kiasi hiki cha 1.4 bilioni na hata katika majumuisho yake Mhe. Waziri alitaja hii nashukuru masikio yangu mazuri alitaja pale la kama hajaitaja basi twende, lakini kama kaitaja 1.4 bilioni tayari ile nyumba imetumia na ndio maana nikataka aniambie kutokana na zile pesa zilivyokuwa 1.4 bilioni. Ningepewa mimi ningejenga

ghorofa zisizopungua nane sasa ile nyumba ambayo ni ghorofa moja nasikia bado haijapandishwa au inapandishwa sasa hivi kutumia 1.4 bilioni vipi imekuwa nataka ufafanuzi Mheshimiwa wala si makubwa katika haya.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri sijui una maelezo zaidi

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Malezo Mheshimiwa kilichotakiwa kusema ni thamani ya jengo lile ambalo zimetumika muda mrefu uliopita, si mwaka huu. Kwa msingi huo hapa mimi siziombi hizo wala sizitaki. Sasa kama kuna ripoti yoyote ya *CAG* au nini ya uchunguzi wowote wa Baraza kwenda kuchunguza ni ruhusa.

Lakini hapa siwezi kutolea ufafanuzi utolewe. Ufafanuzi kuhusu kifungu kipi hatuombi hizo pesa hapa wala hatuzihitaji hapa. Sasa kama kuna tatizo lolote Baraza linaweza kuamua linavyoona linafaa kuhusu kuchunguza thamani yenyewe na ujenzi uliopo ruhusa. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa nafasi hii najua Mhe. Waziri anaruka kimanga hili suala. Lakini anaruka kimanga halitaki, samahani nikisema hivyo kama nimemkwaza hapo, samahani tena naomba niombe radhi.

Lakini hii taasisi mwanzo ilikuwa kwa Makamu wa Kwanza wa Rais, baada ya harakati ya kumalizika uchaguzi ina maana mzigo wote umekwenda kwenye Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, bado fungu letu wanalo awe na fedha tulimuidhinishia, mimi sina makubwa mimi anipe hesabu lakini kaniambia hesabu haipo basi. Hapo ningeomba kiti chako Mhe. Mwenyekiti, tukazifanyia uchunguzi kule kwa sababu hizi pesa ni nyingi lakini ufanisi wake haupo ni pesa za wavuja jasho, hasa tukisema twende tu humu washatumia 1.4 bilioni iwe hamna chochote, iwe maana jumba mpaka sasa hivi hamna chochote wala halijamaliza 1.4 bilioni na tayari anaomba pesa nyengine kwa ajili ya kitengo chake, pengine anajua ataziingiza kule kule pesa nyengine.

Sasa ningeomba na wewe unisaidie sana Mhe. Mwenyekiti, katika hili. Mimi siko tayari kulikubali kwa sababu ya zile pesa za wavuja jasho wa nchi hii. Mwenzangu anapenda sana kutumia wakwezi na wakulima, mimi nasema za Wazanzibari. Hebu naomba ufafanuzi wake la kuna sababu tuunde Tume tukakaguwe ile sehemu tujiridhishe halafu baadaye tuendelee na masuala mengine.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe kama sasa hivi tunapitisha mafungu hatuchangii tena, kama

kuchangia tumeshachangia na utaratibu wa kupitisha mafungu kuna programu kuu na kuna programu ndogo, ndiyo fungu linaloombewa hilo la fedha. Sasa Mhe. Abdalla Maulid Diwani kama ana hoja yeye pamoja na wengine wote watakuwa na hoja kwenye fungu kuu na programu ndogo yake ambayo inaombewa wapige buti kwenye maeneo hayo, tena wapige wanavyotaka ni haki yao kufanya hivyo na wala sisi hatutowazuia.

Lakini si sahihi Mhe. Mwenyekiti, kusimama kupinga hoja kwenye programu ambayo hata fedha yake haiombewi. Sasa hivi ndio ambalo Mhe. Waziri amelitolea ufafanuzi. Sasa niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe kama watizame programu ndogo ambazo zipo na fedha ambayo inaombewa kwenye programu kuu. Halafu wapige buti wanavyotaka kama haipo tusikae hapa mpaka usiku kwa jambo ambao halimo kwenye programu kuu wala programu ndogo. Niwaombe hivyo sana Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nilichangia nasema kwamba wanaoleta unga, wasambaji wa unga na sio hao tu hata wabakaji, majambazi na mashoga wanyongwe. Sheria iwekwe ya kunyongwa lakini sasa Mhe. Waziri alipokuja kujumuisha anasema yeye haoni kwamba ni lazima Sheria hiyo kwamba kunyongwa ni nzuri, yaani tufuate hii iliyokuwepo inatosholeza. Sasa nimuulize Mhe. Waziri anijibu vizuri yeye ana uzito gani wa mtu kunyongwa kwa mtu ambaye amefanya mambo haya. Kwa nini tunafika kuachia kwa sababu mtu atakapokuwa hawekewi kesi ya kunyongwa anao uwezo wa kutoroshwa baadae.

Mhe. Mwenyekiti, atakapokamatwa mtu kwenda kuwekwa ndani baadae huko baada ya miaka mitano akafanyishwa anaumwa apelekwe wapi anatoroshwa, zimeshatumika nyingi duniani mtu kunyongwa. Mimi anipe sababu kwani hataki watu wanyongwe.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Nadir hoja yake ambayo anaijenga. Kwanza nimwambie haki ya kuwa hai ni haki ya Kikatiba, imelindwa na Katiba haki ya mtu kuwa hai. Hilo la kwanza.

Lakini la pili sina kumbukumbu za hukumu ambazo zimetolewa za watu kunyongwa lakini nina kumbukumbu za hukumu za vifungo vya maisha. Kwa hivyo nimwambie Mhe. Nadir inawezekana hoja yake alivyoiona yeye ni nzuri lakini pia nimwambie haki ya kuishi na haki ya kuwa hai ni haki ambayo inalindwa Kikatiba. Na hili Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe wanajua ni *debate* kubwa sana, *it is a very huge debate* kwa wale ambao wanazungumzia kunyongwa na wale ambao wanazungumzia haki ya mtu kuwa

hai. *It is a very huge debate* na mimi nisingeomba tuchukulie *very smooth.* Nizungumze hayo na nimwambie kama haki hii kwa sasa inalindwa Kikatiba.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kabla hujaendelea labda na mimi niongezee kidogo katika maneno mazuri ya Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Suala la hukumu ni suala la Mahakama, wanachoweza kufanya wao hao hawa, yaani ile nje niliyokueleza tuna mashaka na mtu madawa ya kulevya tunampeleka kwenye vyombo vinavyohusika atapelekwa mahakamani, mahakama ndiyo itakayoamua kama huyu ana hatia na kwa kosa hili anastahiki adhabu ipi. Lakini Waziri tukimtaka hapa sasa hivi aeleze kwa nini watu wasinyongwe tunamuonea. Kwa sababu hicho kiko nje ya uwezo wake wa kazi, nje ya mipaka yake ya kazi kwa sababu hukumu ni suala la makahama si suala la Waziri. Kwa hivyo nafikiri kwa sababu tusipoteze tu wakati. Sasa nakupa hiyo nafasi Mheshimiwa tena.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, jambo hili linawezekana tukalipitisha sisiWawakilishi lakini wizara yake ndio husika ilikuwa pia ikubali katwambia basi na nyinyi shirikianeni mupitishe. Kwa sababu Sheria za *Human Rights* za mtu asinyongwe ni Sheria za kikafiri tunazozifuata sisi. Sheria tunazozitaka sisi zetu wenyewe tutunge wenyewe, tunyonge mtu kwani tunaweza. Mimi naomba akubali tu.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilipochangia nilionesha nia. Mhe. Mwenyekiti, nakubali kukosolewa katika hapo kama nitakuwa nakosea kwa hichi ninachokisema.

Mhe. Mwenyekiti, tumekwenda kuiangalia nyumba na pesa zilizotajwa zimetumika hazifanani na ile *value for money.* Sasa hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, iko hapa...

Mhe. Mwenyekiti: Unarudi kwenye nyengine ya Mhe. Abdalla Diwani au vipi.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ndio maana nikasema nakubai kukosolewa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Hapana kwa sababu tushaizungumza hapa tushamalizana nayo.

Kifungu SC040102	Programu ndogo ya Kupunguza Mahitaji ya Matumizi ya Dawa za Kulevya	76,612,000

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti mimi nitaendelea kwenye hoja nyengine kwa kuwa wanaeleza kwamba wanadhibiti na *Airport* na masuala ya bandari, kwa kuwa wameweka vidhibiti vya madawa ya kulevya Bandarini, *Airport* na maeneo mengine .

Ningependa kujua kwa sababu kuna taarifa mashine zilizokuwepo *Airport*, hazina uwezo mkubwa hasa mara kwa mara kuweza kugundua masuala ya unga. Mashine zilizokuwepo pale haziko kabisa kwenye kiwango ni mashine ambazo sio nzuri na watu hufika wakati huondosha mbwa wakati wa kupitisha watu unga. Ningependa kujua Kitengo cha Madawa ya Kulevya wana mbwa wangapi wa kunusa madawa ya kulevya na mashine ngapi ambazo wameziweka katika kila maeneo hayo waliosema na muda gani wanaweka kwa sababu wanapelekwa kwa muda na wakati mwengine huondoshwa mbwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hiki ni Kupunguza Mahitaji ya Matumizi ya Dawa za Kulevya ni *Sober*, nadhani kama nitakuwa sikosei cha mwanzo huko ambacho kishapita ni Kudhibiti Uingizaji na Usambazaji wa Dawa za Kulevya. Nafikiri hapo ndio pangekuwa pahali pake.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana na mimi kama alivyosema rafiki yangu niko tayari kukoselewa kwa sababu hilo fungu kubwa mimi silijui liko wapi wala dogo liko wapi. Hoja yangu naipitisha tena hapa niko tayari kukoselewa kama nimekosea niambiwe.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa hoja yako ihusiane na hiki ndio mpe Mhe. Waziri ushamuelewa

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa lakini hapa kazi yetu kupunguza Mahitaji ya Matumizi ya Madawa ya Kulevya. Msingi wake kila yeye akifurahia kujenga maana yake yeye anafanya kazi hiyo ya kupunguza madawa ya kulevya.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Sawa sawa nakubali sana. Sasa mimi ninacho *complain* sikatai kujenga zile gharama za ujenzi wa kile kitu chenyewe ndipo palipo na hoja yangu. Hoja huku nyuma tumeipitia mpaka tulipofikia nyuma kuna 1.4 bilioni ujenzi wa ile nyumba ya kule Kidimini. Ndio haihalisi na hizo zenyewe. Pesa nyingi sana lakini nyumba haipo ya pesa hizi kulikoni. Ndio maana pale nikasema kwamba basi tutafute kitu hata nifahamishwe mpaka nifahamu 1.4 bilioni kwa pale Kidimni zimetiwa wapi.

Mhe. Mwenyekiti: Nimekulewa Mheshimiwa na Mhe. Waziri kakuelewa. Mhe. Waziri naomba majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza hapa hizi hasa ni ule msaada wa *Sober House*. Hata huku Kidimni hatujaanza kazi ya kwenda kufanya hiyo tathmini kwa sababu hatujamaliza hata ujenzi wenyewe. Kwa hivyo Kidimni haiwezi kuwa *operational* ikafanya kazi kama hizi za kupunguza kama hujamuongezea. Hapo itakapokuja tukapata tunaongeza. Mimi nilichoshauri Baraza lako kama kunaonekana kuna matatizo *value for money* kwenye ule ujenzi, kuna *CAG*, kuna kamati zinaundwa Mheshimiwa. Lakini hapa hatuzungumzii lile, hatuna haki hiyo hapa. Kwa hivyo sasa sisi tumelipokea hili shauri kwa utaratibu wa kiserikali tunamtuma *CAG* akangalie uwezekano unaoonekana unafaa.

Lakini si kwa hapa, hapa akisema hii hatuna *right* ya kufanya. Mheshimiwa lazima sisi tunafundishwa kila siku namna ya kupitisha kifungu utaratibu wake huo ninauheshimu.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa nimekuelewa mimi. Ningekushaurini Serikali, hebu litizameni hili swali, mtumeni huyo *CAG* akaangalie halafu baadae tuleteeni habari tu hapa mtueleze kilichojiri. Hakuna haja tena sisi kuanza kuunda Tume na vitu gani, fanyeni nyinyi wenyewe Serikali halafu njooni mtwambie sawa.

Jumla Kuu	**Programu Kuu ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya**	**151,775,000**
Kifungu PC0402	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Tume ya Dawa za Kulevya	
Kifungu kidogo SC040201	Programu ndogo ya Utawala na Uendeshajiwa Dawa za Kulevya	377,761,000

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeomba lile suala langu sasa nijibiwe hapa la mbwa wangapi waliokuwa nao na mashine ngapi.

Mhe. Mwenyekiti: La mashine na mbwa. Mhe. Mjumbe umuhimu ni kwamba uwe makini pale pahali panapohusika ndio ulilete.
Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Wakati mwengine utakuta watu wanainuka wengi atujibu tupate faida.

Kifungu PC0402	Uendeshaji na Uratibu	
Kifungu SC040202	Programu Ndogo ya Kuratibu Shughuli za Tume ya Dawa ya Kulevya Pemba	69 362,000
Jumla Kuu	Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Dawa za Kulevya	**477,123,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU C01 – MIRADI YA MAENDELEO
OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Kifungu PC0102	Programu Kuu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali	
Kifungu SC010201	Programu Ndogo ya Kukabiliana na Maafa	794,950,000

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, mimi suala la maafa nilizungumza kwamba jimboni kwangu Chaani kuna sehemu zimeathirika na kuna nyumba zimevunjika na watu wameingiliwa na maji. Sasa ningependa kujua wizara yake walipopita kote kufanya utafiti kwa wale ambao hutoweza kuwasaidia, tayari jimbo langu wameshafika na lini wataweza kuwasaidia kwa mujibu wa ratiba zao kwa upande wao mbali ya upande wangu mimi, maana yake naweza nikaja nikaingizwa na mimi nataka nijue upande wao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ningependa alirudie hilo suala lake sikulisikia vyema.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, mimi kutokana na maafa yaliyotokea naamini Tume ya Maafa imeshatembelea sehemu nyingi kuwakagua watu waliopata maafa. Sasa je, jimbo langu mimi kumetokezea maafa ya mvua watu wamevunjikiwa na nyumba na masuala mengine. Je, Tume hiyo jimbo langu imeshafika na lini wataweza kuwasaidiwa kwa upande wenu sio upande wa Mwakilishi. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Umemuelewa nafikiri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kutokana na hali ya mvua kumetoa maafa sehemu mbali mbali na watu kufanyiwa tathmini katika Kitengo cha Maafa wamekuwa wameshughulika kufanya kazi hizo na taarifa zote za waliofanya tathmini zipo na sasa kumetolewa utaratibu maalum kupitia Kamati hii ya Kukabiliana na Maafa

kuna maelekezo kupitia msaada utakaopitia katika Serikali za Mikoa, na kupitia Mikoa watawasiliana na wenzao wa Wilaya kupata tathmini hiyo na kila mmoja ataonekana nani asaidiwe nini kupitia Kamati hizo za Mikoa na Wilaya. Kwa hivyo naamini kama wapo watu ambao wataonekana kumefikia kile kiwango cha kuhitaji kusaidiwa kwa maana ya vigezo vilivyowekwa na serikali basi watasaidiwa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana.

Kifungu SC010201	Programu Ndogo ya Kukabiliana na Maafa	794,950,000
Kifungu SC010203	Programu Ndogo ya Shughuli za SMZ, SMT, Utafiti na Masuala ya Muungano	13,068,827,000
Jumla Kuu	Programu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali	13,863,777,000

Mhe. Suleiman Makame Ali: Nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mwenyekiti, sina nia ya kumkwaza rafiki yangu Mhe. Waziri kwenye suala hili, lakini nataka nimuulize kidogo nipate ufafanuzi hapa, nadhani ni kwenye kaya maskini kwenye fungu hili hapa. Nilipokuwa nikichangia nilizungumza kwamba kuna baadhi ya maeneo wananchi wetu ambao serikali ina nia njema kabisa kwa kuwapatia wananchi pesa za kaya maskini, lakini kuna baadhi ya maeneo zile pesa hawazipati kama inavyopaswa wanakatwa mikato ya ajabu ajabu.

Vile vile kuna baadhi ya maeneo wengine hizi pesa wananyimwa kabisa na kutishiwa tishiwa. Kwa hivyo nataka nijue kwenye hizi pesa zinazokuja je, wizara itahakikisha wanazilinda vipi ili zionekane zinafika kwa wale walengwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Suleiman Makame Ali kwa swali lake hilo inabidi tufanye utafiti zaidi kwa sababu taarifa hizi ambazo yeye amezisema, tulifanya tathmini baada ya kupata taarifa ya upotevu wa fedha hizi za Mradi huu wa *TASAF* na tukafuatilia. Kwa bahati nzuri kwa upande wa Unguja na Pemba matatizo yalikuwa madogo ukilinganisha na wenzetu kwa Tanzania Bara na wale ambao walionekana wanakwenda kinyume na taratibu wameondolewa katika nafasi zao na taratibu nyengine za kisheria zitafuata. Kitu cha msingi ni haya maelezo ya Mhe. Suleiman itabidi tufuatilie zaidi kwa sababu jambo kubwa hapa ni kupata wale wanaolalamika kwa sababu anajua yeye jimbo lake ni lipi

atatwambia Shehia gani ambayo anaona yapo matatizo hayo ili watu wetu wakafanye tathmini kukutana moja kwa moja na walengwa wenyewe ili kujua nani hapati fedha zake kwa mujibu wanaotakiwa kupata.

Mhe. Mwenyekiti, na wale ambao hawakuwemo kwa sababu haya mambo yalifanywa na jamii yenyewe kupitia wataalamu walipokwenda kuwasaidia, ni *selection* iliyofanywa na wananchi huko. Sasa kama yuko mtu pengine hakuwemo kwenye utaratibu, hayumo kabisa na yeye ni maskini inawezekana na maelezo aliyoyatoa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu pia tulipata tatizo kwa Pemba katika kufuatilia jambo hili wakati wananchi wakisaidiwa wengine hata waliokuwa maskini unamuuliza nyumba yako ina bati, anasema ina bati, nyumba yako ina umeme anasema ina umeme, nyumba yako ina *freezer* anasema ina *freezer*. Sasa ukishajibu masuala kama hayo unakuwa *disqualified* yule, akiondoka anasema eeh! hanioni mimi nyumba haina hata kuti ile nitaweza kutia bati.

Sasa mambo kama hayo inakuwa hukutoa ile *information* sahihi. Matokeo yake unakuwa *disqualified***.** Kwa hivyo tunatafuta uwezekano wa ku-*review* pale ambapo wengine sasa wata-*qualify* kuondoka ili tuwatizame wale ambao wanapaswa kupewa. Tutachukua hadhari zaidi ili kuona namna lakini tutalifuatilia hili suala ambalo kwa nini upate pesa kasoro na kuna utaratibu wa kupata kamili. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba tuendelee kwa roho safi kabisa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nishukuru kwamba jimbo langu wamefaidika Shehia tatu. Shehia ya Bandamaji, Shehia ya Masingini na Shehia ya Kinyasini aliyoitaja Mhe. Naibu Waziri. Sasa mimi nina Shehia nane na tayari wenzao wa Shehia tano zilizobakia zilizokuwa hazijafaidika na *TASAF* wameshaona choyo tayari. Ni lini sasa hizi Shehia tano mtawapelekea maendeleo ya kusaidia kama mlivyosaidia hizi Shehia tatu mwanzo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli suala la Mhe. Mwakilishi lina ugumu kujibika kwa sababu kwa sasa tayari wale wanaendelea kufaidika wanafaidika na pale wale wengine watakao-*qualify*, sasa wakitoka kwenye huu mpango ndio tunaanza ile *phase* ya wale ambao wengine wenye mahitaji hayo. Lakini niseme tu kwamba mradi huu umefanya kazi kubwa mpaka kufikia Machi, 2017 zaidi ya bilioni 18.1

zimetumika katika kusaidia wananchi, kwa maana ya ruzuku, miradi ya jamii na kadhalika. Kwa hivyo ni mradi muhimu sana ambapo tunapaswa tusaidie sana wananchi wetu wale wanao-*qualify* waweze kuondoka na wengine waweze kupata. Hata hivyo tutawafikiria kama upo uwezekano wa kuongeza katika Shehia nyengine kwa upande wake kama fedha ipo tutatambulisha mheshimiwa. Ahsante sana.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, mimi ushauri tu ni vyema basi kama ingekuwa fedha nyengine zinakuwa bado, basi hizi milioni 218,000,000 walizozitoa kwa Shehia tatu wangezigawa kwa Shehia nane wakapata wote japo kidogo kidogo halafu zitapokuja nyengine wakaongezewa tena kuliko kuwapa watatu wakakosa watano. Ahsante sana.

Jumla Kuu	Programu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali	13,863,777,000
Kifungu PC0104	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais	
Kifungu SC010402	Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti	500,000,000

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, mimi kidogo nimesimamia wananchi sasa hivi na kuna malalamiko kidogo kwamba wenzetu madereva wa serikali kwa sababu ni utawala wa Mawaziri na Manaibu Waziri wanapokaa muda mrefu nje ndani ya Baraza la Wawakilishi hawapati chakula kwa muda wote, baadhi yao kidogo tu husaidiwa chochote. Sasa wanataka kujua kuna posho yoyote wanasaidiwa au vipi? Kwa sababu…

Mhe. Mwenyekiti: Samahani mheshimiwa wakati wa mchango wako ulili-*raise* hili?

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Yamo yote haya.

Mhe. Mwenyekiti: Naam!

Mhe. Abdul-latif Yussuf: Yote yamo labda alisahau Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Naam!
Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Yote yamo mimi napiga *remix* yote yamo alisahau tu Mhe. Waziri walilalamika kwamba hawapati posho…

Mhe. Mwenyekiti: Aah! Yaani uliwasemea ulipokuwa ukichangia?

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Nilizungumza.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, hili jambo hakuli-*raise* Mheshimiwa lakini niseme tu madereva wa mawaziri wana posho zao za udereva. Mheshimiwa hata sisi tukiwa hapa hakuna chakula tunachopewa hapa lazima pale tunapopata *break* tunakwenda kula, na tunapokwenda kula tuna utaratibu wetu wa kukaa na wenzetu na kadhalika. Kwa hivyo, mfanyakazi wa umma kuna utaratibu wa utumishi wa umma lazima awe nazo. Mimi nadhani wanafanyakazi nzuri madereva wetu pale wanapopaswa kufikiriwa kwa lolote basi serikali inafanya hivyo na sisi wenyewe binadamu tunajua tunavyokaa nao. Ahsante sana.

Kifungu SC010402	Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti	500,000,000
Jumla Kuu	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais	500,000,000
Jumla Kuu		**14,363,777,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU C05 – TUME YA UKIMWI

Kifungu PC0501	Programu Kuu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa Ukimwi
Kifungu SC050101	Programu Ndogo ya Mawasiliano na Utetezi

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, wasiwe na wasi wasi hata tukitoka saa sita tunafanya kazi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachotaka kujua kwa sababu Zanzibar imeathirika sana na madanguro na wanawake wanaojiuza. Nungwi na maeneo mengi kama Mbweni hapo Matrekta, pale CCM baa na sehemu nyenginezo namshukuru sana na nampongeza sana Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi kafika yeye mwenyewe na kaiona hali.

Sasa ni lini serikali itachukua jitihada ya kutosha kwa Wakuu wa Mikoa wote na Polisi kwenda kuwabeba juu juu hawa wanaojiuza Watanzania Bara na Wazanzibari wanaojiuza pamoja na wageni wa nje wapo Nungwi, wazungu wanajiuza kusambaza UKIMWI.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, sikumsikia Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf wakati akichangia akisema hivyo, lakini ushauri mzuri alioutoa tutaufanyia kazi pale ambapo tunaona panahitaji kushughulikiwa jambo hilo tutafanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante mheshimiwa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Kwa leo Mhe. Mwenyekiti, mimi nishamaliza sipigi tena. Ahsante sana.

Kifungu SC050101	Programu Ndogo ya Mawasiliano na Utetezi	
Kifungu SC050102	Programu Ndogo ya Uratibu wa Muitiko wa Taifa wa UKIMWI	129,639,000
Jumla Kuu	Programu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI	235,044,000
Kifungu PC0502	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Tume ya UKIMWI	
Kifungu SC050201	Programu Ndogo ya Uratibu wa Masuala ya UKIMWI Pemba	183,124,000
Kifungu SC050202	Programu Ndogo ya Utawala na Undeshaji Unguja	428,632,000
Jumla Kuu	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Tume ya UKIMWI	611,756,000
Jumla Kuu		**446,800,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizibila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naafiki.
Mhe. Spika: Ahsante mheshimiwa.

Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na tuiamue wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe, nadhani baada ya hatua hiyo sasa tutakuwa tumekamilisha. Naomba nitoe shukurani zangu kwa mashirikiano ambayo tumekuwa nayo mpaka hapa tulipofika saa 3:00 lakini tumeweza kuangalia hii *trend* inavyokwenda kwa wizara zile nyengine tutajitahidi sana tuwe tunaondoka mapema. Kwa hivyo wale wachangiaji tutajaribu kwa kadri inavyowezekana tusichangie kwa wingi huo wa kuweza kufikisha wakati kama huu, hapa tumalize kwa wakati.

Baada ya maelezo hayo naomba nikumbushe tena kuhusiana lile suala la wale Waheshimiwa ambao wanataka kwenda Pemba kwamba kesho watustahamilie kwa sababu nikiwaruhusu watu wote wenye majimbo waende zao Pemba kesho Ijumaa tutakosa *quorum* humu ndani. Kwa hivyo watustahamilie halafu hizo safari aidha wazifanye jioni ya hiyo kesho Ijumaa au Jumamosi asubuhi halafu wafanye shughuli zao mpaka Jumapili ili Jumatatu waweze tena kuwepo hapa.

Baada ya maelezo hayo nachukua nafasi hii sasa kuakhirisha Baraza mpaka kesho siku ya Ijumaa saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 2:54 usiku Baraza liliakhirisha hadi
tarehe 12/05/2017 saa 3:00 asubuhi)